# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

## RIPOTI YA UTAFITI WA ENEO LA ULINZI NA UHIFADHI WA TAARIFA BINAFSI

**RIPOTI NAM. 7 /2023**

**JUNI, 2023**

**MHESHIMIWA HAROUN ALI SULEIMAN,**

**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS- KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA,**

**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA DKT. MWINYI TALIB HAJI,**
**MWANASHERIA MKUU WA ZANZIBAR,**
**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA DKT. KHALID SALUM MOHAMED,**

**WAZIRI WA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI,**

**ZANZIBAR.**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya Mwaka 1986, kwa heshima, Tume inawasilisha Ripoti ya Mapitio ya Utafiti wa Eneo la Ulinzi na Uhifadhi wa Taarifa Binafsi.

**…………..……………**

**KHADIJA SHAMTE MZEE**
**MWENYEKITI,**
**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA,**
**ZANZIBAR**

**28 Juni, 2023.**

## MAKAMISHNA WA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR



**MHE. KHADIJA SHAMTE MZEE**

**MWENYEKITI**



**DKT.YAHYA KHAMIS HAMAD**
**KAMISHNA**



**ND. SALIM MOHAMED ABDALLA**
**KAMISHNA**



**ND. JUMA MSAFIRI KARIBONA**
**KAMISHNA**



**DKT. SIKUJUA OMAR HAMDAN**
**KAMISHNA**



**MHE. JAJI Geoge Joseph Kazi**
**KAMISHNA**

**ND. MUSSA KOMBO BAKARI**
**KATIBU**

| | |
|---|---|
| Mhe. Khadija Shamte Mzee | Mwenyekiti |
| Mhe. Jaji George Joseph Kazi | Kamishna |
| Dkt. Yahya Khamis Hamad | Kamishna |

| | |
|---|---|
| Dkt. Sikujuwa Omar Hamdan | Kamishna |
| Nd. Salum Mohammed Abdalla | Kamishna |
| Nd. Juma Msafiri Karibona | Kamishna |
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu |

**WATAFITI**

| | |
|---|---|
| Mhe. Khadija Shamte Mzee | Mwenyekiti wa Tume |
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu wa Tume |
| Dkt. Mahfoudha Masoud Ali | Mkurugenzi wa Mapitio ya Sheria |
| Nd. Khamis Ali Jaku | Mkurugenzi wa Mipango, Utumishi na Rasilimali Watu |

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar,

Vuga, Zanzibar,

P.O BOX 2539,

Simu +255 24 2231143,

Nukushi +255 24 2231137,

barua pepe info@lrcz.go.tz,

tovuti www.lrcz.go.tz

**VIFUNGU VYA UTANGULIZI**

**Sheria zilizotumika……………………………………………………………………………ix**

**Shukrani……………………………………………………………………………………………xiii**

**Muhtasari…………………………………………………………………………………………xiv**

**SURA YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**………………………………………………………………………………………1
1.1 Mamlaka ya Tume………………………………………………………………………………1
1.2 Chimbuko la Utafiti……………………………………………………………………………1
1.3 Maelezo ya tatizo………………………………………………………………………………3
1.4 Njia zilizotumika katika Utafiti………………………………………………………………3
1.5 Lengo la utafiti…………………………………………………………………………………4
1.6 Hadidu rejea……………………………………………………………………………………4
1.7 Historia ya Mfumo wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi za Watu……………………………….5

**SURA YA PILI**

**2.0 DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI ................................................................8**
2.1 **Utangulizi.......................................................................................................................8**
2.2 Maana ya taarifa.........................................................................................................................9
2.3 Maana ya taarifa binafsi ..........................................................................................................9
2.4 Maana ya taarifa binafsi nyeti.................................................................................................10
2.5 Dhana ya ulinzi wa taarifa.......................................................................................................10
2.6 Dhana ya faragha katika ulinzi wa taarifa...........................................................................11
2.7 Umuhimu wa Faragha..............................................................................................................13
2.8 Haki za msingi katika ulinzi wa taarifa...............................................................................14
2.9 Idhini katika utoaji wa taarifa...............................................................................................14
2.10 Uchakataji wa taarifa...............................................................................................................15
2.11 Utoaji wa Ridhaa.........................................................................................................................17
2.12 Ulinzi wa taarifa za watu walio katika mazingira magumu...........................................17

**SURA YA TATU**

**3.0 MIPANGO YA KITAIFA, SERA NA SHERIA MBALI MBALI……………………………18**
**3.1 Utangulizi…………………………………………………………………………………………18**
**3.2** Dira ya Maendeleo na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi…………………………………18
**3.2.1** Dira ya Maendeleo ya Zanzibar2050……………………………………………………18
**3.2.2** Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) 2022-2025……………………19

**3.3** Sera……………………………………………………………………………………………………..20
**3.3.1** Sera ya utawala Bora ya Mwaka 2011…………………………………………………………..20
**3.3.2** Sera ya Mawasiliano ya Mwaka 1997…………………………………………………………21
**3.3.3** Sera ya Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari ya mwaka 2016……………………..21
**3.3.4** Sera ya Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari ya Zanzibar Mwaka 2013…………22
**3.3.5** Sera ya Serikali Mtandao yam waka 2012……………………………………………...23
**3.3.6** Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003…………………………………………………..25
**3.3.7** Sera ya utumishi wa Umma ya Mwaka 2010……………………………………………..25
**3.3.8** Sera ya Afya ya Mwaka 2011……………………………………………………………...26
**3.3.9** Sera ya Elimu ya Mwaka 2006……………………………………………………………...26
3.4 Sheria za Muungano……………………………………………………………………………27
3.4.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977……………………..27
3.4.2 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Nam.11 ya mwaka 2022…………………………28
3.4.3 Sheria ya Mamlaka ya kusimamia Mawasiliano Tanzania Nam. 12 ya 2003…..31
3.4.4 Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (R.E) Sura ya 306 ya 2022….32
3.4.5 Sheria ya Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote Nam. 11 ya 2006…33
3.4.6 Sheria ya Banki ya Taasisi za Kifedha Nam. 5 ya mwaka 2006……………………...33
3.4.7 Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 ya Mwaka 2016…………………………………………34
3.4.8 Sheria ya Makosa ya Mtandao, Nam. 14 ya mwaka 2015……………………………….34
3.5 Sheria za Zanzibar……………………………………………………………………………...36
3.5.1 Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984…………………………………………………………36
3.5.2 Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam.3 ya 2018….36
3.5.3 Sheria ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali ya Nam. 13 ya 2012…………...38
3.5.4 Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya mwaka 2018………………………………...39
3.5.5 Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011………………………………...39
3.5.6 Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015……………………40
3.5.7 Sheria ya Uchaguzi Nam. 4 ya 2018…………………………………………………………41
3.5.8 Sheria ya Msaada wa Kisheria Nam. 13 ya Mwaka 2018……………………………...41
3.5.9 Sheria ya Usimamizi na Kujikinga na Ukimwi Zanzibar Nam. 18 ya 2013………42
3.5.10 Sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar
Nam. 1 ya mwaka 2012……………………………………………………………………...43

3.5.11 Sheria ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Nam. 10 ya 2011....44
3.5.12 Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Nyaraka Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 2008..........45
3.5.13 Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara Nam. 12 ya mwaka 2012........................46
3.5.14 Sheria ya udhibiti wa Mali Haramu Nam. 10 ya mwaka 2009...............................47
3.5.15 Sheria ya Usajili wa mali zinazohamishika Nam. 4 ya mwaka 2011.....................48
3.5.16 Sheria ya Adhabu ya Nam. 6 ya mwaka 2018.........................................................49
3.5.17 Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005..........................................................52

**SURA YA NNE**

**4.0 MAONI YA WADAU.........................................................................................53**

**4.1 Utangulizi................................................................................................53**

4.2 Maoni ya Kisera....................................................................................................53

4.3. Maoni ya Kisheria................................................................................................54

**4.3** Maoni ya Kiutendaji..........................................................................................**68**

**SURA YA TANO**

**5.0 MIKATABA YA KIMATAIFA, NA UZOEFU WA NCHI NYENGINE.........................71**

**5.1 Utangulizi...............................................................................................71**

**5.2** Mikataba ya Kimataifa na Kikanda..................................................................71

5.2.1 Azimio la Kimataifa juu ya haki za Binaadam la mwaka 1948.............................71

5.2.2. Mkataba wa Kimataifa wa haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966..........................72

5.2.3 Mkataba wa Ulinzi wa Watu Binafsi kuhusu uchakataji wa Taarifa Binafsi Nam. 108 wa 1981.........................................................................................72

5.2.4 Itifaki ya ziada ya Mkataba wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi kuhusiana na Uhifadhi Wa moja kwa moja wa Taarifa Binafsi Nam. 181 yaa mwaka 2001..............................74

5.2.5 Azimio la Afrika kuhusu Kanuni za Uhuru wa Kujieleza 2019.....................................75

5.2.6 Mkataba wa Nchi za Afrika wa ulinzi wa Mitandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa mwaka 2000........................................................................75

5.2.7 Mkataba wa Kufananisha Sheria za Kulinda taarifa kwa Nchi za Jumuia Ya Maendeleo za nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) wa mwaka 2008....................77

5.2.8 Mkakati wa Usalama wa Mtandao na Uhalifu wa Mtandao wa Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS)......................................................79

5.2.9 Sheria ya Nyongeza juu ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Nchi Wanachama Wa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) 2010................80
5.2.10 Kanuni za Maadili Juu ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi za Wafanyakazi 1997.............82
5.3 UZOEFU WA NCHI NYENGINE..........................................................................................84
5.3.1 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Kenya Nam. 24 ya mwaka 2019................................84
5.3.2 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Afrika ya Kusini Nam. 4 ya 2013.................86
5.3.3 Sheria ya Uganda ya Ulinzi wa Faragha na Taarifa Nam. 9 ya 2019........................88
5.3.4 Sheria ya Mauritius ya Ulinzi wa Taarifa Nam. 120 ya 2017......................................90
5.3.5 Sheria ya Zambia ya Ulinzi wa Taarifa Nam. 3. 2021....................................................93
5.3.6 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya United Kingdom Sura ya 29 ya 1998 .....................96
5.3.7 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Botswana Nam. 32 ya mwaka 2018.......................97
5.3.8 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Ghana Nam. 843 ya mwaka 2012............................99
5.3.9 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Antigua na Barbuda Nam. 10 ya 2013.................101
5.3.10 Sheria ya Ulinzi wa taarifa ya Zimbabwe Nam. 5 ya 2021.........................................103
5.3.11 Sheria ya Ulinzi wa taarifa Binafsi ya Malaysia Nam. 70 ya mwaka 2010............105
5.3.12 Sheria ya Ulinzi wa taarifa ya Swedish na Finland 1050 ya 2018..........................106

**SURA YA SITA**

**6.0 MATOKEO YA UTAFITI……………………………………………………………………….109**
**6.1 Utangulizi………………………………………………………………………………………109**
**6.2** Njia zilizotumika katika Utafiti………………………………………………………………109
**6.3** Makundi ya Wadau (Sampuli ya utafiti) na Uchambuzi wa Takwimu………………109
**6.4** Matokeo ya Utafiti……………………………………………………………………………..116
6.3.1 Matokeo ya Kisera………………………………………………………………………………116
6.5 Matokeo ya Kisheria…………………………………………………………………………………..117

**SURA YA SABA**

**7.0 MAPENDEKEZO YA TUME NA HITIMISHO……………………………………………128**
7.1 **Utangulizi……………………………………………………………………………………………128**
7.2 Mapendekezo ……………………………………………………………………………………....128

7.2.1 Mapendekezo ya Kisera……………………………………………………………………………..128
7.2.2 Mapendekezo ya Kikanuni……………………………………………………………………………128
7.2.3 Mapendekezo ya Kisheria……………………………………………………………………………..132
7.2.4 Mapendekezo ya Kiutendaji…………………………………………………………………………..139
7.3 Hitimisho…………………………………………………………………………………………………..140
**Rejea……………………………………………………………………………………………………...143**

## ORODHA YA SHERIA NA SERA ZILIZOTUMIKA

## MIPANGO NA SERA

Zanzibar Development Vision 2050

Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025

Sera ya Utawala Bora ya Mwaka 2011

Sera ya Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari ya Mwaka 2016.

National Information and Communication Technology Policy 2016.

Zanzibar Information and Communication Technology Policy 2013.

Sera ya Serikali Mtandao, 2012

Sera ya Watu Wenye Ulemavu mwaka 2018.

Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003.

Sera ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010

Sera ya Afya ya Mwaka 2011.

Sera ya Elimu ya Mwaka 2006.

**SHERIA**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya mwaka 1986

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Binafsi ya Tanzania Nam. 11 ya Mwaka 2022.

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Nam.24 ya 2019 ya Kenya
Sheria ya Afrika ya Kusini ya Kulinda Taarifa Binafsi Nam 4 ya 2013.

Sheria ya Uganda ya Ulinzi wa Taarifa na Faragha Nam. 9 ya 2019.

Sheria ya Mauritius ya Ulinzi wa Taarifa Nam. 120 ya 2017.

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Zambia Nam. 3 ya 2021.

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya United Kingdom Sura ya 29 ya 1998.

Sheria ya ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Botswana Nam. 32 ya 2018

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Ghana ya 2012.

Sheria ya ulinzi wa Taarifa ya Antigua na Barbuda Nam 502.

Sheria ya Kulinda Taarifa ya Zimbabwe Nam. 5 ya mwaka 2021.

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Binafsi ya Malaysia Nam. 709 ya 2010.

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Swidesh na Finish Nam. 1050 ya 2018.

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Malaysia Nam. 70 ya Mwaka 2010.

Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Mawasiliano Tanzania ya Mwaka 2003

Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (R.E) ya Mwaka 2022

Sheria ya Mawasiliano kwa Wote ya Mwaka 2006.

Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha Nam. 5 ya mwaka 2006.

Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 ya mwaka 2016

Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya Mwaka 2018.

Sheria ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Nam. 13 ya Mwaka 2012.

Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 a Mwaka 2018.

Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya Mwaka 2011.

Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya Mwaka 2015.

Sheria ya Uchaguzi Nam. 4 ya Mwaka 2018.

Sheria ya Usimamizi na Msaada wa Kujilinda na Ukimwi Zanzibar Nam. 18 ya Mwaka 2013.

Sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar Nam. 1 ya Mwaka 2012.

Sheria ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Nam. 10 ya Mwaka 2011.

Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Rekodi za Nyaraka Zanzibar Nam. 3 ya Mwaka 2008.

Sheria ya Usajili wa Biashara Nam. 12 ya Mwaka 2012.

Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, Nam. 10 ya mwaka 2009.

Sheria ya Usajili wa Mali Zinazohamishika Nam. 4 ya mwaka 2010.

Sheria ya Makosa ya Mtandao Nam. 14 ya mwaka 2015.

Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005.

**Mikataba ya Kimataifa**

Azimio la Kimataifa Juu ya Haki za Binaadam la mwaka 1948.

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa Mwaka 1966.

Mkataba wa Ulinzi wa taarifa binafsi na uchakataji wa taarifa 108 wa 1981.

Convention 108 + And the future data protection global standard - Data Protection (coe.int)

Mkataba wa nyongeza wa ulinzi wa taarifa binafsi na uchakataji wa taarifa

Declaration of Principles on Freedom of Expression 2019 | African Commission on Human and Peoples' Rights (au.int)

Mkataba wa Umoja wa Nchi za Africa wa Ulinzi wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Mkataba wa Jumuiya ya SADC

ECOWAS -Regional Cybersecurity and Cybercrime strategy

Sheria ya Nyongeza ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS).

Mkataba wa kimataifa wa ulinzi wa Taarifa binafsi za wafanyakazi wa 1997.

Kanuni za Jumla za Ulinzi wa taarifa (GDPR) ya Umoja wa Nchi za Ulaya

## SHUKRAN

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imefanikiwa kukamilisha utafiti wa Eneo la Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Data Protection) kwa lengo kuangalia mfumo wa ulinzi wa taarifa binafsi za watu zinazokusanywa kwa mujibu wa sheria mbali mbali. Aidha, Tume imefanikiwa kuainisha changamoto zilizopo kisheria katika ulinzi huo na kutoa mapendekezo ya kisheria na kiutendaji ambayo yatasaidia

kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi na hivyo kutekeleza matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 na kufikiwa malengo yaliyowekwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050.

Shukrani za pekee kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kutambua misingi ya haki za Binaadamu ikiwemo kulinda taarifa binafsi.

Aidha shukrani za dhati ziende kwa Mheshimiwa Mwalim Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa juhudi zake katika kusimamia utawala bora na Mheshimiwa Dkt. Khalid Salum Mohammed kwa maelekezo, miongozo na ushirikiano wake katika kufanikisha utafiti huu.

Aidha, Tume inatoa shukrani kwa taasisi za Serikali, Taasisi ya CENTER FOR YOUTH DIALOGUE (CYD), PACT Tanzania na Freedom House kwa kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa asilimia kubwa katika kuwafikia wadau na masuala mengine yaliyofanikisha kukamilika kwa ripoti hii.

Pia tunatoa Shukrani kwa wataalam mbali mbali wa masuala ya uwekaji na uhifadhi wa taarifa binafsi kutoka taasisi za Serikali na taasisi binafsi, kutokana na uzoefu wao katika eneo hili na masuala ya matumizi ya TEHAMA. Tume inawashukuru wadau wote waliojitolea kutoa maoni yao ya kizalendo na utaalamu kwa manufaa ya Taifa ambao umeisaidia sana Tume katika kufanikisha utafiti huu.

Aidha, shukrani kwa Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Ndg. Mussa Kombo Bakari na wataalam wa Sheria, Utafiti na Mipango, walioongoza zoezi la utafiti na kufanya uchambuzi yakinifu wa taarifa na uandishi wa ripoti hii.

Ahsante.

**MUHTASARI**

Ulinzi wa taarifa binafsi za watu na taarifa za taasisi mbalimbali ni muhimu kwa maisha ya binaadamu katika kuheshimu haki ya faragha na mawasiliano baina ya taasisi zinazohifadhi taarifa, wananchi na wawekezaji. Taarifa hizo zinatumika katika maeneo mengi yakiwemo maeneo ya kazi, ubia wa biashara,

jamii, vikundi, vilabu na biashara za aina mbalimbali. Haki ya kulinda taarifa binafsi za mtu ni hitaji ambalo limetokana na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na mikataba ya kimataifa ambayo inatoa haki na msingi wa kuhifadhi, kuchakata, kulinda na kutoa taarifa binafsi. Haki hizo zinatakiwa kutekelezwa kwa vitendo kupitia utaratibu ambao nchi utajiwekea.

Katika kufanya utafiti huu, njia mbalimbali zimetumika ikiwemo kupitia rejea mbali mbali za ndani na nje ya nchi, kuangalia miongozo ya kimataifa na Sheria za nchi nyengine, kupitia Katiba ya Zanzibar, Sera na Sheria mbali mbali za ndani ya nchi, pamoja na kukusanya maoni ya wadau na wataalamu wa eneo la taarifa binafsi hapa Zanzibar.

Utafiti umebainisha maeneo muhimu ya kuzingatiwa katika eneo la ulinzi wa taarifa binafsi za watu ikiwemo matumizi ya taarifa nyeti na utoaji wake, haki za msingi katika ulinzi wa taarifa, mambo ya kuzingatiwa katika uchakataji wa taarifa, utoaji wa ridhaa kwa watu wa kawaida na wenye mahitaji maalum. Aidha, utafiti umeainisha maeneo muhimu katika ulinzi na uhifadhi wa taarifa binafsi ikiwemo kutambua na kusimamia taasisi za Serikali na binafsi zinazohifadhi taarifa binafsi, chombo cha usimamizi wa taarifa binafsi, taratibu za kutoa taarifa nje ya nchi, uwasilishaji wa malalamiko kwa wananchi na uchukuaji wa hatua kwa wanaokiuka masharti ya kulinda taarifa binafsi, na miongozo na viwango vya kiusalama katika kulinda na kuhifadhi taarifa binafsi.

Aidha, baada ya kukamilika kwa ukusanyaji wa maoni na taarifa nyenginezo, Tume imebaini kutokuwepo kwa utaratibu na mifumo inayotambulika kwa taasisi za Serikali na binafsi katika ulinzi wa taarifa binafsi, na kukosekana

mfumo maalum wa usimamizi kwa taasisi zote zilizopo Zanzibar. Kutokuwepo kwa utaratibu huo, kunapelekea kuwepo changamoto na mapungufu yanayohitaji kusimamiwa kupitia mfumo maalum wa kisheria na miongozo itakayolinda haki za watu katika eneo la taarifa binafsi. Maeneo mengine yanayokwaza katika eneo hii ni kukosekana kwa misingi ya ulinzi wa taarifa, kukosekana ufafanuzi wa taarifa zinazohitaji kulindwa, usajili wa watunza taarifa, miongozo ya maadili katika ulinzi wa taarifa binafsi pamoja na kutokuwepo chombo maalum cha usimamizi wa masuala ya taarifa binafsi za wananchi.

Utafiti umependekeza maeneo mbali mbali ya kufanyiwa kazi katika kuimarisha eneo la ulinzi wa taarifa binafsi ikiwemo uanzishwaji wa sheria maalum ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na mapendekezo mengine ikiwemo kuweka wazi malengo ya kuwepo kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, kuweka misingi katika masuala ya ulinzi wa taarifa, kutambua vyombo vya usimamizi wa masuala ya taarifa na kazi zake, kuweka utaratibu wa usajili kwa taasisi na watu binafsi, kuweka misingi ya kimaadili, kuweka utaratibu mzuri wa masuala ya nidhamu, malalamiko na adhabu, kuwa na usimamizi wa taarifa ulio bora zaidi kwa manufaa ya nchi kiujumla ikiwemo masuala ya uwekezaji.

Mapitio ya eneo la ulinzi wa taarifa binafsi yatasaidia kuweka vyema misingi mizuri ya usimamizi wa taarifa binafsi, kuondoa athari za uvujaji wa taarifa binafsi za watu kinyume na taratibu, kuweka maadili kwa watumishi wanaosimamia uwekaji wa taarifa, kuweka mahusiano na mazingira mazuri ya Serikali na wawekezaji na kuwepo utaratibu wa kusajili taasisi na watu binafsi wanaohusika na ulinzi, uhifadhi, utoaji na uchakataji wa taarifa binafsi. Tume

inaamini matokeo na mapendekezo ya utafiti huu iwapo yatafanyiwa kazi ipasavyo, yatasaidia kuweka usimamizi mzuri katika masuala ya ulinzi wa taarifa binafsi, na kuondoa khofu ya utolewaji wa taarifa binafsi za watu na taasisi kinyume na taratibu.

## SURA YA KWANZA

## 2.0 UTANGULIZI

### 2.1 Mamlaka ya Tume

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imeanzishwa chini ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Nam.16 ya mwaka 1986.[1] Kwa mujibu wa Sheria hii, Tume imepewa jukumu la kuzifanyia utafiti na mapitio Sheria zote za Zanzibar kwa lengo la kurekebishwa pale inapohitajika ili ziende sambamba na maendeleo na mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.[2] Aidha, Sheria iliyoanzisha Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, imeipa mamlaka taasisi hii ama kufanya mapitio ya sheria au kundi la sheria au eneo fulani la sheria.[3]

Kutokana na uwezo iliyopewa wa Kisheria na katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, Tume imefanyia mapitio ya eneo linalohusu sheria zinazogusa ulinzi wa taarifa binafsi kwa ajili ya kuainisha mapungufu yaliyopo katika usimamizi wa taarifa binafsi.

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, inatarajia mapitio haya yatasaidia kuweka utaratibu wa mfumo bora wa uhifadhi na utoaji wa taarifa binafsi.

---

[1] Kifungu cha 3 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya mwaka 1986 kinaanzisha Tume hii ya Kurekebisha Sheria Zanzibar.
[2] Kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar namba 16 mwaka 1986.
[3] Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Nam. 16 ya mwaka 1986, kifungu cha 4(2)(a)

## 2.2 Chimbuko la utafiti

Chimbuko la utafiti huu linatokana na haja ya kutii misingi ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 ya kulinda haki ya faragha ya kila mtu kama ilivyozingatiwa katika kifungu cha 15 cha Katiba. Kifungu hicho cha Katiba kinaeleza haki ya kila mtu kuheshimiwa na kupata hifadhi ya maisha yake binafsi na ya nyumbani kwake, heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake.[4] Aidha, utafiti huu ni utekelezaji wa moja kwa moja wa Katiba kutaka mamlaka ya nchi kuweka utaratibu na namna ambayo haki ya mtu ya faragha inaweza kuingiliwa bila ya kuathiri haki hiyo iliyotolewa kikatiba.[5]

Aidha, chimbuko la utafiti huu linatokana na maelekezo ya Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi ya kutaka kufanyika kwa utafiti huu baada ya kuwepo kwa Sheria kama hii kwa upande wa Tanzania Bara ambayo imeshatungwa na kuanza kutumika kuanzia mwaka 2022. Hali hiyo imepelekea na kwa upande wa Zanzibar kama nchi kuwa na Sheria inayofanana na hiyo kwa sababu Sheria ya Tanzania Bara imetamka kwamba Sheria itatumika Zanzibar kwa masuala ya Muungano tu, na hivyo kujitokeza mapungufu ya kukosa Sheria inayosimamia eneo hili kwa Zanzibar.

Vile vile, chimbuko la utafiti huu linatokana na changamoto zinazojitokeza katika eneo la ulinzi na uhifadhi wa taarifa binafsi katika taasisi binafsi na taasisi za Serikali ambazo hazina sheria na miongozo ya moja kwa moja inayoelekeza katika utaratibu wa kuchakata taarifa, uhifadhi, kuzilinda na

[4] Kifungu cha 15(1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.
[5] Kifungu cha 15(2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984..

kuzitoa taarifa hizo kwa watu au taasisi nyengine. Vile vile, changamoto ya kutokuwepo mipaka juu ya taarifa za kutolewa na mamlaka zinazopaswa kupewa taarifa bila ya idhini ya mtoaji zimepelekea kufanyika utafiti huu.

## 2.3 Maelezo ya tatizo.

Suala la ulinzi na uhifadhi wa taarifa binafsi linagusa haki ya msingi ya faragha kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Aidha, kukua kwa teknolojia na utandawazi kumelifanya eneo la ulinzi wa taarifa binafsi kupata changamoto kubwa kutokana na udukuzi wa taarifa na uchakataji mbaya wa taarifa mbali mbali ambazo baadae husambazwa kinyume na taratibu.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari imeweka misingi katika eneo la ulinzi na uhifadhi wa taarifa kwa kuanzisha Sheria mahsusi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ili kukabiliana na changamoto mbali mbali. Sheria hii inagusa Zanzibar kwa maeneo ya muungano na baadhi ya maeneo ambayo yatahitaji ushirikiano na taarifa kutoka upande mwengine. Hata hivyo, kwa upande wa Zanzibar eneo hili bado halijaekewa utaratibu maalum, mbali ya kuwepo kwa baadhi ya taasisi zinazoratibu na kusimamia taarifa katika taasisi zao.

## 2.4 Njia zilizotumika katika Utafiti

Katika kufanya utafiti huu, njia mbali mbali zimetumika ambazo zimeweza kusaidia kupata taarifa na kuweza kufanikisha malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu. Njia hizo ni pamoja na kupitia rejea za ndani na nje ya nchi,

kuangalia mikataba na miongozo ya kimataifa na uzoefu wa Sheria za nchi nyengine, Katiba, Sera na Sheria mbali mbali, pamoja na kukusanya maoni ya wadau na washirika muhimu katika eneo hili la ulinzi wa taarifa binafsi.

## 2.5 Lengo la Utafiti

Lengo kuu la Utafiti huu ni kuangalia mfumo wa ulinzi wa taarifa binafsi za watu zinazokusanywa kwa mujibu wa sheria mbali mbali, kuainisha changamoto zilizopo kisheria katika ulinzi huo na kutoa mapendekezo ya kisheria na kiutendaji ambayo yatasaidia kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi za watu na hivyo kutekeleza matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya 1984.

## 2.6 Hadidu rejea

Katika kufanya utafiti huu, Hadidu rejea zifuatazo zimezingatiwa:

(a) Kupitia sheria mbali mbali zinazotoa mamlaka ya kukusanya taarifa binafsi za watu na kuangalia mfumo wa ulinzi uliopo kwenye sheria hizo, kubainisha ubora na udhaifu wake pamoja na kupendekeza namna ya kuimarisha ulinzi huo;

(b) Kuangalia uzoefu wa nchi mbali mbali juu ya ulinzi wa taarifa binafsi za watu na kupendekeza namna uzoefu huo unavyoweza kutumika na kusaidia kuimarisha mfumo wa ulinzi wa taarifa binafsi za watu wa Zanzibar;

(c) Kuangalia Sera mbali mbali zinazohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi za watu pamoja na mikataba ya kimataifa inayohusiana na eneo hilo na namna zinavyoweza kusaidia mfumo imara wa ulizni wa taarifa binafsi za watu Zanzibar;

(d) Kukusanya maoni ya wadau mbali mbali wanaohusika na ulinzi wa taarifa binafsi za watu kwa lengo la kupata mapendekezo ya kisheria na yatakayosaidia kuimarisha mfumo wa ulinzi wa taarifa binafsi Zanzibar;

(e) Kutoa mapendekezo yanayofaa ya kisheria na kiutendaji yatakayoimarisha mfumo wa ulinzi wa taarifa binafsi za watu Zanzibar.

## 2.7 Historia ya Mfumo wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi za Watu

Haki ya faragha ambayo inafungamanishwa na suala la haki za binadamu na uhuru wa watu ni dhana kongwe ya muda mrefu kama ilivyo historia ya mwanadamu.[6] Hata hivyo, pamoja na dhana hiyo kuwa ni ya muda mrefu kwa maeneo mengi, dhana hiyo kwa wakati huo haikuwekwa na kulindwa kisheria.[7] Masuala haya ya faragha yalijitokeza zaidi wakati jamii ilipoanza kushuhudia matendo ya kurikodi taarifa za watu ambayo ilikuwa ni teknolojia mpya na hivyo kuanza kujitokeza kwa haja ya ulinzi wa haki hii ya faragha.

---

[6] Asrienn Luk'acs,WHAT IS PRIVACY? THE HISTORY AND DEFINITION OF PRIVACY, University of Szeged, Faculty of Law and Political Sciences, Department of Labour Law and Social Security and Sorbonne Law School Universit'e Paris 1, PhD student, lukacs.adrinn@juris.u-szeged.hu

[7] Ibid.

Eneo hili limekumbwa na changamoto nyingi ikiwemo ukuaji wa sayansi na teknolojia.  Hivyo, sheria za haki za faragha zimekuwa zikitungwa na kufahamika kama sheria zinazoweka misingi ya jumla kuonesha kwamba uvamizi wa faragha dhidi ya taarifa binafsi za mtu ni makosa yanayoweza kushtakiwa katika mahakama na aliyeathirika kupata haki yake kwa kiasi alichoumizwa kutokana na kuingiliwa kwa taarifa zake hizo.[8]

Haki ya faragha ya mtu kwa ujumla ilianza kwa ulinzi wa kimwili wa mtu pamoja na maskani yake na kuingia kwenye ulinzi wa taarifa binafsi ambapo mwaka 1891, mwanasheria wa kimarekeni Samuel Warren na Louis Brandeis waliitafsiri haki ya faragha kama haki ya kuachwa huru bila ya kuingiliwa katika uhuru wa mtu binafsi.[9]

Aidha, mwaka 1967, Alan Westin katika Makala yake ya Faragha na Uhuru aliieleza dhana ya faragha kama haki ya mtu mmoja mmoja, kundi la watu au taasisi kuamua kwa kiwango gani taarifa zao zinaweza kutolewa kwa watu wengine.[10] Hii inamaanisha kuwa, dhana ya faragha inazuia taarifa za mtu, watu, kikundi au taasisi kutolewa bila ya kwanza kupatikana kwa ridhaa yao juu ya utoaji wa taarifa hizo.

Historia ya uwepo wa Sheriainaonesha kuwa suala la haki za faragha ya taarifa binafsi za watu limekuwa katika sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya benki ambapo Januari 2003, kumekuwa na taarifa zilizoenea za ''Royal Bank'' ya

---

[8] Ibid, ukurasa wa 2.

[9] V. Matyáš et al. (Eds.): The Future of Identity, IFIP AICT 298, pp. 13–42, 2009. © IFIP International Federation for Information Processing 2009
History of Privacy* Jan Holvast & Partner, Privacy Consultants, NL- Landsmeer, The Netherlands. henp.holvast@wxs.nl

[10] Ibid.

nchini Canada kuweka utaratibu ambao unasababisha taarifa binafsi za wateja takriban 180,000 zinazohusu masuala ya fedha kuathiriwa kwa kuweza kutolewa hata nje ya mipaka ya nchi hiyo.[11]

Kwa msingi huu, wakati wa ukuaji wa tekolojia duniani ambayo inafanya upatikanaji wa taarifa za watu kuwa rahisi kutumiwa na kusafirishwa kwenda sehemu nyengine, ulinzi wa taarifa hizo binafsi za watu umekuwa muhimu sana.

Kwa upande wa Zanzibar kuna taasisi nyingi zinazohifadhi na kuchakata taarifa binafsi ikiwemo taasisi za fedha, vitambulisho, sekta ya afya, mwawasiliano, umiliki, ardhi, biashara n.k, ingawa hakuna Sheria mahsusi inayoratibu na kusimamia eneo la uhifadhi, uchakataji na utoaji wa taarifa.

[11] LAW REFORM COMMISSION OF SASKATCHEWAN CONSULTATION PAPER: RENEWING THE PRIVACY ACT, JULY, 2009

# SURA YA PILI

## 2.0 DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI (PERSONAL DATA PROTECTION)

### 2.1 Utangulizi

Haki ya kulinda taarifa binafsi za mtu ni hitaji ambalo limetokana na mikataba ya kimataifa ambapo haki hizo pia zimelindwa na Katiba za nchi mbali mbali

miongoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa.[12] Haki hizo zinatakiwa kutekelezwa kwa vitendo kupitia utaratibu mbalimbali ambao nchi utajiwekea.[13] Aidha, eneo la haki ya kulinda taarifa binafsi limeanza kuwekewa zaidi misingi wakati wa utumiaji wa mifumo ya kimtandao ulipoanza, na mataifa ya Afrika na mashirika ya kikanda yalipoanza kupitisha sheria na kanuni mbalimbali zinazohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi.[14]

Ulinzi wa taarifa binafsi ni muhimu kwa maisha ya binaadamu katika kuheshimu maisha ya kibinafsi na ya familia, nyumba na mawasiliano.[15] Taarifa hizo zinatumika katika maeneo mengi yakiwemo maeneo ya kazi, ubia wa biashara, jamii, vikundi, vilabu na biashara halali za aina zote.[16]

## 2.2 Maana ya taarifa (data)

Taarifa imetafsiriwa na waandishi mbalimbali kuwa ni maelezo yanayoonesha maisha ya mtu, kuelezea kitu au kufanya maamuzi ya kitu. Kwa mfano, bwana Paur Voigt ameelezea maana ya taarifa ni maelezo yanayomtambulisha mtu maisha yake, ishara au viashiria.[17]

---

[12] Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966, ibara ya 17

[13] ALT Advisory Module 4: Data privacy and data protection (2020) Media Defence, ukurasa 1 inapatikana DATA PRIVACY AND DATA PROTECTION (mediadefence.org)

[14] Ibid

[15] Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966, ibara ya 17

[16] Asrienn Luk'acs,WHAT IS PRIVACY? THE HISTORY AND DEFINITION OF PRIVACY, University of Szeged, Faculty of Law and Political Sciences, Department of Labour Law and Social Security and Sorbonne Law School Universit'e Paris 1, PhD student, lukacs.adrinn@juris.u-szeged.hu

[17] Paur Voigt, The General Data Protection Regulation (GDPR) Berlin, 2017 uk 11

Pia, bwana Stephen Kai-yi WONG na bwana Guobin ZHU wameeleza maana ya taarifa ni kuwa uwasilishaji wowote wa habari ambao unajumuisha uwasilishaji wa maoni katika hali yeyote ambao unajumuisha utambulisho wa mtu binafsi.[18]

Aidha, baadhi ya waandishi wametafsiri taarifa kuwa ni habari inayomtambulisha asili ya mtu moja kwa moja au kinyume chake kwa njia sahihi zitakazotumika na mchukuaji wa taarifa au mtu mwengine yeyote ambaye ana jukumu la kuchukua taarifa kwa misingi ya kisheria ambayo itahusisha namba ya kitambulisho, sehemu anayoishi, urithi, uchumi, utamaduni na utambulisho wake katika jamii.[19]

## 2.3 Maana ya taarifa binafsi (personal data)

Taarifa binafsi inamaanisha taarifa yoyote inayomuhusu mtu aliye hai, ambapo mtu huyo atajulikana kupitia taarifa hiyo na inaweza kujumuisha kupitia vile jina, tarehe ya kuzaliwa, anwani ya barua pepe, nambari ya simu, anwani, sifa za mtu binafsi au taarifa ya eneo analoishi.[20]

Aidha taarifa binafsi lazima ziwe katika maandishi, na pia inawezekana ikawa taarifa hiyo inaonekana kwa picha au inasikika kama sauti au video. Hata hivyo,

---

[18] Stephen kai-yi WONG, Guobin ZHU, The personal Data(private) Law in Hong –Kong , University of Hong Kong 2020 uk 10

[19] S. Nair, M. Dashti, B. Crispo, and A. Tanenbaum. A Hybrid PKI-IBC Based Ephemerizer System. Proc. New Approaches for Security, Privacy and Trust in Complex Environments, 241-252, 2007.

[20] The data protection Commission, the Basic Data Protection, July 2019, uk 3

ulinzi wa taarifa utatumika pale tu ambapo taarifa hizo zinatumika au kuchakatwa kwa njia ya kieletroniki.[21]

## 2.4 Maana ya taarifa binafsi nyeti

Taarifa binafsi nyeti ni taarifa maalum ambazo zinatakiwa kupewa ulinzi wa ziada katika kuzilinda na kuzihifadhi.[22] Taarifa zenyewe ni taarifa inayohusiana na kabila, asili ya mtu, mitazamo ya kisiasa, imani za kidini, chama cha wafanyakazi, urithi, mifumo ya bayometriki, hali ya kiafya, hali ya kijinsia na hali ya uchaguzi wa kijinsia.[23]

## 2.5 Dhana ya ulinzi wa taarifa

Ulinzi wa taarifa maana yake ni utaratibu mzima wa kulinda maelezo au taarifa binafsi ya mtu ili taarifa hizo zisiweze kuharibika, kuingiliwa au kupotea na kutoa uwezo wa kurejesha tena taarifa hiyo katika hali ya asili.[24]

Aidha, ulinzi wa taarifa maana yake ni utaratibu wa kisheria ambao umewekwa kwa ajili ya kulinda taarifa binafsi katika jamii ili kudhibiti matumizi mabaya ya taarifa hizo kwa Serikali na kampuni ambazo zinapokea taarifa na kuzichakata.[25]

---

[21] Ibid

[22] Kanuni za Jumla za Ulinzi wa taarifa (GDPR) ya Umoja wa Nchi za Ulaya ibara ya 9(1)

[23] ibid

[24] Elizabeth Andrew Mamba ''Assessing the relevance of the Existing Legal regime in Tanzania for Data protection'' Uk. 3

[25] A Guide for Policy Engagement on Data Protection, Data Protection, Explained also available on : https://www.privacyinternational.org/explainer/41/101-data-protection

Bi Elizabeth Andrew Mamba ametafsiri maana ya ulinzi wa taarifa kuwa ni utaratibu wa kulinda taarifa muhimu dhidi ya uharibifu, upotevu na uvujaji pamoja na kuhakikisha faragha ya taarifa inapatikana kwa kuhakikisha watu wanatumia taarifa zao kwa uadilifu".[26]

Wakiandika juu ya dhana ya ulinzi wa taarifa, Paul de Hert na Serge Gutwirth wanatoa maoni kwamba haiwezekani kufupisha ulinzi wa taarifa katika mistari miwili au mitatu. Ulinzi wa taarifa ni neno linalohitaji majumuisho ya mambo mengi na mawazo kuhusu uchakataji wa taarifa ya kibinafsi[27]. Ulinzi wa taarifa unazingatia haki za msingi na uhuru wa watu asilia, na hasa haki yao ya faragha kuhusiana na uchakataji wa taarifa kibinafsi.[28]

Taarifa binafsi ili ziweze kulindwa kwa usahihi na ziweze kupatikana kwa muda unaohitajika, kunatakiwa kuandaliwa mikakati madhubuti itakaosaidia taarifa hizo kutumika kwa usahihi kwa madhumuni yaliyokusudiwa na pamoja na kukinga taarifa hizo kuweza kupotea, kuharibika au kuvuja.[29]

## 2.6 Dhana ya faragha katika ulinzi wa taarifa

---

26 https://ico.org.uk/for-organisations/guide-to-data-protection

27 P de Hert and S Gutwirth , ' Data Protection in the Case Law of Strasbourg and Luxemburg : Constitutionalisation in Action ' in S Gutwirth and others (eds), Reinventing Data Protection ? ( New York , Springer , 2009 ) 3

28 ibid

29 Agency of Protection of Data Guidelines for Data Protection by Defaul (2020) Page 22

Faragha ina historia ndefu lakini kwa sababu ya ugumu wake, faragha imethibitika kuwa ngumu kuieleza na imekuwa na mjadala wa kina kwa wanafalsafa, wanasaikolojia, na wasomi wa sheria.[30] Neno "faragha" hupatikana katika kiwango cha kibinafsi na mara nyingi humaanisha mambo tofauti kwa watu tofauti.[31]

Katika jamii ya kisasa, neno faragha hutumiwa kuashiria dhana tofauti, lakini zinazopishana, kama vile haki ya uadilifu au kuwa huru kutokana na utafutaji au ufuatiliaji wa kitu.[32] Dhana ya faragha pia ni mahususi na hupewa maana tafauti kulingana na sababu zilizotajwa za taarifa inayokusanywa, nia ya wahusika wanaohusika, na vile vile matarajio ya kisiasa, mikataba na kiutamaduni.[33]

Dhana za faragha zimefungamana kwa karibu na zile za usiri na usalama, ingawa, faragha mara nyingi hutumiwa kwa kubadilishana na maneno kama "usiri" na "usalama," ambayo yana maana tofauti.[34] Faragha inashughulikia swali la nani anaweza kupata taarifa za kibinafsi na chini ya hali gani, faragha inahusika na ukusanyaji, uhifadhi, na utumiaji wa taarifa za kibinafsi, na inachunguza kama taarifa inaweza kukusanywa na inaweza kutumika kwa ajili

---

[30] Westin A. How the public views privacy and health research. Institute of Medicine; 2007

[31] Lowrance WW. Privacy and health research: A report to the U.S. Secretary of Health and Human Services. 1997

[32] Allen A. Genetic privacy: Emerging concepts and values. In: Rothstein M, editor. Genetic secrets: Protecting privacy and confidentiality in the genetic era. New Haven, CT: Yale University Press; 1997. pp. 31–59.

[33] Nissenbaum H. Privacy as Contextual Integrity. Washington Law Review. 2004;79:101–139.

[34] The Fundamental Right to Data Protection Normative Value in the Context of Counter-Terrorism Surveillance, https://media.bloomsburyprofessional.com/rep/files/9781509901678sample.pdf , HART Publishing, OXFORD AND PORTLAND, OREGON 2017

nyengine. Suala muhimu katika uchanganuzi wa faragha ni iwapo mtu huyo ameidhinisha matumizi fulani ya taarifa zake za kibinafsi.[35]

## 2.7 Umuhimu wa Faragha

Kuna sababu mbalimbali za kuweka thamani ya juu katika kulinda faragha, usiri, na usalama wa taarifa mbalimbali kama afya,[36] na maeneo yenye haki ya msingi ya binadamu.[37] Hivyo kuheshimu thamani ya faragha ni muhimu kwa ustawi wa mwanadamu na ni aina ya utambuzi wa sifa zinazowapa wanadamu upekee wao wa kimaadili.[38]

Mtazamo wa kawaida zaidi ni kwamba faragha ni muhimu kwa sababu inawezesha au kukuza maadili mengine ya kimsingi, ikiwa ni pamoja na maadili ya utu.[39]

Ukiukaji wa faragha na usiri sio tu unaweza kuathiri utu wa mtu, lakini unaweza kusababisha madhara, unyanyapaa, aibu, na ubaguzi. Kwa hivyo, bila uhakika

---

[35] Westin A. Privacy and freedom. New York: Atheneum; 1967.

[36] Pritts JL. Altered states: State health privacy laws and the impact of the federal health Privacy Rule. Yale Journal of Health Policy, Law & Ethics. 2002;2(2):327–364

[37] Fried C. Privacy. Yale Law Journal. 1968;77:475–493, Terry NP, Francis LP. Ensuring the privacy and confidentiality of electronic health records. University of Illinois Law Review. 2007;2007(2):681–736.

[38] loustein E. Privacy as an aspect of human dignity: An answer to Dean Prosser. New York Law Review. 1967;39:34.

[39] Solove DJ. A taxonomy of privacy. University of Pennsylvania Law Review. 2006;154:516–518.

fulani wa faragha, watu wanaweza kusita kutoa taarifa za wazi na kamili hata kwa watu wanaopaswa kupewa taarifa hizo kisheria.[40]

Watu binafsi wana uwezekano mkubwa wa kushiriki na kuunga mkono utafiti ikiwa wanaamini kuwa faragha yao inalindwa. Aidha, ulinzi wa faragha unasaidia ubora wa taarifa kwa ajili ya utafiti na mipango ya baadae.[41] Kupitia vifaa vya kielektroniki vinavyotumika kuhifadhia taarifa binafsi au za faragha vinatumiwa na watu binafsi na kujumuisha taarifa zao zote katika eneo moja.[42] Hivyo miundombinu na teknolojia zinazohifadhi faragha zinatakiwa kuonesha wanaotoa taarifa na vifaa vinavyohifadhi taarifa kwa watu binafsi.[43]

## 2.8 Haki za msingi katika ulinzi wa taarifa

Ulinzi wa taarifa na haki za binadamu sio dhana mpya, lakini inaongezeka umaarufu.[44] Suala la haki ya ulinzi wa taarifa linategemeana na masuala mbalimbali ikiwemo wajibu wa kulinda haki ya ulinzi wa taarifa na hasa wakati gani taarifa zao za kibinafsi zinachakatwa.[45] Haki za kimsingi zinaunganishwa

---

[40] Abdulrauf, L. 2020. "Data Protection in the Internet: South Africa." In Data Protection in the Internet, edited by Dário Moura Vicente and Sofia de Vasconcelos Casimiro. Ius Comparatum - Global Studies in Comparative Law 38. 349-370. Springer.

[41] David C Vladeck, 'Consumer Protection in an Era of Big Data Analytics' (2016) 42 Ohiyo Northern University Law Review 493, 504.

[42] Whitman, James Q. 2004. "The Two Western Cultures of Privacy: Dignity versus Liberty." Yale law journal 113: 1151-1221.

[43] Warren, S.D, and L.D. Brandeis. 1890. "The right to privacy." Harvard Law Review 4(5): 193-220.

[44] S Nouwt , ' Towards a Common European Approach to Data Protection : A Critical Analysis of Data Protection Perspectives of the Council of Europe and the European Union ' in S Gutwirth and others (eds), Reinventing Data Protection ? ( New York , Springer , 2009 ) 275, 278

[45] L Floridi , ' The ontological interpretation of informational privacy' ( 2005 ) 7 Ethics and Information Technology 185, 194

na haki za binadamu zinatokana na Katiba hasa katika ulimwengu wa mtandao. Hivyo, ni muhimu kutambua kwamba haki ya ulinzi wa taarifa inaweza kukiukwa na kuleta madhara kwa kiasi kikubwa.[46]

## 2.9 Idhini katika utoaji wa taarifa

Kuridhika au kutoa idhini ni muhimu katika eneo la uhifadhi na utoaji wa taarifa, ili kuondoa changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza katika utoaji wa taarifa.[47] Idhini inatakiwa kutolewa kwa uhuru, usawa na uwazi kati ya muhusika wa taarifa na mdhibiti wa taarifa.[48]

Aidha, uwezo wa kutoa idhini unahitaji msingi ya ukusanyaji wa taarifa, ambapo changamoto za mtumiaji wa taarifa zinahitaji kuzingatiwa.[49] Idhini inahitajika kwa ujumla ili kukusanya taarifa nyeti, kwa madhumuni ya msingi yanayokubalika.[50]

## 2.10 Uchakataji wa taarifa

Uchakataji wa taarifa unafanywa na mchakataji ambaye ni mtu wa tatu, na ikiwemo taasisi za umma au mashirika ambayo wanapokea taarifa binafsi kwa

[46] F Fabbrini , Fundamental Rights in Europe — Challenges and Transformations in Comparative Perspective ( Oxford , Oxford University Press , 2014 ) 37

[47] Prictor, Megan, Harriet J. A. Teare, Jessica Bell, Mark Taylor, and Jane Kaye. 2019. Consent for data processing under the General Data Protection Regulation: Could 'dynamic consent' be a useful tool for researchers? Journal of Data Protection and Privacy 3: 93–112

[48] Taylor, Mark. 2012. Genetic Data and the Law: A Critical Perspective on Privacy Protection. Cambridge: CUP

[49] Tassé, Anne Marie, Isabelle Budin-Ljøne, Bartha Maria Knoppers, and Jennifer R. Harris. 2010. Retrospective access to data: The ENGAGE consent experience. European Journal of Human Genetics 18: 741–45

[50] Bart Custers and Helena Uršič, 'Big Data and Data Reuse: A Taxonomy of Data Reuse for Balancing Big Data Benefi ts and Personal Data Protection' (2016) 6 International Data Privacy Law 4, 8–9.

ajili kuzitafsiri ili ziweze kutumika.[51] Mchakataji wa taarifa ana jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa anachakata taarifa kwa usiri, usahihi na usalama ili usiathiri matokeo ya uchakataji wa taarifa.[52]

Kwa maneno ya jumla, "uchakataji" unaweza kuonekana kama operesheni yoyote inayofanywa kwenye taarifa, kuanzia ukusanyaji, kurikodi, kuhifadhi, matumizi, utoaji, kusambaza, kufuta na kuharibu taarifa.[53]

Taarifa binafsi zinazochakatwa zinaweka uwazi juu ya utambulisho katika mtandao kwa kumtambua mtu moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, kwa kuongeza, utambulisho unahusisha vifaa, programu, na zana nyengine.[54]

Taarifa inachukuliwa kuwa ya kibinafsi, inapoweza kuunganishwa na mtu fulani, na wadhibiti ni watu wa asili au wa kisheria ambao huamua kuchakata taarifa ya kibinafsi. Lengo kuu la ulinzi wa taarifa ni kuhakikisha usawa katika uchakataji wa taarifa na, kwa kiasi fulani, usawa katika matokeo ya uchakataji huo.[55]

---

[51] Nikita druggal What Is Data Processing: Cycle, Types, Methods, Steps and Examples Feb 27, 2023
[52] Kanuni za Jumla za Ulinzi wa taarifa (GDPR) ya Umoja wa Nchi za Ulaya ibara ya 6
[53] P Alston , ' Making Space for New Human Rights: The Case of the Right to Development ' , ( 1988 ) 1 Harvard Human Rights Year Book 3, 39 . 108
[54] Viktor Mayer-Schönberger and Yann Padova, 'Regime Change? Enabling Big Data through Europe's New Data Protection Regulation' (2016) 17 Columbia Science & Technology Law Review 315, 326.

[55] Boyd D, Crawford K (2012) Critical questions for big data: Provocations for a cultural, technological, and scholarly phenomenon. *Information, Communication & Society* 15(5): 662–679.

Haki ya uchakataji inalindwa na kanuni, ambazo, kwa ujumla, zinazingatia taarifa za kibinafsi zinazopaswa kukusanywa na kushughulikiwa kwa haki na uhalali; madhumuni ya kukusanya taarifa; usahihi, muda wa kuhifadhi taarifa; idhini ya mtu ambaye taarifa zake zinahusiana au ni muhimu kwa baadhi ya taasisi nyengine za uchakataji wa taarifa; hatua za usalama zinazopaswa kuchukuliwa ili kulinda taarifa na matumizi yaliyoidhinishwa.[56]

## 2.11 Utoaji wa Ridhaa.

Suala la ridhaa linatakiwa kuzingatia usawa katika uchukuaji wa taarifa na inaainisha mahusiano katika kudhibiti taarifa, pamoja na mwingiliano kati ya watumiaji na kampuni kubwa na raia na vyombo vya dola kama vile vyombo vya kutekeleza sheria na usalama.[57]

Aidha, zipo hatua sita muhimu zinazotumika katika uchakataji wa taarifa binafsi nazo ni kukusanya taarifa, kufanya maandalizi ya taarifa, uingizaji wa taarifa, uchakataji wa taarifa, ufafanuzi wa taarifa pamoja na kuhifadhi taarifa.[58]

## 2.12 Ulinzi wa taarifa za watu walio katika mazingira magumu

Tume ya Watu wa ulaya inayohusiana na Haki za Binaadamu imeorodhesha makundi ambayo hayana uwezo kisheria, na wapo katika mazingira magumu

---

[56] De Hert & Gutwirth (2006) Privacy, data protection and law enforcement. In: Claes E, Duff A and Gutwirth S (eds) *Privacy and the Criminal Law*. Oxford, UK: Hart, pp. 61–104.

[57] Daniel J Solove, 'Introduction: Privacy Self-Management and the Consent Dilemma' (2013) 126 Harvard Law Review 1880, 1902.

[58] Kanuni za Jumla za Ulinzi wa taarifa (GDPR) ya Umoja wa Nchi za Ulaya ibara ya 16-17

wa kutoa idhini yao ambapo wanaweza kupata matokeo mabaya sana ikiwa taarifa zao za kibinafsi zitasambaa katika jamii. Makundi yenyewe ni watoto, wajawazito, wazee, watu wenye walemavu wa akili, watu wenye ulemavu wa viungo, watu ambao wanatafuta hifadhi (asylum seekers), makabila yenye watu wachache na hayana ushawishi mkubwa.[59]

Watoto wanahitaji ulinzi mahususi unapokusanya na kuchakata taarifa zao za kibinafsi kwa sababu hawajui athari zinazoweza kutokea kutokana na umri wao.[60]

**SURA YA TATU**

## 3.0 MIPANGO YA KITAIFA, SERA NA SHERIA MBALI MBALI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii ya Tatu inaelezea mipango mikuu kama vile Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Dira ya Maendeleo Zanzibar 2050 inayotoa miongozo juu ya misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi. Aidha, sura hii imefanya uchambuzi juu ya mitazamo ya Sera na Sheria mbali mbali ambazo kwa namna moja ama nyengine zinatoa mwongozo na kusimamia masuala yanayohusiana na ukusanyaji, uchakataji na ulinzi wa taarifa binafsi.

[59] European commissionEthics in Social Science and Humanities July 2021 ukurasa wa 11
[60] Kanuni za Jumla za Ulinzi wa taarifa (GDPR) ya Umoja wa Nchi za Ulaya ibara ya 8

Suala la ukusanyaji wa taarifa binafsi limeguswa katika sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na sheria za kimuungano kama ilivyoanishwa kupitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yam waka 1977, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na mamlaka binafsi za Tanzania Bara na Zanzibar.

## 3.2 Dira ya Maendeleo na Ilani ya Chama Tawala.

### 3.2.1 Dira ya Maendeleo 2050.

Kupitia Dira ya Maendeleo katika msingi wa 3 ambao unatoa mwongozo juu ya masuala ya miundombinu,[61] imeelezea na kutoa miongozo juu ya masuala ya habari na mawasiliano kupitia Mamlaka ya Mawasiliano kama ni msimamizi wa mawasiliano na habari.[62] Ingawa Dira haikutoa mwongozo wa moja kwa moja juu ya namna ya ulinzi wa taarifa binafsi unavyotakiwa kuwa lakini imezitaka taasisi mbali mbali za mawasiliano, zihakikishe zimeweka mifumo mizuri ya kisheria pamoja na utumiaji wa vifaa vya kisasa ili kutoa huduma bora na salama za kimawasiliano habari na ulinzi wa taarifa.

Aidha, katika kuhakikisha utaratibu mzuri katika masuala ya habari na mawasiliano, Dira imeweka mikakati ya kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ili kuhakikisha upatikanaji wa taarifa kwa wazanzibari wote.[63]

[61] Zanzibar development vision 2050 Pillar III (Infrastractural Linkages)
[62] Tanzania Communication Regulation Authority (TCRA)

[63] Supra. Aspiration on information and communication. Uk. 64

### 3.2.2 Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) 2025

Kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika sura yake ya Sita ambayo inazungumzia masuala ya utawala bora, utawala wa Sheria pamoja na madaraka ya wananchi, imetoa mwongozo juu ya masuala ya maendeleo ya nchi na ustawi wa jamii. Ilani inataka maendeleo yazingatie misingi ya utu, ushirikishwaji, demokrasia, uwajibikaji, uwazi, utekelezaji, tija, ufanisi pamoja na uzingatiaji wa haki katika masuala yote yanayohusisha wananchi.[64]

Aidha, Ilani ya CCM imezitaka taasisi za kiuchumi na kimaendeleo, kutengeneza mifumo ya kuratibu na kuhifadhi taarifa, ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa taarifa ambazo ni sahihi.[65] Vilevile, katika sekta ya mawasiliano itajikita zaidi katika kuimarisha ubora wa taarifa kwa kuongeza faragha na usiri wa taarifa za wananchi katika mawasiliano kwa kukamilisha kutunga Sheria ya kuimarisha ulinzi wa taarifa na takwimu.[66]

Aidha, ilani ya CCM imezingatia masuala ya demokrasia na utawala bora kama sehemu ya msingi ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii, na kisiasa. Katika kufanikisha hilo, juhudi kubwa zimechukuliwa kwa Zanzibar katika kuimarisha taasisi na mifumo ya upatikanaji wa haki. Hivyo, miongoni mwa mikakati yake yanayotakiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka 5 ijayo ni kutekeleza shughuli za Serikali kwa kuzingatia misingi ya demokrasia na utawala bora kama ilivyoainishwa katika katiba za nchi na kuimarisha uwazi na uwajibikaji

[64] Ilani ya (CCM) 2020-2025 (**utawala bora**) namba 109, Uk. 161
[65] Ibid, mkakati wa kuwezesha uwekezaji katika kilimo na biashara Uk.43
[66] Ibid, mawasiliano. 61(b). Uk.97

kwa wananchi. Hivyo, miongoni mwa misingi ya utawala bora ni kuzingatia haki za binaadamu ambapo kwa upande wa taasisi zinazoihusisha na uchukuaji wa taarifa binafsi za wananchi kulinda haki yao hiyo.[67]

## 3.3 Sera

### 3.3.1 Sera ya Utawala Bora ya Mwaka 2011

Sera ya Utawala Bora ni Sera mama katika kusimamia Serikali na Taasisi zake katika utekelezaji wa misingi ya utawala bora wakati wa kutekeleza majukumu. Sera hii imeainisha misingi ya utawala bora ikiwa ni pamoja na uwajibikaji na uwazi, kuzuia rushwa, ufanisi na tija, ushirikishwaji, kuzingatia matakwa ya wananchi pamoja na utawala wa Sheria na haki za binaadamu.[68]

Ingawa Sera hii haikuweka wazi moja kwa moja katika kutoa mwongozo juu ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa taasisi zinazohusiana na upokeaji wa taarifa binafsi za wananchi, lakini kupitia msingi wa kuhakikisha haki za binaadamu, Katiba ya Zanzibar, imeeleza haki ya faragha kwa kila mwananchi ikiwa ni pamoja na masuala ya taarifa zake binafsi kuzingatiwa na kila taasisi za umma na taasisi binafsi zinazohusiana na upokeaji na uchakataji wa taarifa katika kufuata misingi ya ulinzi wa taarifa.[69]

### 3.3.2 Sera ya Mawasiliano ya Mwaka 1997

[67] Ibid, demokrasia na utawala bora namba 198. Uk. 265
[68] Sera ya Utawala Bora ya Mwaka 2011 (lengo kuu) namba 3.3 Uk. 5
[69] Ibid Misingi ya Utawala Bora 2.2. Uk.3

Sera hii ina lengo la kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za mawasiliano katika sekta zote za kiuchumi, lakini pia kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ndani na nje ya nchi. Sera imesisitiza suala zima la kuweka mifumo madhubuti ya kisheria kwa kuitaka Serikali kuweka miongozo na Sheria za kusimamia masuala ya utoaji wa leseni kwa wawekezaji wa sekta ya habari lakini pia kulinda haki za wadau wote wa habari katika masuala ya habari pamoja na kuhakikisha kunakua na mifumo madhubuti ya kufuata misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi.[70]

### 3.3.3 Sera ya Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari ya Mwaka 2016

Sera hii ina lengo la kufanya mageuzi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia matumizi ya teknolojia ya mawasiliano ya habari katika masuala ya uhamasishaji wa habari, ulinzi na usalama, utekelezaji wa utawala bora, kuhamasisha uwekezaji nchini, kutoa nafasi za ajira n.k.[71]

Aidha, katika mikakati ya Sera hii, moja ni kuwa na mifumo ya kisheria juu ya masuala ya usimamizi wa teknolojia ya habari kwa kuhakikisha kwamba zinahamasisha matumizi ya ICT nchini, lakini pia kuwepo kwa Sheria juu ya masuala ya ulinzi wa haki za wadau wa teknolojia ya habari pamoja na kuhakikisha kunakua na mifumo madhubuti ya kufuata katika ulinzi wa taarifa binafsi.[72]

70 Sera ya Tekinologia ya Mawasiliano ya Habari ya Mwaka 2016. mifumo ya kisheria 3.10. Uk. 10
71 National Information and Communiation Technology Policy 2016. Malengo ya Sera. 2.1.3 Uk. 13
72 Ibid, mifumo a kisheria. 1.1.2. Uk. 4

### 3.3.4 Sera ya Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari ya Zanzibar Mwaka 2013.

Sera hii ina malengo ya kuhakikisha upatikanaji na utumiaji wa teknolojia ya mawasiliano ya habari kwa wazanzibari, lakini pia kuhakikisha, ICT inaingizwa katika program za masomo, kuwa na miundombinu ya kuweka ulinzi na usalama wa taarifa pamoja na ulinzi wa taarifa za mitandao katika jamii[73] Aidha, tamko la sera hii katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa katika teknolojia ya habari ni Serikali kuhakikisha inaanzisha utaratibu mzuri wa kisheria ambao utakwenda kutatua changamoto zote za teknolojia ya habari.[74]

Miongoni mwa mikakati iliyowekwa na sera hii, ili kufikia malengo ya kuwa na utaratibu mzuri wa kisheria ambao utahakikisha unakabiliana na changamoto zote za matumizi ya ICT ni pamoja na kuzuia makosa ya kimtandao, kuhusiana na ulinzi wa mteja, ulinzi wa mtoto na ulinzi wa taarifa.[75]

Vilevile, sera hii imeweka majukumu ya wadau wote wa matumizi ya ICT kwa upande wa Serikali ambayo imepewa jukumu la kuanzisha mifumo ya sheria katika kusimamia ICT kwa maslahi mapana ya umma pamoja na kulinda haki za watumiaji wa mifumo hiyo. Watumiaji ama wateja wa ICT wamepewa jukumu la kutumia mifumo hiyo kwa malengo ya maslahi ya jamii na nchi kwa ujumla pamoja na kuwa na jukumu la kufahamu juu ya haki zao, majukumu yao, na stahiki zao juu ya matumizi ya ICT.[76]

---

[73] Zanzibar Information and Communiation Technology Policy 2013. Malengo ya Sera. 2.1 Uk. 9
[74] Ibid, legal and regulatory framework. 3.8.3 policy statement. Uk. 20
[75] Ibid,3.8.4 strategies. Uk. 20
[76] Ibid, 4.2.1 role of stakeholders. Uk. 21

### 3.3.5 Sera ya Serikali Mtandao ya mwaka 2012.

Sera hii ya Serikali Mtandao ya mwaka 2012 ina malengo ya kukuza matumizi ya serikali mtandao kwa taasisi zote za umma na kuhakikisha shughuli zote zinafanywa kupitia mifumo ya ICT, lakini pia kuweka mfumo utakaorahisisha upatikanaji wa taarifa baina ya taasisi za Serikali, kuiweka karibu Serikali na wananchi katika kushiriki juu ya masuala ya kukuza uchumi, lakini pia kukuza uwazi na uwajibikaji.[77]

Miongoni mwa maeneo muhimu yaliyosisitizwa na Sera hii ni pamoja na kuanzisha mfumo wa kisheria wa kusimamia Serikali mtandao katika taasisi za Serikali ili kuweka maadili ya matumizi ya Serikali mtandao kwa watumishi wa umma. Aidha, Sera hii imesisitiza eneo muhimu la Serikali kuweka viwango maalum vya matumizi ya ICT kwa taasisi zote, kuweka viwango kwa wataalamu wa ICT, kuweka viwango vya ubora vya Serikali mtandao lakini pia kuweka viwango vya ulinzi mtandao na taarifa. Vilevile, kuweka umuhimu wa kutoa uelewa kwa wadau wote wa serikali mtandao kufahamu wajibu na haki zao.[78]

### 3.3.6 Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2018

[77] Sera ya serikali mtandao, 3.3 Malengo ya sera. Uk. 4
[78] Ibid,4 policy issues, Uk. 5

Kwa mujibu wa Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2018, dhana ya ulemavu kulingana na mkataba wa kimataifa juu ya haki za watu wenye ulemavu kwamba watu wenye ulemavu ni wale ambao wana udhaifu wa kimwili, akili au hisia, ambao unaweza kuwaathiri kwa muda mrefu au mfupi ambapo hukumbana na vikwazo na changamoto mbali mbali katika ushiriki wa masuala ya kijamii kwa misingi ya usawa na watu wengine wasio na ulemavu.[79]

Dhamira kuu ya Sera hii ni kuwa na uongozi wa kitaifa unaoelekeza ushughulikiaji wa masuala ya ulemavu kwa kuimarisha utetezi na kuwezesha ujumuishwaji wa masuala ya watu wenye Ulemavu katika mipango, sera na programu mbalimbali za ufikiaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu.[80]

Miongoni mwa changamoto ambazo Sera hii imesisitiza ni upatikanaji wa taarifa muhimu kwa watu wenye ulemavu ili kuelewa na kushiriki katika michakato ya kimaendeleo.[81] Ili watu wenye ulemavu wapate taarifa, mahitaji yao maalum lazima yaendane na mazingira. Hata hivyo, watu wenye ulemavu wana vikwazo vinavyowazuia kujiwakilisha wenyewe katika maeneo mbali mbali ikiwemo mbele ya Sheria, wanashindwa kujilinda au kujielezea wenyewe.[82]

---

[79] Sera ya watu wenye ulemavu mwaka 2018. Dhana ya ulemavu. 1.1.4 Uk. 2

[80] Ibid, dhamira namba 4.2 Uk. 23

[81] Ibid, (upatikanaji wa huduma kwa walemavu). 5.3 Uk. 27

[82] Ibid, (changamoto katika upatikanaji wa huduma kwa walemavu) Uk. 28

### 3.3.7 Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003

Sera hii ina lengo kuu la kuwa na mfumo bora zaidi wa anuani ambao umeelekezwa kwa kuweka utaratibu utakaojumuisha majina ya muhusika, majina ya mitaa pamoja na utambulisho wa majengo ili kuweza kufikisha taarifa za muhusika moja kwa moja.[83] Aidha, Sera imeweka mifumo ya ulinzi na usalama katika utoaji wa huduma za posta nchini hususan katika kuzingatia haki ya faragha ya mtu kwenye taarifa zake binafsi katika misingi mikuu ya ulinzi wa taarifa kwa mujibu wa Sheria husika.[84]

### 3.3.8 Sera ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010

Sera hii ina lengo la kufikia usimamizi bora wa utumishi wa umma pamoja na rasilimali watu, lakini pia kuhakikisha utekelezaji wa maadili na miiko ya kiutumishi kwa watumishi wa umma pamoja na kukuza uwezo wa utekelezaji wa majukumu kwa watumishi wa umma.[85] Miongoni mwa maadili ya kiutumishi kwa watumishi wa umma ni kuhakikisha utekelezaji wa misingi ya uhifadhi wa taarifa, hivyo, katika kuhakikisha ufikiaji wa malengo hayo, Sera hii imetoa mwongozo wa kuhakikisha urahisi wa upatikanaji wa taarifa kwa kuhakikisha matumizi ya uhifadhi wa taarifa, matumizi ya teknolojia ya habari pamoja na Serikali mtandao.[86]

---

[83] Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003. national address sytem. 4.4 Uk 9
[84] Ibid, postal security. 4.5. Uk 10
[85] Sera ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010
[86] Ibid,key policy objective 1.5 Uk 6

Aidha, miongoni mwa miiko mikuu ya Sera hii ni kuhakikisha utumiaji mzuri wa taarifa kwa Taasisi za Umma na watumishi wa umma.[87] Vilevile, katika masuala ya usimamizi wa mifumo ya taarifa, Sera hii ina lengo la kuhakikisha uimarishaji wa uhifadhi wa taarifa na nyaraka kwa lengo la kuisaidia Serikali katika utoaji wa huduma bora.[88]

### 3.3.9 Sera ya Afya ya Mwaka 2011

Sera hii ina lengo kuu la kuimarisha huduma za afya za kinga na tiba na kuendeleza ustawi wa watu wa Zanzibar.[89] Aidha, maeneo muhimu yaliotiliwa mkazo katika Sera hii ni utawala na uendeshaji wa sekta za afya kwa kuzitaka ziongeze ufanisi wa utoaji wa huduma bora kwa mujibu wa Sheria na kufuata misingi ya utawala bora.[90]

Kwa kuwa sekta za afya zinahusika moja kwa moja katika kupokea taarifa binafsi za watu ambazo huenda nyengine zikawa ni taarifa nyeti, Sera hii inaitaka Serikali kuhakikisha inafuata misingi ya utawala bora kwa kuweka mifumo madhubuti ya utekelezaji wa misingi hiyo na haki kwa kulinda haki ya faragha ya mtu kupitia utekelezaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi katika Taasisi za Afya.

### 3.3.10 Sera ya Elimu ya Mwaka 2006

[87] Ibid,core value 2.3 Uk 8
[88] Ibid. management information system. 7, uk 31
[89] Sera ya Afya ya Mwaka 2011. lengo kuu la Sera. 6.0 uk 18
[90] Ibid. utawala na uendeshaji wa sekta ya afya. 8.1 uk 19

Sera hii ina dhamira kutoa elimu bora na kuimarisha maisha ya kila Mzanzibari.[91] Aidha, dira na dhamira ya Sera hii ni kufikiwa na kufanikisha malengo nane (8) ya Sera hii. Moja ya malengo hayo ni kuhakikisha utekelezaji wa misingi ya utawala bora katika sekta za elimu ikiwa ni pamoja na suala la uheshimu wa haki za binaadamu na utawala wa Sheria kama ni msingi moja wapo wa utawala bora.[92]

Aidha, Taasisi za Kielimu zinahusika moja kwa moja katika kupokea taarifa binafsi za watu, Sera hii inaitaka Serikali kuhakikisha inafuata misingi ya utawala bora na kuhakikisha inaweka mifumo madhubuti ya utekelezaji wa misingi ya utawala bora na haki kwa kulinda haki ya faragha ya mtu kupitia utekelezaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi katika Taasisi za elimu.

## 3.4 Sheria za Muungano.

### 3.4.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imeorodhesha mambo 22 ya Muungano.[93] Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na masuala ya mawasiliano. Hivyo, usimamizi wa misingi ya taarifa binafsi kwa upande wa masuala ya muungano yatasimamiwa katika mifumo ya kisheria itakayoanzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

[91] Sera ya Elimu ya Mwaka 2006. mission 2.1. uk 4
[92] Ibid. education objectives. 2.3 uk 4
[93] Nyongeza ya Kwanza [mambo ya muungano]

Vilevile, kupitia Katiba hii, miongoni mwa haki muhimu ya wananchi ni haki ya faragha na usalama wa mtu[94] ambapo kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi.

Pia, Katiba imeitaka mamlaka ya nchi kuweka utaratibu wa Sheria kuhusu hali, namna na kiasi ambacho haki ya mtu ya faragha na ya usalama na nafsi yake, mali yake na maskani yake, yanaweza kuingiliwa kisheria. Vilevile, kila mtu anao uhuru wa kufanya mawasiliano na kutoingiliwa katika mawasiliano yake.[95]

### 3.4.2 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Nam. 11 ya Mwaka 2022

Sheria hii imeanzishwa kwa lengo la kuweka masharti na misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi ili kuweka kiwango cha chini cha matakwa ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi pamoja na kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi zinazochakatwa na vyombo vya Serikali na Binafsi. Hivyo, Sheria hii imezingatia mambo muhimu yafuatayo:

#### (a) Mipaka ya Matumizi ya Sheria

[94] Ibid, Ibara ya 16(1), (2)
[95] Ibid ibara ya 18(c)

Sheria hii imekusudiwa kutumika kwa upande wa Tanzania Bara na masuala ya Muungano ambayo Zanzibar inahusika kama yalivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.[96]

### (b) Tafsiri ya Maneno Muhimu

Sheria hii imetafsiri maneno "taarifa binafsi" kama ni taarifa kuhusu mtu anayetambulika ambazo zimetunzwa kwa namna yeyote, ikiwa ni pamoja na taarifa binafsi zinazohusu rangi, asili ya kitaifa au kikabila, dini, umri au hali ya ndoa ya mtu binafsi. Tafsiri imeeleza pia taarifa binafsi zinazohusu elimu, historia ya matibabu, jinai, ajira au miamala ya kifedha ya mtu binafsi; namba yoyote ya utambulisho, alama au namna nyengine maalum inayomtambulisha mtu binafsi; anwani, alama za vidole au kundi la damu la mtu binafsi; jina la mtu binafsi linaloonekana katika taarifa binafsi za mtu mwengine anayehusiana naye au pale ambapo ufichuzi wa jina hilo utadhihirisha taarifa binafsi za mtu.

Vile vile, Sheria hii imetafsiri maneno "taarifa nyeti" kama ni: taarifa ya vinasaba, taarifa inayohusu watoto, taarifa inayohusu makosa, hukumu za jinai au hatua za kiusalama, taarifa za kibayometriki; ikiwa imechakatwa, ni taarifa binafsi inayoonesha asili ya rangi au kabila. Taarifa nyeti zinajumuisha pia itikadi za kisiasa, imani za kidini au kifalsafa, ushirika, uanachama wa vyama vya wafanyakazi, jinsia na taarifa za kiafya au mahusiano ya kingono; na taarifa

[96]Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nambai 11 ya Mwaka 2022. kifungu cha 1

binafsi yeyote ambayo kwa mujibu wa Sheria za nchi inachukuliwa kuwa ina athari kubwa kwa haki na maslahi ya mhusika wa taarifa.[97]

### (c) Malengo ya Sheria

Malengo ya Sheria ni kudhibiti uchakataji wa taarifa binafsi, kuhakikisha kwamba uchakataji wa taarifa binafsi za muhusika unaongozwa na misingi ya Sheria, kulinda faragha za watu binafsi, kuweka utaratibu wa kisheria na kitaasisi wa kulinda taarifa binafsi, kuwapa wahusika wa taarifa haki katika kulinda taarifa.[98]

### (d) Misingi ya Ulinzi wa Taarifa

Sheria hii imeainisha misingi ya ulinzi wa taarifa ambayo inajumuisha kuchakatwa taarifa kihalali, uwazi, kukusanya taarifa kwa madhumuni mahususi na halali, taarifa ni sahihi na pale inapobidi, zinaboreshwa kwa kuchukua hatua zote muhimu kuhakikisha taarifa binafsi zisizo sahihi zinafutwa au kurekebishwa bila kuchelewa.

Vilevile, msingi mwengine wa ulinzi wa taarifa ni taarifa zinavyohifadhiwa, taarifa zinachakatwa kwa kuzingatia haki za mtoaji wa taarifa, taarifa zinachakatwa kwa namna ambayo itahakikisha usalama wa taarifa binafsi, kuepuka uharibifu au kuhakikisha madhara yoyote na kuhakikisha kuwa taarifa hazisafirishwi nje ya mipaka ya nchi kinyume cha masharti ya Sheria.[99]

---

[97] Ibid, kifungu cha 3
[98] Ibid, kifungu cha 4
[99] Ibid, kifungu cha 5

### (e) Uanzishwaji wa Chombo cha Usimamizi

Sheria hii imeanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi itakayokua na majukumu ya kufuatilia utekelezaji wa Sheria kwa wakusanyaji; wasajili; wakusanyaji na wachakataji wa taarifa. Chombo hiki kimepewa jukumu la kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu; kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya jambo lolote ambalo Tume itaona linaathiri ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu; kutoa elimu kwa umma kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria. Tume imepewa jukumu la kufanya tafiti na kufuatilia maendeleo ya teknolojia kuhusiana na uchakataji wa taarifa; pamoja na kuanzisha utaratibu wa ushirikiano na mamlaka za nchi nyengine zinazosimamia ulinzi wa taarifa binafsi na kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria hii.[100]

### (f) Haki za Watoa Taarifa.

Sheria hii imeweka vifungu vinavyohusiana na haki za watoa taarifa katika kufuata misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi ikiwa ni pamoja na haki ya kupata taarifa binafsi, haki ya kuzuia uchakataji unaoweza kumuathiri mtoa taarifa, haki ya kuzuia uchakataji wa taarifa binafsi kutumika kwa madhumuni ya utangazaji wa biashara, haki kuhusiana na uamuzi unaofanywa kiautomatiki, kurekebisha, kuzuia, kufuta na kuharibu taarifa binafsi. Aidha, Sheria inaeleza

[100] Ibid, kifungu cha 7

ikitokea moja ya haki hizo zimevunjwa kwa mujibu wa Sheria hii basi muhusika wa taarifa atakua na haki ya fidia.[101]

### 3.4.3 Sheria ya Mamlaka ya kusimamia Mawasiliano Tanzania Nam. 12 ya Mwaka 2003

Sheria imeanzisha Mamlaka ya Kusimamia shughuli za Mawasiliano Tanzania,[102] sheria hii inatumika kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar isipokua katika masuala ya utangazaji.[103]

Kwa mujibu wa Sheria, Mamlaka ya Mawasiliano ina kazi ya kutoa, kusajili upya na kufuta leseni za watoa huduma za mawasiliano, kuweka viwango vya utoaji huduma, kuweka viwango vya masharti ya utoaji huduma n.k.[104]

Sheria imetaja haki za wateja moja kwa moja ikiwemo haki ya ulinzi wa mawasiliano ya mtu na taarifa zake binafsi na kuweka jukumu la kuhakikisha ulinzi wa haki za wateja, kutoa mafunzo kwa Taasisi za Kimawasiliano, kujua haki na wajibu wa wateja, lakini pia kuhakikisha upatikanaji wa huduma muda wowote na kwa wateja wote.[105]

### 3.4.4 Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (R.E) Sura ya 306 ya Mwaka 2022

Sheria hii imeanzishwa kwa lengo la kuweka vifungu vya usimamizi wa huduma za mawasiliano ya kielektroniki pamoja na watoa huduma za

---

[101] Ibid,kifungu cha 33-38

[102] Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Mawasiliano Tanzania ya Mwaka 2003 kifungu cha 4

[103] Ibid, kifungu cha 2(3)(4)

[104] Ibid, kifungu cha 6

[105] Ibid kifungu cha 5

mawasiliano ya posta. Matumizi ya Sheria hii ni kwa upande wa Tanzania Bara pamoja na Tanzania Zanzibar isipokua kwa zile kazi ambazo zinasimamiwa na Kamisheni ya Utangazaji Zanzibar.[106]

Aidha, Sheria imeweka mwongozo na uwezo kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano juu ya kusimamia masuala yote ya mawasiliano ya kielektroniki na posta na kuipa jukumu la kusimamia masuala ya leseni kwa watoa huduma za mawasiliano ya kielektroniki na posta, kusimamia masuala ya uunganishaji na upatikanaji wa mitambo.[107]

Hivyo, kwa kuwa Sheria imeweka jukumu la kuhakikisha ulinzi wa taarifa, wajibu wa kutoa taarifa zinazotakiwa kwa mamlaka iliyopewa uwezo, jukumu la kuripoti wizi wa simu na laini za simu pamoja na kutoa taarifa ya mabadiliko ya umiliki simu au laini ya simu.[108]

Kwa upande wa ulinzi wa mawasiliano ya posta, Sheria imeweka kuwa ni kosa kuharibu au kuvunja boksi la habari, kufungua au kusoma taarifa bila ya ruhusa ya kisheria n.k.[109]

---

106 Sheria ya mawasiliano ya kielektroniki na posta (R.E) ya Mwaka 2022 kifungu cha 2

107 Ibid. PART II & III

108 Ibid. kufungu cha 98-102

109 Ibid, kifungu cha 138-150

### 3.4.5 Sheria ya Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote Nam .11 ya Mwaka 2006

Sheria hii ina lengo la kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kwa wote. Sheria hii inatumika kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar katika masuala ya kifedha juu ya kukuza mawasiliano katika maeneo yanayohusika na maeneo ya mitambo ya huduma, isipokua katika masuala ya utangazaji.[110] Sheria imeanzisha mfuko maalum wenye lengo la kutumika katika masuala ya kukuza mawasiliano Tanzania[111]ambao utasimamiwa na bodi ambayo mjumbe mmoja anatoka Zanzibar.[112]

Aidha, sheria hii katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa, imeweka utaratibu wa kutumia huduma za mawasiliano bila ya udhalilishaji wa aina yoyote, lakini pia, watoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote wamepewa uwezo wa kishera wa kukataa kutoa huduma ya upatikanaji wa mawasiliano kutokana na sababu maalum kwa mujibu wa sheria.[113] Vilevile, wawezeshaji wa huduma za mawasiliano kwa wote wamepewa uwezo wa kisheria kwa wao kuagiza kupatiwa taarifa za mtu yoyote kwa mujibu wa sheria.[114]

### 3.4.6 Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha Nam. 5 ya Mwaka 2006

---

[110] Sheria ya Mawasiliano kwa Wote ya Mwaka 2006. Kifungu cha 2

[111] Ibid, kifungu cha 4

[112] Ibid, kifungu cha 7

[113] Ibid, kifungu cha 14(1) (3)

[114] Ibid, kifungu cha 20

Sheria imeweka utaratibu bora wa kuongoza na kusimamia masuala yote ya kifedha kwa upande wa Mabenki pamoja na Taasisi za Kifedha. Sheria hii itatumika kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.[115]

Benki pamoja na Taasisi nyengine za Kifedha, ni katika maeneo ambayo moja kwa moja yanapokea na kusimamia taarifa binafsi pamoja na haki za watu, katika kuhakikisha utekelezaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi, Sheria hii imeweka utaratibu wa kuzitaka Benki zote na Taasisi zote za Kifedha kuhakikisha usalama wa taarifa binafsi pamoja na maslahi ya mteja isipokua kwa mujibu wa taratibu za Sheria.[116]

Aidha, Sheria imeweka utaratibu wa kuweka akaunti za kuwahakikishia wateja usalama wa fedha na amana zao na kuhakikisha akaunti hizo haziwezi kudhurika na kufanya miamala ya kifedha wakati wowote na katika mazingira yeyote.[117]

### 3.4.7 Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 ya Mwaka 2016

Sheria hii imeanzisha Idara ya Huduma za Uhamiaji ambayo imepewa majukumu na uwezo wa Kisheria wa kuratibu uingiaji na utokaji wa wageni ndani ya nchi, kulinda mipaka ya nchi, kuchunguza matukio ya jinai ya wazawa

---

[115] Sheria ya benki na taasisi za kifedha Nam. 5 ya mwaka 2006, kifungu cha 2
[116] Ibid, kifungu cha 48
[117] Ibid, kifungu cha 36

na wahamiaji yanayohusiana na shughuli za uhamiaji, kuchukua taarifa zote zinazohusiana na uchakataji wa taarifa za paspoti n.k.[118]

Aidha, Idara imepewa uwezo wa kutekeleza majukumu yake sehemu yeyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi nyengine yeyote kwa kuzingatia mipaka ya Idara.[119]Hivyo, kwa vile Sheria hii ina Mamlaka ya Kisheria ya kuchukua taarifa binafsi za watu, lakini pia kuchunguza na kutafuta taarifa muhimu za watu zinazohusiana na masuala ya uhamiaji, imeweka utaratibu wa kuhakikisha utekelezaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa kuwapa wajibu maafisa wa uhamiaji wa kulinda taarifa za mtu kwa kutozitoa kwa mtu yeyote au chombo chochote kinyume na Sheria.[120]

Sheria hii itatumika kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar,[121]na imeanzisha makosa yanayohusiana na mitandao pamoja na matumizi ya teknolojia ya habari. Lakini pia sheria hii imeweka uwezo wa kufanya uchunguzi wa taarifa, ukusanyaji na utumiaji wa ushahidi wa kielektroniki juu ya makosa ya mtandao.

Katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi za watumiaji wa mitandao, sheria imeweka vifungu vya makosa mbali mbali kuhusiana na mitandao kama vile kupata taarifa ya mtu kinyume na sheria, kutumia mifumo ya kompyuta muda unaoruhusiwa na mmiliki wa kompyuta, kuingilia taarifa kinyume na sheria

[118] Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 ya Mwaka 2016
[119] Ibid, kichungu cha 13
[120] Ibid,kifungu cha 15
[121] Sheria ya Makosa ya Mtandao Nam. 14 ya Mwaka 2015, kifungu cha 2

kwa kuharibu, kuifuta au kuibadilisha, kutumia kifaa chochote cha kompyuta kwa ajili ya kutenda kosa.

Aidha, sheria hii katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi katika mitandao, imeweka makosa ya mitandao kuonesha picha za mtoto katika mitandao, au kuzisambaza picha za mtoto, kuweka picha za kimapenzi, kutoa taarifa za uongo, kutoa taarifa za uchunguzi n.k. Hivyo, Sheria hii imeweka kuwa ni makosa ya jinai kutenda kosa lolote kwa mujibu wa sheria na atakayetiwa hatiani atatumikia adhabu ya kifungo au faini au vyote kwa pamoja.[122]

## 3.5 Sheria za Zanzibar

### 3.5.1 Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984

Katiba ya Zanzibar katika Sura ya Tatu inazungumzia kinga ya haki za lazima, wajibu na uhuru wa mtu binafri na imesisitiza juu ya haki ya faragha ya mtu na usalama wake[123] ambapo kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi.[124]

Pia, Katiba imeitaka kuwekwa usalama kuhusu hali, namna na kiasi ambacho haki ya mtu ya faragha na ya usalama na nafsi yake, mali yake na maskani yake,

---

[122] Ibid,
[123] Ibid, kifungu cha 15(1), (2)
[124] Ibid

yaweza kuingiliwa kisheria. Vilevile, kila mtu anao uhuru wa kufanya mawasiliano na kutoingiliwa katika mawasiliano yake.[125]

### 3.5.2 Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya Mwaka 2018

Sheria imeanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar,[126]ambayo imepewa jukumu la kusajili, kuhifadhi kumbukumbu na kutoa vyeti vya matukio ya kijamii kama vile cheti cha kuzaliwa, cheti cha kifo, cheti cha ndoa na talaka pamoja vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi.[127]

Aidha, Sheria imeipa jukumu wakala la kukusanya, kutoa, kuchambua na kusambaza taarifa zilizokusanywa kwa mujibu wa Sheria na kuzizalisha kadri zitakavyohitajika muda hadi muda.[128]

Sheria imeweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa Wakala inatekeleza misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa kuweka majukumu yake katika kuhakikisha uhifadhi, ulinzi na usalama wa taarifa yoyote au taarifa iliyokusanywa, iliyopatikana au iliyohifadhiwa katika rejista.[129]

---

[125] Ibid, kifungu cha 18(1)

[126] Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar Nam. 3 ya Mwaka 2018, kifungu cha 3

[127] Ibid, kifungu cha 4(1) (a)

[128] Ibid, kifungu cha 4(1) (c)

[129] Ibid, kifungu cha 4(1) (h)

Aidha, katika kuhakikisha utekelezaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi, Sheria hii imeweka vifungu vya makosa na adhabu zake ikiwa miongoni mwa makosa hayo ni kuongeza au kufanya marekebisho kwenye cheti au kitambulisho kinyume na Sheria au kuruhusu mtu kutumia cheti au kitambulisho kilichotolewa kwa mtu mwengine, na endapo mtu huyo atatiwa hatiani atakuwa amefanya kosa kisheria na atatakiwa kulipa faini isiyopungua milioni 3 na isiyozidi milioni 5 au kifungo kisichopungua miaka 3 na kisichozidi miaka 5 au adhabu zote mbili.[130]

Kwa upande wa taasisi, ikitenda kosa lolote lililowekwa chini ya sheria, itakapotiwa hatiani italipa faini isiyopungua milioni kumi. Aidha, ikiwa kosa hilo limetendwa na mkurugenzi au afisa yeyote mwenye dhamana kwa majukumu ya taasisi, atatiwa hatiani kwa kosa hilo na ataadhibiwa kwa Sheria husika.[131]

### 3.5.3 Sheria ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Nam 13 ya Mwaka 2012

Sheria imeanzisha Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali,[132] ambayo itakua na jukumu la kuhakikisha ubora na ufanisi katika usimamizi wa utekelezaji na

[130] Ibid. kifungu cha 53(3)
[131] Ibid. kifungu cha 53(5)
[132] Sheria ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali No 13 ya Mwaka 2012. Kifungu cha 3

uwajibikaji wa Sheria zote zinazohusiana na masuala ya usajili wa biashara na mali.[133]

Kutokana na Sheria hii kuhusiana na usimamizi wa masuala ya taarifa binafsi za watu, katika kuhakikisha kua wapokeaji wa taarifa hizo wanazingatia misingi ya ulinzi wa taarifa hizo, wakala atatakiwa kuhakikisha anafuata na kusimamia misingi ya utoaji wa huduma kwa wateja wake na kwa wananchi wote kwa ujumla.[134]

### 3.5.4 Sheria ya Mamlaka ya Tawala za Mikoa Nam. 7 ya Mwaka 2014

Sheria imeanzishwa kwa lengo la kuanzisha Serikali za Mitaa, uwezo wake wa kisheria, kazi na wajibu wa Serikali za mitaa pamoja na mambo mengine yanayohusiana na Serikali za Mitaa. Moja ya majukumu ya Serikali za Mitaa ambalo moja kwa moja linahusisha taarifa binafsi za watu ni kutoa leseni, kuratibu pamoja na kudhibiti shughuli za kibiahara ndani ya mipaka yake.[135] Sheria inataka uwepo wa misingi ya uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu na uratibu wa shughuli mbali mbali.[136]

---

[133] Ibid. kifungu cha 4(1)
[134] Ibid kifungu cha 4(3)
[135] Sheria ya Mamlaka ya Tawala za Mikoa Nam. 7 ya Mwaka 2014. Kifungu cha 21, 23

[136] Ibid, kifungu cha 8

### 3.5.5 Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam 7 ya Mwaka 2018

Sheria hii imeweka utaratibu bora wa uendeshaji wa mchakato wa makosa ya jinai kwa upande wa upelelezi na usikilizwaji wa kesi za jinai ambapo vyombo vya msingi vinavyohusika moja kwa moja na kwa kiasi kikubwa katika mchakato huu ni Jeshi la Polisi, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Mahakama.

Sheria hii imeweka utaratibu wa kupata taarifa za simu au posta kwa kumpa uwezo hakimu kuitaka taasisi ya simu au posta kuwasilisha taarifa hizo.[137]

Aidha, kwa upande wa taarifa za kifedha, Sheria hii imempa uwezo Mkurugenzi wa Mashtaka kupitia amri ya maandishi kumuidhinisha afisa polisi mwenye cheo ambacho si kisicho chini ya Mkaguzi M saidizi kufanya uchunguzi wa hesabu hizo.[138]

Vilevile, kwa upande wa upekuzi au uchukuaji wa taarifa za kompyuta zilizothibitishwa na hati ya kiapo kuwa zina uhusiano na kosa, hakimu amepewa uwezo wa kumuidhinisha afisa polisi kwa ajili ya kufanya uchunguzi huo wa taarifa.[139]

---

[137] Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2018, kifungu cha 133
[138] Ibid, kifungu cha 134
[139] Ibid. kifungu cha 135

### 3.5.6 Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya Mwaka 2011

Sheria hii imeanzishwa kwa lengo la kuweka miundo, uendeshaji na usimamizi wa Taasisi zote za Umma na katika mambo mengine yote yanayohusiana na utumishi wa umma.[140]

Kutokana na Sheria hii kuhusika na usimamiaji wa Taasisi zote za Serikali katika masuala ya kiutumishi ambazo zote zinahusiana kwa namna moja ama nyengine katika kuchukua taarifa binafsi za watu ambazo zinaweza kuwa za watumishi au za wataka huduma, Sheria hii imeweka utaratibu wa kuhakikisha utekelezaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa kwa kuweka kifungu maalum cha miiko ya utumishi ambapo miongoni mwa miiko hiyo ni heshima kwa wote inafuatwa, kuheshimu Sheria za nchi lakini pia matumizi sahihi ya taarifa rasmi.[141]

### 3.5.7 Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya Mwaka 2015

Sheria hii imeweka misingi ya kimaadili ya Viongozi wa Umma[142] na inapokea na kuhifadhi taarifa za Viongozi wa Umma pamoja na kupokea malalamiko na kufanya uchunguzi dhidi ya uvunjaji wa maadili kwa Viongozi wa Umma.[143]

[140] Sheria ya utumishi wa umma No 2 ya Mwaka 2011. Kifungu cha 2
[141] Ibid. kifungu cha 5
[142] Sheria ya maadili ya viongozi wa umma No. 4 ya 20015. Kifungu cha 4
[143] Ibid. kifungu cha 12(1)

Miongoni mwa maadili ambayo Sheria hii imeweka kwa Viongozi wa Umma ni pamoja na kutokutoa siri za kiutumishi na Serikali kwa ujumla.[144]Hivyo, utakuwa ni ukiukwaji wa maadili kwa kiongozi wa umma kutoa taarifa yoyote ambayo ameipata katika kutekeleza majukumu yake au kutoa taarifa yeyote kwa mtu asiyestahiki.[145]

Aidha, Sheria hii imeweka adhabu kwa Viongozi wa Umma watakaokwenda kinyume na maadili ya uongozi kwa kupewa onyo, kusimamishwa kazi, kufukuzwa kazi, kumshauri kiongozi kujiuzulu, kupunguziwa mshahara n.k.[146]

### 3.5.8 Sheria ya Uchaguzi Nam. 4 ya 2018.

Sheria hii imeanzisha Tume ya Uchaguzi kwa upande wa Zanzibar ili kusimamia na kuendesha mwenendo mzima wa uchaguzi na kura ya maoni, kuandaa, kutayarisha, kuhifadhi na kuendeleza daftatri, kutangaza matokeo ya uchaguzi na kura za maoni n.k.[147]

Aidha, Sheria hii imeweka utaratibu madhubuti wa usafirishaji wa taarifa ikiwa mpiga kura atahama kutoka katika Shehia moja kwenda nyengine atatakiwa

[144] Ibid. kifungu cha 18(iv)
[145] Ibid. kifungu cha 20 (a), (b)
[146] Ibid. kifungu cha 30
[147] Sheria ya uchaguzi No 4 ya 2018. Kifungu cha 4

kuomba uhamisho huo kwa afisa uandikishaji kusimamia zoezi hilo kwa mujibu wa Sheria.[148]

Vilevile, Sheria imewataka wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wa vituo katika kuhakikisha usalama na ulinzi wa taarifa, watakula viapo vya kutunza siri na uadilifu mbele ya Hakimu wa Mkoa.[149]

### 3.5.9 Sheria ya Msaada wa Kisheria Nam. 13 ya Mwaka 2018

Sheria imeweka masharti yanayosimamia utoaji wa huduma za msaada wa kisheria. Miongoni mwa kazi za Idara ni kutoa miongozo ya kisera kwa watoa huduma za kisheria, kusajili watoaji wa huduma za kisheria.[150]

Katika kuhakikisha utekelezaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa, Sheria hii imeweka utaratibu wa kusajili watoaji wa msaada wa kisheria na kuweka kumbukumbu na taarifa zinazohusiana na watoaji huduma za msaada wa kisheria.[151]

Sheria hii imempa mamlaka Waziri kutunga kanuni za utendaji katika maeneo mbalimbali ikiwemo kulinda haki na maslahi ya mtu asiyekua na uwezo, wajibu wa mtu asiyekua na uwezo, kulinda siri, uadilifu na mwenendo wa maadili.[152]

[148] Ibid. kifungu cha 29
[149] Ibid. kifungu cha 36(5)
[150] Ibid. kifungu cha 4
[151] Ibid. kifungu cha 4(c), (d)
[152] Ibid. kifungu cha 21(4)

### 3.5.10 Sheria ya Usimamizi na Kujikinga na Ukimwi Zanzibar Nam. 18 ya Mwaka 2013.

Sheria hii imeanzishwa kwa lengo la kuweka usimamizi na misingi ya kujikinga na ukimwi, kulinda na kukuza haki za wanaoishi na ukimwi pamoja na virusi vya ukimwi. Aidha, Sheria inatoa majukumu Tume ya Ukimwi ya kutoa elimu juu ya masuala ya kujikinga, na mazingira bora ya kuishi na ukimwi pamoja na virusi vya ukimwi, kulinda na kukuza uelewa wa haki za waathirika wa ukimwi n.k.[153]

Katika kuhakikisha utekelezaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa, Sheria imeweka utaratibu kwa watoa huduma za afya kulinda taarifa za watoa damu kuhusiana na majibu ya ukimwi.[154] Sheria pia imetambua kuwa kila mtu anastahili haki ya faragha na ni kosa la kisheria kwa mtu yeyote atakayetoa taarifa binafsi za mtu kuhusiana na majibu yake ya ukimwi kutoa taarifa hizo kwa mtu mwengine isipokuwa ya majibu ni mtoto au mlemavu ambaye hatoweza kufahamu majibu yake, au kwa amri ya mahakama.[155]

Vilevile, Sheria imeweka adhabu kwa mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa la kutoa taarifa za mtu binafsi kuhusiana na majibu yake ya ukimwi, atatakiwa kulipa faini isiyopungua milioni moja na laki tano au kifungo kisichopungua miezi 18 au adhabu zote mbili.[156]

---

[153] Sheria ya Usimamizi na Msaada wa Kujilinda na Ukimwi Zanzibar ya Nam 18 ya Mwaka 2013. kifungu cha 3

[154] Ibid, kifungu cha 12(3)

[155] Ibid, kifungu cha 24(1), (2), (3), (4)

[156] Ibid, kifungu cha 24(5)

### 3.5.11 Sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar Nam. 1 ya Mwaka 2012

Sheria hii imeanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ambayo imepewa jukumu la kupokea taarifa zinazohusiana na masuala ya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar, kufanya uchunguzi juu ya taarifa za rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar, na matendo ya mshukiwa wa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar.[157] vile vile, Mamlaka hii imepewa uwezo wa kumtaka mtu yeyote au chombo chochote kutoa taarifa zozote muhimu kwa ajili ya kufanyiwa upelelezi n.k.[158]

Katika kuhakikisha kuwa Mamlaka inatekeleza misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi, ikiwa ni chombo maalum ambacho kinahusika na taarifa nyeti za Watumishi wa Umma, Viongozi wa Umma, Taasisi Binafsi na Taasisi za Umma pamoja na wananchi kwa ujumla, Sheria hii imeweka utaratibu kwa afisa yeyote mwenye mamlaka kutokutoa taarifa yeyote iliyopatikana katika uchunguzi uliofanywa na Mamlaka isipokua kwa ruhusa ya Mkurugenzi Mkuu au kwa uhalali wa utekelezaji wa Sheria nyengine yeyote.[159]

---

157 Sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar Nam 1 ya Mwaka 2012. Kifungu cha 13

158 Ibid. kifungu cha 14

159 Ibid. kifungu cha 29(1)

Aidha, Sheria hii imeweka adhabu kwa atakayetoa taarifa za uchunguzi kinyume na Sheria, na atakapotiwa hatiani atatozwa faini isiyozidi milioni moja au kifungo kisichozidi miaka 2 au adhabu zote mbili.[160]

### 3.5.12 Sheria ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Nam. 10 ya Mwaka 2011

Sheria hii inaanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali[161] ambayo imepewa jukumu kuu la kuishauri na kutoa maelezo kwa Serikali juu ya masuala ya kisayansi pamoja na majibu ya vipimo vya madawa, chakula, madawa ya kulevya na kemikali.[162]

Kwavile, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni chombo maalum ambacho kinahusiana na upokeaji na uchakataji wa taarifa ikiwemo taarifa binafsi za watu, Sheria hii imeweka utaratibu wa kutekeleza misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa kuitaka maabara kuhifadhi na kutunza usiri wa taarifa za majibu ya vipimo vya maabara isipokuwa kwa kutekeleza matakwa ya Sheria za nchi.[163]

Aidha, Sheria hii imeweka adhabu kwa mtu yeyote aliyeajiriwa kufanya kazi katika Maabara atakayetoa taarifa za maabara ambazo ni taarifa nyeti kama vile matokeo ya vipimo vya afya au vinasaba kinyume na Sheria, na atakapotiwa

---

[160] Ibid. kifungu cha 29(2)
[161] Sheria ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Nam 10 ya Mwaka 2011. Kifungu cha 3
[162] Ibid. kifungu cha 5
[163] Ibid. kifungu cha 7

hatiani atatakiwa kulipa faini isiyopungua milioni 3 na isiyozidi milioni 5 au kifungo kisichopungua miaka 2 na kisichozidi miaka 5 au adhabu zote mbili.[164]

### 3.5.13 Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Nyaraka Zanzibar Nam. 3 ya Mwaka 2008

Sheria hii imeanzisha Taasisi ya Rekodi za Nyaraka Zanzibar[165] ambayo itakuwa na jukumu la kuhakikisha Taasisi za Umma zinafuata mfumo wa kuhifadhi nyaraka, kusimamia utekelezaji wa taratibu za uvunjwaji na uharibifu wa nyaraka lakini pia kutoa ushauri kwa Taasisi za Serikali juu ya mfumo wa kuhifadhi nyaraka.[166]

Katika kuhakikisha utekelezaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa, Sheria hii imeweka kuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuhamisha au kuharibu taarifa au nyaraka, au mtu yeyote kusafirisha taarifa au nyaraka nje ya Zanzibar kinyume na Sheria, na akitiwa hatiani atatakiwa kulipa faini isiyopungua laki 5 au kifungo kisichopungua miezi 12 au adhabu zote mbili.[167]

[164] Ibid. kifungu cha 24(1)
[165] Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Rekodi za Nyaraka Zanzibar Nam 3 ya Mwaka 2008. Kifungu cha 4
[166] Ibid. kifungu cha 5
[167] Ibid. kifungu cha 24-25

### 3.5.14 Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara Nam. 12 ya mwaka 2012

Sheria hii imeanzisha Afisi ya Mrajis wa Taasisi za Biashara[168] pamoja na kuweka vifungu vitakavyosimamia masuala yote yanayohusiana na usajili wa taasisi za biashara Zanzibar. Matumizi ya sheria hii yatatumika kwa usajili wa kampuni, biashara za ubia, mashirika pamoja na asasi za kijamii.[169] Katika sheria hii, Mrajis amepewa jukumu la kusajili majina ya biashara, kutoa uthibitisho unaojitegemea wa kila taasisi, kuhifadhi taarifa zao pamoja na kusimamia Rejista hizo.[170]

Kwa vile sheria hii inahusika na ukusanyaji wa taarifa binafsi za vyombo mbali mbali vya biashara, sheria hii katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa hizo imeweka utaratibu wa kuweka majukumu kwa chombo kinachotaka kusajiliwa kutoa taarifa zilizo sahihi, jukumu la kutoa maelezo ya marekebisho ya maelezo yeyote ya chombo kilichosajiliwa, lakini pia kuweka makosa na adhabu kwa chombo chochote kitakachokwenda kinyume na sheria.[171]

Aidha, wamiliki wa vyombo hivyo watakuwa na haki ya kutumia majina yao kama ni haki yao katika masuala yote ya kibiashara pasipo kuingiliwa na mtu

[168] Sheria ya usajili wa biashara. Kif cha 4
[169] Ibid. kifungu cha 2
[170] Ibid. kifungu cha 5
[171] Ibid. kifungu cha 7

mwengine.[172] Pia kuweka kuwa ni kosa kwa kitendo chochote kitakachofanywa na afisa na kupelekea kupotea au kuharibika kwa taarifa.[173]

Sheria hii mbali ya kuwa inahusika na taarifa binafsi za usajili wa vyombo hivyo vya biashara, imeweka utaratibu wa kisheria kuwa taarifa zote zilizosajiliwa katika rejista kuwa ni taarifa za umma.[174]

### 3.5.15 Sheria ya Udhibiti wa Mali Haramu Nam. 10 ya mwaka 2009

Sheria hii imeweka masharti ya kisheria ya udhibiti wa mali haramu, masharti ya kumtia mtu hatiani kwa kosa la umiliki wa mali haramu,[175] pamoja na kuhalalisha adhabu kwa muhalifu mara baada ya kutiwa hatiani.[176]

Sheria hii imewapa uwezo wa kisheria watoa taarifa za uhalifu huo wa umiliki wa mali haramu katika kutoa taarifa za wateja wao wanaoshukiwa kwa makosa. Miongoni mwa taarifa hizo ni pamoja na vitambulisho vyao, hati zao za kusafiria, akaunti za benki, vyeti vya kuzaliwa, kwa upande wa kampuni kutoa taarifa za vyeti vya usajili, au viambatanisho vyovyote ambavyo zitaorodheshwa na Waziri katika kanuni.[177]

Sheria hii katika kuhakikisha misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi, imeweka utaratibu wa kisheria kwa kuweka masharti kwa watoa taarifa kuwapa

[172] Ibid. kifungu cha 9
[173] Ibid. kifungu cha 22
[174] Ibid. kifungu cha 18
[175] Sheria ya udhibiti wa mali haramu. Nam 10 ya mwaka 2009. Kifungu cha 7
[176] Ibid. kifungu cha 8
[177] Ibid. kifungu cha 10

mafunzo maafisa na waajiriwa wote kutoka katika taasisi zao kufahamu namna ya ushughulikiaji wa kesi za umiliki wa mali haramu, pia kuwawekea mipaka kwa mtu yeyote kufungua, kutumia au kutoa taarifa za mtu asiyekuwa sahihi au watoa taarifa wengine.

Hivyo, sheria imeweka utaratibu kuwa afisa yeyote atakapokwenda kinyume na masharti ya sheria hii atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu kwa mujibu wa sheria.[178]

### 3.5.16 Sheria ya Usajili wa Mali zinazohamishika Nam. 4 ya Mwaka 2011.

Sheria hii imeanzisha Afisi ya Mrajis atakayesimamia Afisi ya Msajili wa Umiliki wa Mali zinazohamishika kwa lengo la kusajili makubaliano yeyote yatakayofanywa juu ya mali hiyo kwa kuzingatia sheria za Zanzibar.[179]

Majukumu ya Mrajis kwa mujibu wa sheria hii ni kusajili makubaliano ya umiliki wa mali zinazohamishika, kuweka taarifa za kila siku katika Rejista, pamoja na kusimamia Rejista.[180]

[178] Ibid. kifungu cha 14(2) (3)
[179] Sheria ya usajili wa mali zinazohamishika nam. 4 ya mwaka 2010. Kifungu cha 4, 5.
[180] Ibid. kifungu cha 6

Sheria hii ni moja ya sheria zinazohusika na upokeaji wa taarifa binafsi Zanzibar, na katika kuhakikisha misingi ya ulinzi wa taarifa za wananchi au taasisi zinakuwa salama, imeweka utaratibu wa kisheria kwa kumpa jukumu Mrajis la kuhifadhi makubaliano, usajili pamoja na taarifa zote katika njia iliyokuwa salama.[181]

Aidha, katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi, sheria hii imempa uwezo Waziri anaeshughulikia masuala ya mawasiliano wa kutunga kanuni za utekelezaji mzuri wa sheria hii juu ya masuala mbali mbali ilkiwemo kuweka taratibu za kufanya upelelezi pamoja na taratibu za kutoa taarifa za mtu binafsi.[182]

### 3.5.17 Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar Nam. 9 ya Mwaka 2006.

Sheria hii inasimamia haki na stahiki zote za watu wenye ulemavu na inatumika katika kutekeleza masharti ya sheria kwa taasisi za Serikali, taasisi zisizo za Serikali pamoja na watu binafsi.[183]

[181] Ibid. kifungu cha 6 (d)
[182] Ibid. kifungu cha 34 (e) (d)
[183] Sheria ya watu wenye ulemavu. Nam 9 ya mwaka 2006. Kifungu cha 2

Katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi kwa watu wenye ulemavu, sheria hii imeweka utaratibu wa kisheria wa kuwawezesha walemavu kuweza kupata haki ya mawasiliano au kutoa taarifa kwa kukuza utumiaji wa lugha za ishara nchini.[184]

### 3.5.18 Sheria ya Adhabu ya Nam. 6 ya Mwaka 2018

Sheria hii inaainisha makosa mbali mbali na adhabu zake, kwa upande wa kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi, sheria hii imeweka makosa yanayohusiana na taarifa kwa kuweka utaratibu wa kisheria dhidi ya mtu yeyote ambaye bila idhini anabadilisha vifaa au vitu vinavyotumika au vitakavyotumika ndani ya kompyuta au ataharibu kompyuta au vifaa vya kompyuta, atakuwa ni mkosa.[185]

Aidha, sheria imeweka kosa dhidi ya mtu yeyote ambaye ataharibu au atabadilisha taarifa, atazifanya taarifa kuwa haziwezi kutumika, atakataa kutoa au atamzuia mtu kuchukua taarifa kisheria, atakuwa ni mkosa.[186]

Vilevile, sheria imeweka kosa dhidi ya mtu yeyote atakayeingilia kati mfumo wa kompyuta au taarifa isiyomuhusu bila ya sababu za msingi kwa kuzuia utendaji kazi wa mfumo kwa namna yeyote au kumzuia mtumiaji halali wa

---

[184] Ibid. kifungu cha 15(d)
[185] Ibid. kifungu cha 370-371.
[186] Ibid. kifungu cha 372

kompyuta au kuingilia mawasiliano yeyote yasiyo ya umma atakuwa ni mkosa.[187]

### 3.5.19 Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya Mwaka 2011

Sheria hii imeanzishwa kwa lengo la kusimamia haki za watoto Zanzibar. Sheria hii inajumuisha mambo mbalimbali ya kukuza, kulinda, na kuhifadhi ustawi wa mtoto, masharti ya uwajibishaji kwa mzee wa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa, masuala ya kulea, kuasili na uangalizi wa mtoto pamoja na haki nyengine za msingi kwa mtoto.

Kwa upande wa haki ya faragha ya mtoto, hususan katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi za mtoto, Sheria imeweka utaratibu wa kumpa haki mtoto akiwa katika ukuaji wake, kuweza kushiriki katika mambo mbali mbali yanayomuhusu, ikiwa ni pamoja na masuala ya kujieleza.[188]

Aidha, Sheria imeweka utaratibu wa kusajili jina na tarehe ya kuzaliwa mtoto kwa kushirikiana na taasisi zote zinazohusika kufanikisha usajili huo,[189] haki hii ni ulinzi tosha wa taarifa binafsi kwa mtoto ambapo taarifa zake hizo huhifadhiwa na kuzitumia wakati wowote wa maisha yake katika masuala tofauti ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

[187] Ibid. kifungu cha 373-374
[188] Sheria ya watoto nam. 6 ya mwaka 2011. kifungu cha 5
[189] Ibid. kifungu cha 8

Sheria hii imeweka wajibu kwa kila mtu kutoa taarifa ya ukiukwaji wa haki za mtoto kwa mtu yeyote kwa Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii, Afisa wa Ustawi wa Jamii, Polisi au kwa Sheha.[190]

### 3.5.20 Sheria ya Ushahidi Nam. 9 ya mwaka 2019

Sheria hii imeweka utaratibu wa kusimamia taratibu za kutoa ushahidi unaokubalika mbele ya mahkama kwa kesi za jinai na madai. Sheria hii ya ushahidi haikuweka vifungu vya moja kwa moja vya misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi, ila imeweka vifungu vya kuorodhesha taarifa muhimu kwa ushahidi na taarifa ambazo haziwezi kuchukuliwa kama ni ushahidi.

Miongoni mwa taarifa ambazo sheria hii imeziweka kama ni taarifa muhimu kwa ushahidi ni pamoja na ushahidi unaoweza kutolewa kwa matukio yanayobishaniwa na yanayohusiana na kesi, taarifa za uhusiano wa matukio yanayofanya sehemu ya tukio, sababu za matukio au athari za matukio yanayobishaniwa, dhamira, maandalizi na hisia za kabla au baada ya tukio, vitu vilivyofanywa au kusemwa na wanaokula njama n.k.[191]

Aidha, sheria hii imeweka pia utaratibu wa kisheria kuorodhesha baadhi ya taarifa ambazo hazitazingatiwa katika ushahidi dhidi ya jambo linalobishaniwa, kama vile taarifa za mtu aliyefariki, taarifa za mtu asiyeweza kupatikana, taarifa za mtu asiyeweza kutoa ushahidi.[192]

---

[190] Ibid. kifungu cha 20
[191] Sheria ya Ushahidi Nam. 9 ya Mwaka 2016, kifungu cha 4-15
[192] Ibid, kifungu cha 32

### 3.5.21 Sheria ya Ajira Nam. 11 ya Mwaka 2005.

Sheria hii imefuta sheria ya Ajira ya Nam. 3 ya mwaka 1997 na kuanzisha sheria mpya ya ajira ambayo imeweka utaratibu wa kisheria wa kuweka haki za msingi za wafanyakazi pamoja na kuweka viwango bora vya ajira na mambo yanayohusiana na ajira.

Katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi za wafanyakazi, sheria hii imeweka utaratibu wa kisheria wa kuweka usiri kwa mpelelezi au afisa kazi yeyote wakati wa kutekeleza majukumu yao, kuhakikisha usiri wa taarifa kwa kutozitumia, kuzitoa au kiziweka wazi isipokuwa kwa ajili ya utekeleza wa sheria yeyote Zanzibar.[193]

Aidha, sheria hii imeweka kifungu cha kosa na adhabu kwa mkaguzi au afisa wa kazi yeyote atakaevunja masharti ya usiri kwa mujibu wa sheria hii, na atakapotiwa hatiani atatakiwa kulipa faini isiyopungua laki 2 au kifungo kisichupungua miezi mitatu.[194]

[193] Sheria ya Ajira Nam. 11 ya Mwaka 2005, kifungu cha 20(1), (2), (3)
[194] Ibid, kifungu cha 20

## SURA YA NNE.

### 4.0 MAONI YA WADAU.

### 4.1 Utangulizi.

Katika utafiti huu maoni ya wadau mbalimbali yalikusanywa katika vikao vilivyoitishwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar kwa kushirikiana na taasisi nyengine. Tume imeshirikisha Taasisi mbali mbali za Serikali na za watu Binafsi kutoka Pemba na Unguja. Wadau walitoa mapendekezo ambayo yalizingatia maeneo yafuatayo:

### 4.2 Maoni ya Kisera.

Wadau wameshauri kuwa ipo haja ya kutungwa kwa Sera ya kitaifa itakayohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi. Wadau hao wamependekeza Sera hiyo iainishe mikakati ya kila taasisi inayoshughulika na ukusanyaji, uchukuaji, uhifadhi, ubadilishanaji, uchakataji na utumiaji wa taarifa binafsi.

Aidha wadau hao wameshauri pia Sera hiyo iweke wajibu wa kuanzishwa kwa chombo maalum cha usimamizi na udhibiti wa ulinzi wa taarifa binafsi ambacho kitakuwa ni chombo cha usimamizi na ufuatiliaji.

Imependekezwa Sera hiyo iweke kazi na uwezo wa kila taasisi inayochukua, na kuchakata taarifa za watu binafsi pia iainishe mipaka ya kila taasisi ili kuepusha muingiliano wa majukumu. Wadau wamependekeza Sera itoe fursa ya kufanyika kwa tafiti mbalimbali zinazohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi Zanzibar.

#### 4.2.1. Kuandaliwe masharti ya ulinzi wa taarifa binafsi

Wadau wamependekeza Sera ielekeze namna ya kutoa taarifa kwa taasisi zote za umma na binafsi zinazohusiana na uchukuaji, uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi kwa kuweka masharti (matamko) yatakayolinda taarifa za watu kwa kutokuleta madhara yanayoweza kusababisha kushusha hadhi na utu wa watu. .

### 4.3 Maoni ya Kisheria

1. **Umuhimu wa kutungwa sheria maalum inayohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi**

Wadau wameshauri kutungwa kwa sheria maalum itakayoweza kuweka ulinzi wa kutosha wa taarifa za watu binafsi Zanzibar. Sheria hiyo isimamie taasisi zote zinazokusanya, kuhifadhi na kuzichakata taarifa binafsi za watu.

Aidha wadau wamependekeza kuwa Sheria itakayotungwa iweke vifungu vya usimamiaji na ufuatiliaji wa majukumu ya kila taasisi zinazohusiana na uchukuaji, uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi.

Wadau wamependekeza kuwa sheria iainishe aina ya makosa na adhabu itakayoweza kutolewa na chombo cha usimamizi na uwezo wa mamlaka ya chombo cha usimamizi wa taarifa binafsi.

**2. Sheria itakayotungwa izingatie mikataba ya kimataifa.**

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa izingatie Mikataba ya Kimataifa inayohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi ambayo Tanzania imeiridhia, bila ya kuathiri misingi ya Katiba. Aidha, haki za msingi zilizo ainishwa katika mikataba hiyo zilindwe na taarifa zisitumike kinyume na taratibu.

**3. Usajili wa taasisi zinazohusiana na ulinzi wa taarifa.**

Wadau wamependekeza kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vitakavyoruhusu taasisi zinazohusiana na uchukuaji, uchakataji na uhifadhi wa

taarifa binafsi kusajiliwa. Aidha imeshauriwa kuweka regista maalum la usajili wa taasisi hizo na masharti yake.

Imependezwa usajili usaidie kuainisha orodha ya taasisi za kukusanya taarifa, sifa, masharti na vigezo vitakavyotumika kwa taasisi kuweza kusajiliwa na majukumu yake ya kazi ya taasisi hizo. Wadau pia wameshauri kuwa muda wa usajili uwe kwa kipindi cha miaka mitatu kabla ya kusajiliwa kwa mara nyengine na baada ya kusajiliwa wapewe cheti cha usajili.

## 4. Tafsiri ya mambo ya msingi yanayohusiana na ulinzi wa taarifa.

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vya tafsiri ya mambo ya msingi yatakayotumika katika sheria kwa ajili ya kuondosha mgongano wa uelewa ikiwemo taarifa binafsi, upotoshaji wa maana juu ya maneno yatakayotumika, taarifa binafsi nyeti haki za watoa taarifa na wachakata taarifa, wahifadhi taarifa, idhini, mdhibiti wa taarifa mtoa taarifa, taarifa za afya n.k.

## 5. Taarifa nyeti

Wadau wamependekeza taarifa nyeti zijumuishe taarifa zinazohusiana na kabila, mtazamo wa kisiasa, imani za kidini, uanachama wa chama cha

wafanyakazi, urithi, mifumo wa bayometrik, hali ya kiafya, hali ya kijinsia, taarifa za kimawasiliano, kifamilia, uchumi, ndoa na umiliki wa mali.

Aidha, wadau wameshauri kuwa maeneo haya ya taarifa ni maeneo ya ndani sana na yanamgusa mtu mmoja mmoja, hivyo yanatakiwa yalindwe kwa gaharama kubwa kwani taarifa hizi zikitoka zinaweza kumletea athari mbaya mtoa taarifa na kupelekea kushuka kwa utu na thamani yake katika jamii.

## 6. Kuanzishwe chombo maalum cha usimamizi na udhibiti wa ulinzi wa taarifa binafsi.

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa ianzishwe chombo maalum cha usimamizi na udhibiti wa ulinzi wa taarifa binafsi. Uajiri wa watendaji watakaofanyakazi katika chombo hicho utakuwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya utumishi wa umma.

Aidha, wadau wameshauri kuwa Chombo hicho kinatakiwa kiwe huru katika kutekeleza majukumu yake. Miongoni mwa majukumu yatakayopewa chombo hicho iwe ni usimamiaji, ukusanyaji wa taarifa zote na kuziweka pahala pamoja, pamoja, usajili wa taasisi zinazohusika na uchukuaji, uhifadhi na uchakataji wa taraifa binafsi pamoja na ufuatiliaji wa taasisi zinazohusika na ukusanyaji uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi.

Wadau wameshauri kuwa muundo wa taasisi hiyo uwe kwa mujibu wa miundo ya serikali, chombo hicho kiwekewe mipaka katika kutekeleza majukumu yake

ya kazi katika ufuatiliaji (monitoring) wa kuhakikisha kuwa taasisi zote zinazokusanya, kuhifadhi na kuzichakata taarifa binafsi wanafuata sheria hiyo.

**7. Upokeaji wa malalamiko.**

Wadau wameshauri kuwa chombo kitakachoanzishwa kipewe uwezo wa kupokea malalamiko na kuweza kuyasikiliza kwa hatua za awali. Chombo hicho kijiwekee utaratibu wa kusikiliza maombi na kisifuate utaratibu wa kimahkama.

Aidha, wadau wamependekea kuwa malalamiko yatakayowasilishwa yawe kwa njia ya kujaza fomu maalum ambazo zitatayarishwa na chombo hicho. Hata hivyo chombo hicho kipewe uwezo wa kutoa adhabu kwa mujibu wa kiwango cha makosa kitakachoainishwa na sheria .

**8. Ushirikiano baina ya Tume ya Muungano na Taasisi itakayoanzishwa inayoshughulika na utunzaji wa taarifa binafsi.**

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vya kukuza mashirikiano baina ya Tume ya muungano inayoshughulikia na ulinzi wa taarifa binafsi za muungano na Tume itakayoanzishwa Zanzibar ambayo itapewa jukumu la kulinda taarifa binafsi.

Wadau wameshauri kuwa kwa vile tume hizi zitakuwa na majukumu sawa na zitafanyakazi zinazofanana ni vyema kupitia sheria itakayoanzishwa ikaweka

Kanuni au miongozo itakayotumika katika kubadilishana taarifa binafsi katika pande zote za muungano.

Aidha, wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vya utaratibu wa kimaadili kwa watendaji na Tume hizo katika kuchukua, kuhifadhi na kuchakata taarifa binafsi.

Vilevile, wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vitakavyohusiaana na kubadilishana uzoefu kati ya watendaji wa Tume ya Muungano na Tume itakayoanzishwa kuhusianana ulinzi wa taarifa binafsi, pia wadau wamependekeza kuwa kufanywe utaratibu wa mafunzo kati ya Tume mbili kwa ajili ya kujengeana uwezo wa kimfumo katika kutekeleza majukumu ya kazi zao.

## 9. Misingi ya utoaji wa tarifa binafsi

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vya masharti ambavyo vitazingatia misingi ya utoaji wa taarifa binafsi. Misingi hiyo ijikite katika haki na uwazi katika uchukuaji, uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi.

Wadau wameshauri vifungu hivyo vitasaidia sana kwa watendaji kutimiza wajibu wao wa kuchukua, kuhifadhi taarifa na kuzichakata katika hali ya haki kwa mtoaji wa tarifa pamoja na taasisi. Aidha, taarifa hizo zitachukuliwa,

kuhifadhiwa na kuchakata katika hali ya uwazi bila ya kutokea kwa manung'uniko kutoka kwa mtoa taarifa au taasisi.

**10. Usalama wa taarifa.**

Wadau wamependekeza kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vya kuhakikisha usalama wa taarifa unapatikana katika taasisi ambazo zinachukua, kuhifadhi na kuzichakata taarifa binafsi.

Wadau wameshauri kuwa vifungu hivyo vya usalama vitawahakikishia watoa tarifa kujenga imani na taasisi ambazo zinachukua, kuhifadhi na kuzichakata taarifa zao wanazitumia kwa mujibu wa sheria na utaziepusha taasisi hizo kuingia katika migogoro kwa jamii.

**11. Ukaguzi wa taasisi zinazoshughulikia na ulinzi wa taarifa binafsi.**

Wadau wamependekeza kuwa sheria itakayoanzishwa iweke vifungu vitakavyoruhusu ukaguzi kufanyika katika taasisi zote zinazohusiana na uchukuaji, uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi za watu kwa lengo la kuhakikisha matumizi sahihi ya taarifa pamoja na usalama wa taarifa binafsi.

Aidha, wadau wameshauri kuwa ukaguzi huo ufanyike katika mifumo yote inayohusiana na uchukuaji, uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi kila baada

ya muda kwa watumishi na taasisi husika jambo ambalo litafanya taasisi hizo kuwajibika.

**12. Kuwepo kwa adhabu ya kuvuja kwa taarifa binafsi kwa taasisi na mtendaji.**

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayoanzishwa, iweke vifungu vya adhabu kwa taasisi ambayo itapatikana na hatia ya kuvujisha taarifa ya mtu binafsi, adhabu hiyo iwe kwa upande wa taasisi ni kulipa faini, na kufutiwa usajili.

Aidha, wadau wamependekeza kuwa ikiwa taarifa zitavuja kwa bahati mbaya labda kutokana na mfumo kuharibika wa upokeaji wa taarifa, kwani taasisi nyingi zinatumia mifumo ya kieletroniki katika kufanyakazi zake kwa ajili ya kurahisisha ufanyaji kazi.

Hivyo Taasisi hizo zinatakiwa kumjuilisha mtoa taarifa na kuweka mazingira yatakayomsafisha mtoa taarifa kutokana na taarifa hizo kwani taarifa hizo zinaweza pia kumletea athari mbaya katika jamii.

Wadau pia wameshauri kuwa sheria itakayotungwa ifuate sheria, kanuni na miongozo ya kitumishi katika kipengele cha uvunjifu wa maadili ya kazi kwa mtendaji ambaye atavujisha taarifa.

**13. Kuwepo kwa adhabu kwa wale wote watakaodukua mfumo wa taarifa binafsi, kutumiwa kinyume na madhumuni, kubadilisha au kupotea.**

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vya makosa ya udukuzi wa taarifa pamoja na adhabu kwa wale wote watakaofanyakazi ya udukuzi wa mfumo au taarifa binafsi, kutumia kinyume na madhumuni, kubadilisha au kupotea. Adhabu hiyo iwe ya kifungo na faini kwani kosa hilo ni kosa la kijinai. Mdukuzi huyo anaweza kuzitumia vibaya taarifa hizo na kumpelekea kuharibu jina, taswira na hadhi ya ofisi jambo ambalo litapelekea watu kutokuwa na imani na ofisi hiyo.

Aidha, wadau wameshauri kuwa kwa upande wa mtoa taarifa ambaye ataathirika na udukuzi huo, ambao unaweza kuleta tafauti na migongano katika nchi na hatimae kumletea mtoa taarifa kushuka hadhi yake, kuharibu taaswira yake, kumuondolea utu wake na heshima yake katika jamii na kumfanya asiaminike tena katika jamii na kupelekea athari za kimwili na kisaikolojia; alipwe fidia kutokana na madhara yote ambayo atasababishiwa na mdukuzi.

## 14. Kulipwa kwa fidia kwa mtu ambaye taarifa zake zimevuja, kutumiwa kinyume na madhumuni, kubadilisha au kupotea.

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayoanzishwa iweke vifungu vya fidia kwa wale wote ambao wataathirika na taarifa zao kuvuja, kutumika kinyume na madhumuni au kupotea. Vifungu hivyo vielezee utaratibu wa fidia unaotakiwa ulipwe kulingana na uzito wa makosa yaliyotokea.

Kwa upande wa mtu ambaye taarifa zake zimevuja, wadau wameshauri kuwa kosa hili liwe ni kosa kubwa kwa sababu taarifa binafsi zikivuja zinaweza kusababisha athari kubwa sana katika jamii. Wadau wametoa mfano mtu mwenye ugonjwa wa kuambukiza kama vile ukimwi na mwenyewe anafanya siri ili watu wasijue, taarifa zake zinapovuja zinaweza kushusha hadhi katika jamii, kumdhalilisha na kumsababishia maumivu makubwa na msongo wa mawazo ambao anaweza hata kujidhuru kwa kujiua au kujijeruhi. Fidia yake iwe iwe kubwa ili iwe fundisho kwa wengine.

Kwa upande wa taarifa kutumika kinyume na madhumuni yaliyokusudiwa, kubadilisha au kupotea, wadau wameshauri kuwa, liwe kosa na litolewe fidia kwa mujibu wa uzito wa makosa hayo.

## 15. Kuwepo kwa mfumo wa kisheria wa ulinzi wa taarifa wakati wa uhamishaji wa taarifa binafsi.

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vitakavyolinda taarifa za mtu binafsi wakati zikihamishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine kwa ajili ya matumizi.

Vifungu hivyo viweke masharti ya kisheria ya kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinaenda katika nchi ambayo ina mfumo wa kisheria ya ulinzi wa taarifa binafsi. Aidha nchi hiyo iwe imeridhia mikataba ya kimataifa inayohusiana na ulinzi wa taarifa, iwe na Balozi wa nchi ambayo taarifa hiyo imetoka na pia kuwe na ulinzi wa jeshi la kimataifa (Interpol).

Wadau pia wameshauri kuwa taasisi inayopokea taarifa hiyo ihakikishe kuwa taarifa inatumiwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa na haiwezi kuathiri maslahi ya mtoa taarifa katika nchi ambayo taarifa hiyo imetoka. Aidha mtoa taarifa anapaswa kupewa taarifa kuhusiana na kuhamishwa kwa taarifa zake.

Wadau wameshauri kuwa kuwekwe makubaliano maalum ya mashirikiano baina ya Zanzibar na nchi ambayo taarifa ya mtu binafsi inapelekewa. Hii itasaidia kujiridhisha kuwa taarifa inayohamishwa inatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa bila ya kuathiri haki za mtoa taarifa.

**16. Kuweka ukomo wa uhifadhi wa taarifa kwa baadhi ya taarifa binafsi.**

Wadau wameshauri kuwa matumizi na uchakataji wa taarifa binafsi lazima uwekewe muda maalum katika matumizi. Kuhifadhi baadhi ya taarifa binafsi za watu kwa muda mrefu sio jambo sahihi na linaweza kupelekea mambo mbalimbali yatokee.

Wadau wameshauri kuwa kwa vile taasisi nyingi zinatumia mifumo ya kieletroniki katika kuchukua, kuhifadhi na kuzitumia taarifa hizo. Mifumo ambayo inahitaji gharama kubwa kwa ajili ya kuifanyia marekebisho na kutokana na hali za kiuchumi, taasisi nyingi zinazohusika na uchukuaji wa taarifa binafsi hazimudu gharama hizo jambo ambalo linapelekea kuendelea kukaa nazo kwa muda mrefu na kupelekea taarifa hizo kupotea, kuvuja au kuharibika pamoja na kuzuia uwezo wa taasisi kupokea taarifa nyengine kutokana na mzigo mkubwa wa taarifa ambazo hazina matumizi tena.

Kwa hivyo, wadau wamependekeza kuwa uhifadhi wa taarifa binafsi unaweza kuchukua muda mdogo tu kulingana na mahitaji ya taarifa yenyewe, baada ya kumalizika matumizi yake taarifa hizo zinaweza kufutwa isipokuwa taarifa binafsi ambazo zinaweza kutumika kwa madhumuni ya usalama wa nchi, tathmini ya kodi, uteuzi wa nafasi mbalimbali katika uongozi, taarifa za aina kama hii zinaweza kuendelea kutunzwa kwa ajili ya matumizi ya baadae.

## 17. Haki na wajibu kwa mtoa taarifa

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke kipengele kitakachoelezea haki na wajibu wa mtoa taarifa binafsi. Miongoni mwa haki za mtoa taarifa binafsi ni haki ya ridhaa ya kutoa taarifa, haki ya kupewa maelezo

ya matumizi ya taarifa, haki ya kulindwa kwa taarifa zake, haki ya kulalamika au kushitaki ikiwa taarifa zake zitatumika kinyume na madhumuni, haki ya kupata taarifa zake wakati wowote, haki ya kufahamishwa ikiwa taarifa zake zitahamishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine, haki ya kupata fidia ikiwa taarifa zake zitavujishwa, haki ya kufahamishwa ikiwa taarifa zake zimevuja kwa bahati mbaya.

Aidha, wadau wameshauri kuwa sheria itakayoanzishwa iweke vifungu vya wajibu kwa mtoa taarifa na adhabu ya kinidhamu ikiwa mtoa taarifa atashindwa kutimiza wajibu wake na kutoa taarifa za uwongo ukapelekea kuipotosha taasisi husika. Miongoni mwa wajibu wa mtoa taarifa ni kuhakikisha kuwa taarifa anayoitoa ni ya ukweli na sahihi, kufanya matumizi sahihi ya mitandao, Kutokutuma picha, video au sauti au vitu vyengine mitandaoni ambavyo vitamtambulisha mwenyewe.

## 18. Utunzaji wa siri na maadili katika ulinzi wa taarifa binafsi

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vya utunzaji wa siri na maadili kwa watendaji wanaofanyakazi za kuchukua, kuhifadhi na kuzichakata taarifa za binafsi baada ya kuzipokea kutoka kwa watoaji wa taarifa.

Aidha, wadau wamependekeza kuwa Sheria hiyo iweke kifungu cha adhabu kwa mtendaji ambaye ameshindwa kutimiza wajibu wake wa kutunza siri za mtoa taarifa na kwenda kinyume na maadili yake ya kazi kwani endapo siri

hizo zikavuja na kuwafikia watu wengine wasiohusika inaweza kuhatarisha usalama wa mtu , taifa na jamii kwa ujumla pia itapelekea kuleta athari kwa Taasisi za Serikali katika ushindani wa biashara.

Hivyo, wadau wameshauri kuwa ili watendaji wawe na maadili ya utumishi wa umma pamoja na kutunza siri za Serikali wanatakiwa walishwe kiapo cha usiri na maadili. Hii itajenga imani kwa watoa taarifa na kupelekea kuaminiwa kwa taasisi inayohusika na uchukuaji uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi na itasaidia sana kukuza uwekezaji katika kampuni za nje kuwa na imani na uwepo wa usiri wa taarifa.

## 19. Uwajibikaji wa taasisi zinazohusiana na uchukuaji uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi

Wadau wameshauri kuwa watendaji wanaohusika na uchukuaji,uhifadhi na uchakataji wa taarifa wanatakiwa wawajibike ipasavyo katika kufanya kazi zao ili ufanisi wa kazi uweze kupatikana.

Aidha, wadau wameshauri kuwa sheria iweke vifungu vya makosa ya kwa taasisi zinazohusika na uchukuaji, uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi. makosa hayo yakiwemo, kufutiwa usajili, kulipishwa faini, kunyanganywa hati ya usajili.

## 20. Kutoa taarifa bila ya ridhaa ya mwenye taarifa

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vitakavyoruhusu kutolewa kwa taarifa binafsi bila ya mtoa taarifa kujua. Aidha, taarifa hizo zitolewe sio kwa lengo la kumhujumu mtu au kukosa uthibitisho au kuwe na kibali cha Mahkama.

Wadau wamependekeza mazingira yenyewe yawe ni kwa ajili ya maslahi ya umma, usalama wa nchi, Ulinzi na usalama wa taifa, kuzuia uhalifu usiweze kutokea, ugunduzi wa kitu au zinaweza kusaidia kufanikisha upelelezi wa jinai au zinahitajika kwa ajili ya kufanyika kwa tathmini ya kodi na iwapo zitahitajika kwa ajili ya uteuzi wa maofisa wa kimahkama au nafasi nyengine za uongozi.

## 21. Kuwekwe utaratibu wa adhabu katika uvujaji, upotevu, uuzaji na ubadilishaji wa taarifa kwa kampuni.

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vya makosa kwa uvujaji wa taarifa binafsi kwa kampuni ambazo zinahusika katika uchukuaji, utumiaji na uchakataji wa taarifa binafsi, aidha sheria iweke makosa na adhabu ya upotevu wa taarifa kwa kampuni hizo.

Wadau wamependekeza kuwa Sheria hiyo iweke vifungu vya makosa kwa makampuni yenye ubia ikiwa watabadilishana taarifa binafsi kutoka kampuni moja kwenda kampuni nyengine bila ya uhalali na bila ya mtoa taarifa kujua. Makosa hayo yawekewe adhabu kwa makampuni hayo kwani mtoa taarifa atakapojua kuwa kuwa taarifa zake zimepelekewa katika kampuni nyengine

sio ile ambayo mtoa taarifa ametoa taarifa zake zinaweza kumletea athari ya kimwili na kisaikolojia.

Vilevile wadau wamependekeza sheria iweke makosa ya kuuziana taarifa kutoka kampuni moja kwenda kampuni nyengine. Makosa hayo yawekewe adhabu kwani ikiwa kampuni hizo zitauziana taarifa na mtoa taarifa akijua kuwa taarifa zake zimeuzwa kunaweza kumletea matatizo makubwa ya kisaikolojia.

## 22. Kuweka utaratibu wa kudhibiti mitandao ya kijamii katika ulinzi wa taarifa.

Wadau wameshauri kuwa sheria itakayotungwa iweke vifungu vya udhibiti wa mitandao ya kijamii katika ulinzi wa taarifa. Aidha wadau wameshauri chombo kitakachoanzishwa kishirikane na taasisi zinazoshughulikia na mambo ya mifumo katika kuweka udhibiti wa kimtandao katika ulinzi wa taarifa binafsi.

Udhibiti huo ujikite katika upatikanaji wa taarifa binafsi na utumaji wa taarifa kupitia mitandao ya kijamii kama vile Facebook, u- tube, twiter, whats App na mitandao mengine. Aidha wadau wameshauri kuwa kutumike njia maalum ambazo zitakazomfanya mtu ambaye hahusiki na uchakataji wa taarifa kutoweza kuingia katika mfumo kwa ajili ya kuchukua taarifa binafsi au kuzitumia kwa njia anayoitaka mwenyewe.

Katika kuhakikisha utaratibu wa udhibiti unafanikiwa kwa taasisi zinazohusika na uchukuaji , utumiaji na uchakataji wa taarifa wadau wameshauri kuwa taasisi hizo ziwe na mifumo inayosomana ambayo itaweza kumuona na kumdhibiti mtu wa tatu ambaye ni mgeni katika mifumo asiweze kuchukua na kuzitumia taarifa binafsi za mtu mwengine.

**4.5. Maoni ya Kitendaji.**

**1. Elimu kwa watendaji**

Wadau wameshauri elimu itolewe kwa watendaji wanaohusika na uchukuaji wa taarifa binafsi ili elimu hiyo izidi kuwaongezea uwezo na maarifa katika kufanikisha majukumu yao ya kazi.

Wadau wamependekeza kuwa elimu hiyo ijikite sana katika nyanja nzima ya maadili, uwajibikaji, utunzaji wa siri, utumiaji wa vifaa vya kieletroniki ambavyo vinatumika katika uchukuaji , uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi, umuhimu wa kiapo cha utunzaji siri, athari za kuvujisha, kupoteza, kutotumia taarifa kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kuwa tayari kupokea na kujifunza kutumia teknolojia mpya mara tu inapovumbuliwa duniani. Kupitia elimu hiyo watatoa huduma kwa usawa, uhakika, na watafanyakazi zao kwa ufanisi.

**2. Elimu kwa watoaji wa taarifa binafsi**

Wadau wameshauri kuwa watoaji wa taarifa wanatakiwa wapewe elimu ili waweze kuelewa faida na hasara za kutoa taarifa zao binafsi na namna ya taarifa zao zinavyolindwa na kuhifadhiwa, kuhamishwa kutoka nchi moja kwenda nchi nyengine pamoja na haki na wajibu wao katika utoaji wa taarifa binafsi.

Aidha, wadau wamependekeza kua utoaji huo wa elimu uwekwe kisheria ambapo utazilazimisha taasisi kutoa elimu hiyo pamoja na kuwekewa adhabu kwa taasisi iwapo taasisi hizo zitashindwa kufanya wajibu huo wa kisheria..

**3. Kuwe na teknolojia ya hali ya juu itakayotumika kulinda taarifa binafsi**

Wadau wamependekeza kuwa mashirika ambayo yanachukua, kutumia na kuchakata taarifa binafsi wawe na utaalam wa hali ya juu katika kutilia mkazo katika udhibiti wa taarifa ambazo zinatumia mifumo inayoendeshwa na teknolojia katika kulinda taarifa binafsi.

Wadau wameshauri kuwa Taasisi na mashirika yanatakiwa yaende na wakati na wawe mbele zaidi kiteknolojia katika kutumia mifumo ya teknolojia mpya kila inapovumbuliwa duniani. Aidha wadau wamependekeza taasisi na mashirika hayo mara kwa mara yawe yanapata mafunzo kwa ajili ya kuongeza utaalamu ambapo utawasaidia katika kutafuta njia za kujilinda dhidi ya wadukuzi wa mitandao ambao wanaoiba taarifa binafsi kupitia teknolojia.

### 4. Kubadilishana uzoefu na taasisi zinazofanyakazi za uchukuaji wa taarifa binafsi

Wadau wameshauri kuwa taasisi za Zanzibar zinazofanyakazi ya kuchukua, kutumia na kuchakata taarifa binafsi zinatakiwa ziwe na utamaduni wa kufanya ziara za kujifunza katika taasisi mbalimbali ambazo zina majukumu sawa na taasisi za Zanzibar kwa lengo la kujifunza na kupata uzoefu kupitia taasisi hizo .

Ziara hizo zitasaidia sana katika utendaji wao wa kazi kwani watapata kusoma, kubadilishana mawazo na kujifunza vitu vipya vizuri ambavyo hawajawahi kuvifanya.

Aidha, ziara hizo za kimasomo zitasaidia sana taasisi kwenda na wakati kwani teknolojia kila siku inakuwa, inabadilika na mambo mengi sana mapya yanabuniwa na kuingizwa katika mitandao ambayo kwa kiasi kikubwa yanaathiri ulinzi wa taarifa. Hivyo uzoefu huo watakaoupata utawasaidia sana katika utekelezaji mzima wa majukumu yao ya kazi.

## SURA YA TANO

## 5.0 MIKATABA YA KIMATAIFA NA UZOEFU WA NCHI MBALIMBALI

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inazungumzia Mikataba ya Kimataifa na Kikanda uzoefu wa nchi mbalimbali ambazo Tume imepitia kwa lengo la kuangalia uzoefu na taratibu za kisheria zilizowekwa juu ya ulinzi wa taarifa binafsi.

## 5.2 Mikataba ya Kimataifa na Kikanda.

### 5.2.1 Azimio la Kimataifa juu ya Haki za Binadam la Mwaka 1948

Umoja wa Mataifa ulitoa azimio la Kimataifa juu ya Haki za Binadamu (UDHR) tarehe 10 Disemba, 1948 likiwa ni miongoni mwa maazimio ya kwanza kutolewa na Umoja wa Mataifa. [195]

Azimio hilo la Kimataifa limeeleza kuwa hakuna mtu atakayeingiliwa faragha yake, familia, nyumba au mawasiliano yake, wala kushambuliwa kwa heshima na sifa yake. Kila mtu ana haki ya kulindwa na sheria dhidi ya kuingiliwa na mashambulizi hayo.[196]

### 5.2.2 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966.

Mnamo tarehe 16 Disemba, 1966 Umoja wa Mataifa katika Mkutano wake Mkuu ulipitisha makubaliano juu ya uwepo wa haki za Kiraia na Kisiasa, kuzitaka Nchi wananchama kuheshimu haki za kiraia na za kisiasa.

Aidha, mkataba huu umeweka haki ya kulindwa kwa faragha za watu na kuweleza kuwa hakuna mtu atakayeingiliwa kiholela au kinyume cha sheria na faragha yake, familia, nyumba au mawasiliano yake, wala mashambulizi yasiyo

[195] Azimio la Kimataifa Juu ya Haki za Binaadam la mwaka 1948.
[196] Ibid Kifungu cha 12.

halali kwa heshima na sifa yake, kila mtu ana haki ya kulindwa na sheria dhidi ya kuingiliwa na mashambulizi hayo.[197]

### 5.2.3 Mkataba wa Ulinzi wa Watu Binafsi kuhusu Uchakataji wa Taarifa binafsi Nam 108 wa 1981.

Mkataba huu ulisainiwa mnamo tarehe 28 Januari 1981 na ilikuwa chombo cha kwanza cha kisheria cha kimataifa katika eneo la ulinzi wa taarifa. Chini ya Mkataba huu, Nchi wanachama wanatakiwa kuchukua hatua muhimu katika sheria zao za ndani ili kuhakikisha heshima katika eneo la uchakataji wa taarifa binafsi.[198]

Hata hivyo Mkataba huu umezitaka Nchi wanachama kuzingatia mambo yafuatayo;

**(a) Ubora wa Taarifa.**

Mkataba unataka taarifa zinazokusanywa  na kuhifadhiwa, kwa njia ya haki na kisheria, kuhifadhiwa kwa madhumuni maalum na ya halali. Pia Mkataba huu unataka kuwa taarifa binafsi zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.[199]

**(b) Usalama wa taarifa.**

Mkataba umezitaka Sheria za nchi wanachama za kuhakikisha kuwa taarifa binafsi zinasimamiwa na kulindwa kwa usalama wa taarifa hizo, ikiwemo mafaili ya kielektroniki dhidi ya uharibifu wa makusudi au bahati mbaya au bila

---

[197] Ibid, kifungu 17(1)na (2)
[198] Convention 108 and Protocols - Data Protection (coe.int)
[199] Mkataba wa Ulinzi wa taarifa binafsi na uchakataji wa taarifa 108 wa 1981. Kifungu cha 5(a-e)

ya kufuatwa kwa sheria. Mkataba umezungumzia upotezaji wa bahati mbaya wa taarifa hizo au kutolewa kwa taarifa hizo bila ya ruhusa au kufanya mabadiliko ya taarifa hizo ambayo hayajaruhusiwa au usambazaji.[200]

**(c) Makundi Maalum ya Taarifa.**

Makundi ya taarifa yalioelezwa ni taarifa ambazo zinazofichua asili ya rangi ya mtoa taarifa, maoni au itikadi za kisiasa au imani za kidini, pamoja na taarifa binafsi zinazohusiana na masuala ya magonjwa (afya) ya mtoa taarifa au masuala ya jinsia.[201]

**(d) Mfumo wa Usafirishaji wa Taarifa Binafsi Nje ya Mipaka ya Nchi.**

Mkataba huu pia umetaka Sheria za ndani kutoa ulinzi madhubuti na unaofaa kwa taarifa binafsi ambazo zinavuka mipaka kutoka nchi moja na kwenda nchi nyengine, kwa kuzingatia kiwango cha ubora wa ulinzi wa taarifa katika nchi hizo kabla ya kuzituma.[202]

### 5.2.4 Itifaki ya Ziada ya Mkataba wa Ulinzi wa Taarifa binafsi Kuhusiana na Uhifadhi wa Moja kwa Moja wa Taarifa Binafsi Nam. 181 wa Mwaka 2001.

Nyongeza hii ya Mkataba imekuja kuweka kiwango kipya cha muhimu cha ulinzi wa taarifa, Mkataba wa 108 umeweza kuwakilisha kiwango cha kimataifa

[200] Ibid, kifungu 7.
[201] Ibid, kifungu 6.
[202] Ibid, kifungu 12

katika ulinzi wa taarifa binafsi.[203] Mkataba huu ulizingatia mambo mengi ikiwemo masuala ya kuwa na udhibiti wa taarifa binafsi na kuwa na chombo ambacho kitakuwa na jukumu la kusimamia ulinzi wa taarifa binafsi.[204] Miongoni mwa mambo muhimu ambayo ambayo yametiliwa mkazo katika mkataba huo ni;

**(a) Mamlaka za Usimamizi.**

Nchi mwanachama inatakiwa kuwa na mamlaka moja au zaidi ya kusimamia na kuhakikisha utekelezwaji wa sheria pamoja na uchukuaji wa hatua katika sheria na kanuni zake. Aidha, mamlaka zitakazoanzishwa zinatakiwa ziwe na uwezo wa kufanya uchunguzi na kuingilia kati mambo ya uvunjifu wa uhifadhi wa taarifa binafsi. Vile vile, Mamlaka hizo ziwe na nguvu ya kufungua kesi au kutoa onyo kwa mamlaka ambazo zinakwenda kinyume na sheria.[205]

**(b) Usafirishaji wa Taarifa ya Binafsi kwa Mpokeaji Ambaye sio Mwanachama katika Mkataba.**

Katika mkataba nchi wanachama zimetakiwa kuweka mazingira ya kusafirisha taarifa binafsi kwa mpokeaji ambaye yupo nchini au katika Taasisi au Shirika ambalo sio mwanachama wa Mkataba, ili kuhakikisha kiwango cha kutosha cha ulinzi wa taarifa na usalama katika uhamishaji wa taarifa binafsi iliyokusudiwa. Aidha usafirishaji huo unazingatia sheria za ndani kwa ajili ya maslahi ya nchi husika.[206]

---

[203] Convention 108 + And the future data protection global standard - Data Protection (coe.int)
[204] Mkataba wa nyongeza wa ulinzi wa taarifa binafsi na uchakataji wa taarifa.181 kifungu cha 1
[205] Ibid, kifungu cha 1
[206] Ibid, kifungu 2

### 5.2.5 Azimio la Afrika kuhusu Kanuni za Uhuru wa Kujieleza 2019.

Azimio la Kanuni za Uhuru wa Kujieleza na Upatikanaji wa Taarifa Barani Afrika, lilipitishwa na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu katika kikao chake cha 65 cha kawaida kilichofanyika kuanzia tarehe 21 Oktoba hadi 10 Novemba 2019 Mjini Banjul, Gambia.[207]

Azimio hili limezingatia masuala ya ulinzi wa taarifa binafsi licha ya kuwa limetoa uhuru wa kupata habari na taarifa lakini kwa upande wa taarifa binafsi zinahitaji kulindwa na kusimamiwa kwa mujibu wa sheria.[208] Aidha, Azimio limewataka nchi wanachama kuwa na sheria ambayo itatoa haki ya kupata taarifa katika mitandao na kuhakikisha usalama wa taarifa za watumiaji binafsi zinakuwa katika hali ya usalama.[209]

### 5.2.6 Mkataba wa Nchi za Afika wa Ulinzi wa Mitandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa mwaka 2000.

Mkataba huu uliridhiwa mnamo mwaka 2000 na Nchi Wanachama za Umoja wa Afrika (AU). Lengo la Mkataba huu ni kuwa na mfumo wa sheria ambao utakuwa unatumika katika Nchi Wanachama za Umoja wa Afrika na kufikia malengo ya kuzuia uhalifu wa kimtandao pamoja na ulinzi wa taarifa binafsi. Kwa lengo la kufikia misingi ya utawala bora na misingi ya haki za binaadamu

[207] Declaration of Principles on Freedom of Expression 2019 | African Commission on Human and Peoples' Rights (au.int)

[208] Ibid, kifungu cha 40.

[209] Ibid, kifungu cha 40(1)

ikiwemo haki ya kuwa na faragha kwa kila mtu.[210] Miongoni mwa mambo muhimu ambayo yamesisitizwa katika Mkataba ni;

**(a) Kulindwa kwa Taarifa Binafsi**.

Uwepo mfumo wa sheria ambao utakuwa na nguvu kwa lengo la kulinda haki ya umma, kupeleka haki za msingi za faragha na uhuru wa kulinda taarifa binafsi. Nchi wanachama zimetakiwa kuhakikisha zinaondoa aina zote za ukandamizaji wa uhuru wa farahgha na ulinzi wa taarifa binafsi sambamba na kuhakikisha kuwa kunakuwa na utaratibu mzuri wa ukusanyaji na usambazaji wa taarifa binafsi pamoja na kuhakikisha kuwa haki za watu zinaheshimiwa.[211]

**(b) Usimamizi wa Taarifa Binafsi**.

Mkataba unazitaka nchi wanachama kuwa na Sheria ambazo zitaweza kusimamia uchukuaji wa hatua za ulinzi wa taarifa binafsi katika masuala ya ukusanyaji wa taarifa binafsi, uchakataji wa taarifa binafsi, usafirishaji wa taarifa kwa Serekali, Jamii, matumizi ya umma au kampuni binafsi.

Aidha, mkataba huu hauzingatii masuala ya Usalama wa Umma, Ulinzi, Utafiti, uendeshaji wa kesi za jinai, usalama wa Nchi isipokuwa iwe imetafsiriwa katika sheria maalum.[212]

---

[210] Mkataba wa Umoja wa Nchi za Africa wa Ulinzi wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2000.
[211] Ibid, kifungu cha 8 (1) na (2).
[212] Ibid, kifungu cha 9(1) na (2)

### (c) Kuanzishwa kwa Taasisi ya Usimamiaji wa Taarifa Binafsi.

Mkataba huu pia umezitaka nchi wanachama katika sheria kulinda taarifa binafsi, na kuanzisha chombo chenye mamlaka kwa lengo la kudhibiti taarifa binafsi na chombo hicho kinahitajika kuwa kinajitegemea na kifanye kazi kwa mujibu wa Sheria, pamoja na kutoingiliwa katika utendaji wake kazi.[213]

## 5.2.7 Mkataba wa Kufananisha Sheria za Kulinda Taarifa kwa Nchi za Jumuia ya Maendeleo za Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) wa mwaka 2008.

### (a) Mamlaka ya Ulinzi wa Taarifa.

Mkataba umezitaka nchi wanachama kuwa na chombo huru cha kusimamia ulinzi wa taarifa ambacho kitakuwa kinajuulikana kama Mamlaka ya Ulinzi wa Taarifa**.** Lengo la Mamlaka hiyo itakuwa na usimamizi na udhibiti wa taarifa binafsi pamoja na kusimamia Sheria na haki husika za faragha katika eneo la kitaifa. Aidha, mamlaka hiyo itakuwa na jukumu la kutoa maoni katika njia bora za kulinda taarifa ama kwa hiari ya Mamlaka au kwa ombi la Serikali, Bunge, juu ya jambo lolote ambalo linahusiana na kanuni na matumizi ya msingi wa haki ya faragha.[214]

### (b) Ubora wa Taarifa.

Mkataba huu unazitaka nchi wanachama katika sheria, kuhakikisha kuwa sheria zinakuwa  na uwezo mkubwa wa kudhibiti taarifa, kuweza kumchagua

[213] Ibid, kifungu cha 11.
[214] Mkataba wa Jumuia ya SADIC wa mwaka 2008 juu ya Ulinganishi wa Sheria za Kulinda Taarifa, Sehemu ya Tatu.

mdhibiti wa taarifa ambaye atahakikisha kuwa taarifa binafsi iliyochakatwa inakuwa ni ya kutosha na inayofaa kuhusiana na madhumuni ambayo imekusanywa au kuchakatwa.[215]

### (c) Kanuni za Uchakataji wa Taarifa Binafsi.

Mkataba umezitaka nchi kuweka mazingira mazuri kwa sheria na kanuni kwa mdhibiti wa taarifa ili aweze kuhakikisha kuwa anafuata taratibu zilizopo wakati wa kuhifadhi taarifa binafsi na kuona umuhimu na kutambua kuwa taarifa binafsi inashughulikiwa kwa haki na sheria.

Kwa upande wa mkusanyaji wa taarifa binafsi anatakiwa kuhakikisha taarifa inakusanywa kwa misingi ya haki na kuweka wazi madhumuni ya taarifa hizo sambamba na kuzingatia haki za mtoa taarifa.[216]

### (d) Majukumu ya Mdhibiti wa Taarifa na Mchakataji Taaria.

Mkataba huu umezingatia masuala ya kuwapa majukumu mdhibiti na mchakataji wa taarifa, hivyo nchi wanachama zina wajibu wa kuwapa kisheria watunzaji wa taarifa sambamba na wachakataji wa taarifa jukumu la kumpa taarifa yule mtu ambaye taarifa zake zinachukuliwa, kwa lengo la kufahamu nini dhamira ya kuchuliwa kwa taarifa zake, matumizi ya taarifa zake na awe huru kutoa taarifa.

---

[215] Ibid, Sehemu ya Nne, kifungu cha 11.
[216] Ibid, Sehemu ya Tano kifungu cha 12 na 13.

Aidha, mkataba umeeleza wajibu wa kuwapa taarifa Mamlaka ya Udhibiti wa Taarifa kwa ukusanyaji wa taarifa binafsi ambazo wanazifanya kama ni ukusanyaji au utunzaji wa taarifa hizo ili ziwepo katika mamlaka husika.[217]

**(e) Haki za Mtoa Taarifa.**

Mkataba umezitaka nchi wanachama katika sheria husika za nchi kuhakikisha kuwa inaweka haki za msingi kwa mtoa taarifa kwa jambo lolote ambalo linahusiana na utambulisho wake kupata bila ya maelezo na malipo.

Aidha, taarifa zinatakiwa zihifadhiwe kwa mfumo wa haki na usawa kwa mujibu wa sheria. Haki ya kuridhia imeelezwa na kuhusishwa na haki ya kujua kuwa taarifa zake zitatumika kwa muda gani na ukomo wa kuweza kuzipata taarifa hizo.[218]

### 5.2.8 Mkakati wa Usalama wa Mtandao na Uhalifu wa Mtandao wa Jumuiya ya maendeleo ya nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS.)

Lengo la kuu la Mkakati huu ni kuanzisha mfumo wa kimkakati wa jamii utakaozingatiwa na nchi wanachama katika mikakati yao ya kitaifa na kutekelezwa katika mipango ya utekelezaji juu ya usalama wa mtandao na mapambano dhidi ya uhalifu wa mtandao kabla ya mwisho wa mwaka 2022.[219]

**(a) Kuimarisha Usalama wa Mitandao.**

---

[217] Ibid, Sehemu ya Sita kifungu cha 21.
[218] Ibid, Sehemu ya Saba kifungu cha 31 na 32.
[219] Ecowas Regional Cybersecurity and Cybercrime strategy) kifungu cha 2A.

Katika kuimarisha usalama mtandao na taarifa, kila nchi mwanachama wa ECOWAS itakuwa na jukumu la kuanzisha Mamlaka ambayo itakuwa na uwezo wa kusimamia usalama wa kimtandao kwa niaba ya Serikali na kuwa na majukumu ya kuhakikisha inasimamia usalama wa kimtandao katika Nchi za Afrika Magharibi. Aidha, mamlaka hiyo itakuwa na jukumu la kusimamia masuala ya usalama wa kimtandao na kusimamia sheria na kanuni za nchi husika.[220]

(b) **Kuendeleza msingi wa usalama wa jumla**.

Mkakati huu umezitaka kila nchi mwanachama kuendeleza msingi mkuu wa usalama unaoweka mahitaji ya chini ya usalama wa habari na kuweka utaratibu wa kisheria ambao utasimamia mihimili inayofanyia kazi mambo hayo.[221]

### 5.2.9 Sheria ya Nyongeza Juu ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Nchi Wanachama wa Jumuia ya Maendelea ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) 2010.

Katika kikao cha Thelathini na Saba (37) cha Wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendelea ya Nchi za Afika Magharibi kilichofanyika Abuja Nchini Nigeria, Wakuu hao waliridhia kupitisha makubaliano ya ziada katika ulinzi wa Taarifa binafsi.[222] Miongoni mwa mambo ambayo yameridhiwa katika makubaliano hayo ni;

---

[220] Ibid, kifungu cha iv

[221] Ibid, kifungu cha 2.6.

[222] Sheria ya Nyongeza ya Ulinzi wa Taarifa Binafsa kwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo kwa Nchi za Afirika Magharibi (ECOWAS).

### (a) Uhifadhi wa Taarifa Binafsi kwa Ajili ya Matumizi ya Umma.

Uhifadhi wa Taarifa Binafsi ambao unaweza kufanywa kwa ajili ya matumizi maslahi ya umma unaweza kufanywa kwa niaba ya Serikali, mamlaka Serikali za Mitaa, chombo chochote kilichojumuishwa chini ya sheria. Miongoni mwa mambo ambayo yataruhusiwa kwa ajili ya umma ni usalama wa taifa, masuala ya ulinzi, sensa, usimamizi wa mishahara, pensheni, kodi na majukumu mengineyo.[223]

### (b) Taratibu za Maombi ya Taarifa na Idhini.

Sheria imeweka utaratibu mzuri ambao unatakiwa kuzingatiwa pamoja na hatua za kupata idhini kwa watoa taarifa. Mhifadhi wa taarifa anatakiwa kutoa utambulisho na anuwani yake kwa mtoa taarifa, kueleza lengo la ukusanyaji wa taarifa, mtu au taasisi ambayo anatarajia kushirikiana nayo katika ulinzi wa taarifa hizo, muda ambao atatumia au kuhifadhi taarifa hizo, ulinzi na usalama wa taarifa hizo, pia kueleza mtu au taasisi ambazo zikihitaji taarifa hizo inaweza kupatiwa. [224]

### (c) Kuanzishwa Chombo cha Usimamizi wa Taarifa Binafsi.

[223] Ibid, kifungu cha 6
[224] Ibid, kifungu cha 7

Kila nchi mwanachama aliyeridhia makubaliano haya anapaswa kuanzisha chombo ambacho kitakuwa na jukumu la kusimamia na kuhakikisha kuwa taarifa binafsi zinakuwa salama.[225]

### (d) Kinga kwa Watendaji wa Mamlaka.

Makubaliano haya yamewataka nchi wanachama kuwawekea kinga watumishi na watendaji wa mamlaka ili wawe huru katika kutekeleza majukumu yao kulingana na maelekezo ya Sheria ya Nchi husika.[226] Hali hii itasaidia watumishi hao kufanya kazi kwa uhuru na kuweza kukamilisha majukumu yao katika ufanisi unaokubalika.

### (e) Usiri wa Kitaalamu na Kanuni.

Mkataba umewataka nchi wanachama kuwa na utaratibu maalum wa kuweka katika sheria ambao utahusiana na masuala ya usiri pamoja na kanuni za uendeshaji wa ukusanyaji wa taarifa binafsi, hali ambayo itahakikisha kuwa taarifa hizo zinalindwa na kuwa salama kutokana na usiri wa watendaji na kufuatwa kwa kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.[227]

### (f) Haki ya Kurekebishwa na Kuharibu.

Ikiwa Taarifa Binafsi ambayo imekusanywa kwa mtoa taarifa na akatoa taarifa ambayo haijakamilika au isiyo sahihi, au taarifa ambayo ina mashaka au

[225] Ibid, kifungu cha 10
[226] Ibid, kifungu cha 17
[227] Ibid, kifungu cha 18

iliyopitwa na wakati au marufuku; mchambuzi au muhifadhi, atakuwa na haki ya kumuomba mdhibiti wa taarifa kuwa na taarifa kama hizo kuweza kuzirekebisha, kuziongeza, au kuharibiwa, kama inavyoona inafaa.[228]

### 5.2.10 Kanuni za Maadil Juu ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi za Wafanyakazi 1997.

Katika ulinzi wa Taarifa Binafsi Shirika la kimataifa la Marekani limeona kuwa kunahaja ya wafanyakazi wa taasisi mbali mbali kuwawekea taratibu za kimaadili ambazo wanatakiwa kuzifuata wakati wa kukusanya taarifa binafsi, pamoja na kuhakikisha usalama wa taarifa hizo.[229]

#### (a) Misingi ya Ulinzi wa Taarifa.

Kanuni imeweka misingi ya ulinzi wa taarifa ambayo ni pamoja na kukusanya na kudhibiti taarifa kwa njia ya haki na usawa na kwasababu maalum ambayo itasababisha kukusanya taarifa za wafanyakazi, taarifa hizo zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.[230]

#### (b) Ukusanyaji wa Taarifa za Wafanyakazi.

[228] Ibid, kifungu cha 41
[229] Mkataba wa kimataifa wa ulinzi wa Taarifa binafsi za wafanyakazi wa 1997.
[230] Ibid kifungu cha 5.

Kanuni zimeelekeza kuwa taarifa binafsi za wafanyakazi zikusanywe kwa wafanyakazi wenyewe na ikiwa kuna haja ya kukusanywa mtu wa tatu muajiri atalazimika kumpa taarifa ya undani mfanyakazi juu hatua anayo chukuwa.[231]

### (c) Usalama wa Taarifa Binafsi.

Licha ya kuwa kanuni hizi zimeruhusu ukusanyaji wa taarifa binafsi lakini zinamtaka muajiri ahakikishe usalama wa taarifa za wafanyakazi pale ambapo atakuwa anazidhibiti, na kuhakikisha kuwa taarifa hizo hazipotezwi, haziharibiwi, wala kutolewa kinyume na sheria.[232]

### (d) **Uhifadhi wa Taarifa Binafsi.**

Kanuni hizi zimezungumzia suala la uhifadhi wa taarifa binafsi kwa muda maalum, na taarifa ambazo zinahusiana na masuala ya kiafya taarifa hizo zitahifadhiwa ikiwa kuna sababu maalum kwa maelekezo ya kiafya.[233]

## 5.3 UZOEFU WA NCHI NYENGINE.

### 5.3.1 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Kenya Nam. 24 ya Mwaka 2019.

[231] Ibid kifungu cha 6.
[232] Ibid kifungu cha 7
[233] Ibid, kifungu cha 8

Kenya imetunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Nam.24 ya Mwaka 2019 kwa lengo la kutekeleza masharti ya Katiba katika masuala ya usiri pamoja na udhibiti wa uchakataji wa taarifa binafsi.

### (a) Kuanzishwa kwa Afisi ya Uhifadhi wa Taarifa.

Sheria imeanzisha Afisi ya Kamishna wa ulinzi wa taarifa, ambayo itakuwa inajitegemea, [234] inapewa jukumu la kufanya ukaguzi wa vyombo vya umma na binafsi kwa na kutathmini ulinzi wa taarifa binafsi pamoja na usajili wa wadhibiti wa taarifa.[235]

### (b) Wajibu ya Usiri.

Sheria imekataza kutoa taarifa yoyote ile ambayo inahusiana na mtu binafsi isipokuwa kwa hitaji la kisheria. Vile vile, ni kosa kwa mtumishi kutoa taarifa binafsi ya mtoa taarifa yeyote bila ya idhini ya Afisi au matakwa ya kisheria.[236]

### (c) Usajili wa Wadhibiti wa Taarifa na Wakusanyaji wa Taarifa.

Kwa mujibu wa Sheria hii mtu yeyote haruhusiwi kufanya shughuli ya kukusanya, kudhibiti au kuchambua taarifa isipokuwa awe amesajiliwa na Kamishna wa Taarifa.[237]

[234] Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Nam.24 ya 2019, kifungu cha 4
[235] Ibid, kifungu cha 8 (b)-(e)
[236] Ibid, kifungu cha 16.
[237] Ibid Kifungu cha 18 .

Licha ya kuwa kuna usajili wa wakusanyaji na wahifadhi wa taarifa, Kamishna anaweza kukataa maombi ya mkusanyaji wa taarifa au mchakataji pale ambapo atajiridhisha kuwa ameshindwa kukamilisha vigezo vya kisheria.[238]

### (d) Misingi ya Ulinzi wa Taarifa.

Sheria hii pia imeweka misingi ya ulinzi wa taarifa na kila mdhibiti wa taarifa au mchakataji wa taarifa atahakikisha anapofanya kazi yake ya kuhifadhi au kuchakata taarifa binafsi, anasimamia misingi ya haki ya faragha kwa lengo la kuhakikisha usalama wa taarifa unafanyika kwa mujibu wa sheria.[239]

Mkusanyaji wa taarifa binafsi anatakiwa kuzingatia misingi ya haki na uwazi kuhusiana na ukusanyaji wa taarifa kwa kuhakikisha kuwa taarifa anayokusanya ndiyo inayohitajika, inayofaa kulingana na madhumuni ya ukusanyaji wa taarifa husika.[240]

### (e) **Wajibu wa Kutoa Taarifa**.

Sheria imeweka wajibu kwa Mdhibiti au mkusanyaji wa taarifa kabla ya kukusanya taarifa binafsi, kumjuulisha mtoa taarifa juu ya sababu na malengo ya uchukuaji wa taarifa hizo binafsi. Na iwapo taarifa hizo zitahamishwa basi mdhibiti au mkusanyaji wa taarifa anatakiwa kumpatia taarifa mtoa taarifa juu ya uhamishwaji wa taarifa hizo na kumhakikishia usalama wa taarifa zake

[238] Ibid kifungu cha 19.
[239] Ibid kifungu cha 25( a) na (b)
[240] Ibid Kifungu cha 25(c) -(e)

pamoja na madhara yanayoweza kutokea iwapo kutatokea ukiukwaji wa taratibu husika.[241]

**(f) Ukomo wa uhifadhi wa Taarifa binafsi.**

Sheria hii imezungumzia suala la muda wa udhibiti wa taarifa, mdhibiti au mchakataji wa taarifa anaweza kuhifadhi taarifa binafsi kwa muda mrefu iwapo taarifa hizo zitakuwa ni muhimu ili kukidhi jambo ambalo limekusudiwa.

Aidha, kwa upande wa jambo ambalo sio la muda mrefu basi taarifa hizo zifutwe mapema kadri inavyowezekana, isipokuwa matumizi ya historia, takwimu n,k.[242]

**(g) Fidia kwa Muathirika wa Taarifa.**

Sheria imemuangalia mtu anayepata madhara kwa sababu ya kuvunjwa kwa masharti ya Sheria hii, ikiwa madhara hayo ni kupoteza utu wake, heshima yake hata vitu vya thamani ana haki ya kulipwa fidia kwa uharibifu huo kutoka kwa Mdhibiti wa Taarifa.[243]

### 5.3.2 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Afrika ya Kusini Nam. 4 ya 2013.

[241] Ibid Kifungu cha 29(a)-(e)
[242] Ibid Kifungu cha 39(1)(a)na (b)
[243] Ibid kifungu cha 39(1)(c) na (d)

Sheria imetungwa kwa madhumuni ya kulinda au kudhibiti Haki ya msingi ya binadamu ambayo ni haki ya kuwa na faragha ya taarifa binafsi na kuwapa watu fidia zao kutokana uvunjifu wa haki ya faragha.[244]

### (a) Taarifa Binafsi Kutoka Nchi Moja Kwenda Nchi Nyengine.

Kwa mujibu wa Sheria, Mdhibiti au mkusanyaji wa taarifa haruhusiwi kutoa taarifa kwa mtu wa tatu au nje ya nchi isipokuwa mtu huyo awe anatambulika na sheria au kuna mkataba ambao unakubalika kwa mujibu wa sheria kwa ridhaa ya mtoa taarifa.[245]

### (b) Ruhusa kwa Taarifa Binafsi ambazo ni Nyeti.

Sheria imekataza kutoa taarifa ambazo zinahusiana na maradhi na masuala ambayo yanahusiana na jinsia isipokuwa kukiwa na umuhimu kwa ajili ya utafiti au takwimu sambamba na hilo kupewa taarifa mtoa taarifa.[246]

Aidha, Sheria hii pia imekataza kudai au kutoa tarifa za binafsi zinahusiana na imani za dini au imani za kifilosofia isipokuwa kwa taasisi inayohusika na mambo ya kiroho au ya kidini au taarifa ambazo zinahusika na taasisi yake na taarifa ambazo zina umuhimu katika kufikia malengo makuu ya mtoa taarifa au taasisi inazohusiana na imani.[247]

---

[244] Sheria ya Afrika ya Kusini ya kulinda taarifa binafsi Nam 4 ya 2013.
[245] Ibid Kifungu cha 72.
[246] Ibid Kifungu cha 29(a) na (b).
[247] Ibid Kifungu cha28.

### (c) Wajibu wa Kuwa na Usiri.

Sheria imemtaka mtu yeyote ambaye anafanya kazi kwa niaba ya mdhibiti au kwa maelekezo ya mdhibiti wa taarifa, kutunza siri baada ya kumaliza muda wake, ajira yake au mkataba wake, isipokuwa kwa taarifa ambazo zinakubaliwa na sheria au kwa taarifa ambazo zinahusisha majukumu ya Mtu Kisheria.[248]

### 5.3.3 Sheria ya Uganda ya Ulinzi wa Faragha na Taarifa Nam. 9 ya 2019.

Lengo la Sheria ni kulinda faragha ya mtu binafsi na taarifa binafsi kwa kusimamia ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kutoa haki za watu ambao taarifa zao zimekusanywa na majukumu ya wakusanyaji wa taarifa, wadhibiti wa taarifa, kudhibiti matumizi au utoaji wa taarifa binafsi; na mambo ambayo yanayohusiana uhifadhi wa taarifa.[249]

### (a) Misingi/Taratibu za kulinda taarifa.

Kwa mujibu ya Sheria, misingi maalum inajumuisha kukusanya, kuchakata na kudhibiti taarifa kwa haki na kisheria sambamba na kuhifadhi taarifa binafsi kwa kipindi kinachokubalika kisheria, kuchukua taarifa inayohitajika na kuzilinda kwa utaratibu unaokubalika.[250]

### (b) Kuanzishwa kwa Afisi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

[248] Ibid Kifungu cha 54.
[249] Sheria ya Uganda ya Ulinzi wa Taarifa na Faragha Nam. 9 ya 2019.
[250] Ibid kifungu cha 3(1)(a-g).

Sheria imeanzisha Afisi maalum ya kusimamia ulinzi wa taarifa binafsi itakayokuwa na jukumu la kulinda taarifa binafsi, kusimamia wachakataji wa taarifa na wahifadhi wa taarifa.[251]

**(c) Ridhaa ya Kukusanya au Kuhifadhi Taarifa Binafsi**.

Kwa mujibu ya sheria mtu yeyote haruhusiwi kukusanya taarifa au kuhifadhi tarifa binafsi bila ya kupata ridhaa kwa muhusika (mtoa taarifa), isipokuwa katika masuala ya usalama wa taifa, matakwa ya sheria, kwa ajili ya utafiti, kuchunguza, kushtakiwa au kuadhibiwa kwa kosa au uvunjaji wa sheria sambamba na masuala ya tiba.[252]

**(d) Marufuku ya Kukusanya na Uhifadhi wa Taarifa binafsi ambazo Nyeti**

Sheria imepiga marufuku kwa mtu yeyote kukusanya au kuhifadhi taarifa binafsi inayohusiana na dini au falsafa ya imani, maoni ya kisiasa, masuala ya jinsi na jinsia, taarifa za kifedha, hali ya afya au kumbukumbu za matibabu. Sheria imempa uwezo mkusanyaji wa taarifa au mhifadhi wa taarifa kukusanya taarifa hizo zikiwa zimetolewa kwa uhuru na muhusika bila ya kulazimishwa.[253]

**(e) Ulinzi/uhifadhi wa faragha.**

[251] Ibid kifungu cha 4(1,2,3 na 4)
[252] Ibid kifungu cha 7(1) (2)(a)-(e).
[253] Ibid kifungu cha 9(1,2,3)(a,b,c)(I,ii,iii)

Sheria imeweka kifungu cha ulinzi wa faragha kwa kumlazimisha Mkusanyaji wa taarifa, mchakataji au mdhibiti kukusanya, kushikilia au kuchakata taarifa binafsi katika hali ambayo inakiuka haki ya faragha ya mtoa taarifa, hivyo mtoa taarifa anatakiwa awe katika mazingira ya kulindiwa haki yake ya faragha.[254]

### (f) Makosa katika Kuvunja ulinzi wa taarifa binafsi kinyume na Sheria.

Sheria imeweka makosa mbali mbali ambayo yanakatazwa kufanywa na mkusanyaji wa taarifa au mdhibiti wa taarifa ikiwemo kutoa taarifa binafsi bila ya kufuata utaratibu wa sheria, kuuza taarifa, kuchakata taarifa kinyume na sheria, kutoa taarifa binafsi nje ya nchi bila ya kufuata miongozo iliyopo na kufanya kazi bila ya kusajiliwa.

### (g) Kupata au kutoa taarifa binafsi kinyume cha Sheria.

Mtu hatoruhusiwa kukusanya taarifa kinyume cha sheria au kutoa taarifa kwa mtu mwengine taarifa ya kibinafsi iliyohifadhiwa au kuchakatwa na mkusanyaji wa taarifa, mdhibiti wa taarifa, na mtu anayekwenda kinyume na sheria atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini.[255]

Aidha, sheria hii pia imekataza kuuza taarifa binafsi, kuiharibu kwa makusudi au kufanya makosa yote mawili kwa pamoja na atakaye kwenda kinyume

[254] Ibid kifungu cha 10.
[255] Ibid kifungu cha 35 na 36.

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria.[256]

### 5.3.4 Sheria ya Mauritius ya Ulinzi wa Taarifa Nam. 120 ya 2017

Lengo la kutungwa kwa Sheria ni kuimarisha udhibiti na ulinzi wa taarifa kibinafsi, kuimarisha haki za msingi za faragha ya mtu pamoja na kulinganisha na matakwa ya viwango vya kimataifa vya ulinzi wa faragha.[257]

#### (a) Kuanzishwa kwa Afisi ya Ulinzi wa Taarifa.

Sheria imeanzisha Afisi ya Umma ya Ulinzi wa Taarifa kwa lengo la utekelezaji wa majukumu ya ulinzi wa taarifa chini ya sheria hii, na Afisi itakuwa huru katika utekelezaji wa majukumu yake, itafanya kazi kwa uhuru kamili na inasimamiwa na kamishna wa ulinzi wa taarifa.[258]

#### (b) Uwezo wa kuingia katika eneo na kufanya ukaguzi.

Sheria imempa uwezo Afisa aliyeidhinishwa kuingia katika majengo yoyote, kwa ruhusa ya mahakama ikiwa kuna hofu ya kuvunjwa kwa sheria kwa lengo la kufanya ukaguzi au kuangalia usalama wa taarifa au kutumia uwezo katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.[259]

[256] Ibid kifungu cha 37.
[257] Sheria ya Mauritius ya ulinzi wa Taarifa Nam. 120 ya 2017.
[258] Ibid, kifungu cha 4
[259] Ibid, kifungu cha 11

### (c) Kusajiliwa kwa Mchakataji au Mkusanyaji wa Taarifa.

Sheria inaelekeza kusajiliwa kwa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa.[260]

Aidha, mtu yeyote anayekusudia kufanya kazi kama mtunza taarifa au mchakata taarifa, atalazimika kupeleka maombi kupitia fomu maalum na kupeleka kwa Kamishna. Kamishna ana uwezo wa kumsajili au kutokumsajili kwa kushindwa kukamilisha matakwa ya sheria.[261]

### (d) Taratibu zinazohusiana na uchakataji wa taarifa binafsi.

Sheria hii imemtaka Mdhibiti au Mchakataji wa wa taarifa kuhakikisha kuwa taarifa binafsi inachakatwa au kuchukuliwa kihalali, kwa haki na kwa njia ya uwazi na madhumuni yaliyokusudiwa.[262]

### (e) Wajibu wa kuharibu Taarifa binafsi.

Sheria imeelekeza utaratibu wa kuharibu taarifa binafsi pale ambapo madhumuni ya kutunza taarifa yamemalizika au kutokufikiwa kwa lengo la uhifadhi wa taarifa hizo.[263]

---

[260] Ibid,kifungu cha 14
[261] Ibid, kifungu cha 15
[262] Ibid Kifungu cha 21(a-f)
[263] Ibid Kifungui cha 27 (1)(a na b)(2).

**(f) Taarifa Binafsi za Watoto**.

Sheria imepiga marufuku kwa mtu atakayeshughulikia taarifa binafsi za mtoto ambaye yupo chini ya umri wa miaka 16, kutoa au kuchukua taarifa zozote bila kupata idhini ya mzazi au mlezi wa mtoto.[264]

**(g) Kusafirisha Taarifa Nje ya Nchi**

Mdhibiti au mchakataji anaweza kuhamisha taarifa binafsi kwa kwenda nje ya nchi kwa kumpa taarifa Kamishna wa Afisi ya Ulinzi Taarifa au kupata uthibitisho kwa Kamishna wa Ulinzi wa Taarifa binafsi, baada ya kufahamishwa kuhusu hatari zinazoweza kupatikana kutokana na uhamisho huo.[265]

**(h) Utoaji wa Taarifa Binafsi Bila ya Halali.**

Sheria imepiga marufuku kwa Mdhibiti yeyote ambaye, bila sababu za kisheria kufichua taarifa binafsi kwa namna yoyote ambayo haiendani na malengo ya ukusanyaji wa taarifa hiyo, au kwa malengo ambayo hayaendani na madhumuni ya yaliyokusudiwa, ikibainika kama mdhibiti amefanya hivyo atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiopungua rupees laki mbili.[266]

---

[264] Ibid kifungu cha 30(1 na 2).
[265] Ibid kifungu cha 36(1)(a, b na c).
[266] Ibid kifungu cha 42 na 43.

### 5.3.5 Sheria ya Zambia ya Ulinzi wa Taarifa Nam 3 ya 2021.

Lengo kuu la Sheria ni kuweka mfumo madhubuti na mzuri kwa ajili ya matumizi na ulinzi wa taarifa na kuweka taratibu za ukusanyaji wa taarifa pamoja na kuanzisha Afisi ya Ulinzi wa Taarifa na kuwasajili wa Wakusanyaji au Wanaoshughulikia taarifa.[267]

#### (a) Kuanzishwa kwa Afisi ya Kamishna wa Ulinzi wa Taarifa.

Sheria hii imeanzisha Afisi ya Kamishna wa Ulinzi wa Taarifa chini ya Wizara inayoshughulikia masuala ya mawasiliano. Afisi hiyo itakuwa na jukumu la kuweka taratibu za ulinzi wa taarifa na usiri katika jamhuri ya Zambia, kuwasajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa sambamba na kuishauri Serikali njia bora za ulinzi wa taarifa. Afisi imepewa uwezo wa kufanya utafiti katika mambo ambayo yanahusiana na utafutaji wa njia bora za ulinzi wa taarifa na kupokea na kufanya uchunguzi juu ya malalamiko yanayotokana na sheria hii.[268]

#### (b) Mkaguzi.

Sheria pia imetoa nafasi ya kuchaguliwa kwa Afisa Mkaguzi kutoka miongoni mwa Watumishi wa Umma kwa lengo la kuhakikisha kuwa sheria inafuatwa. Sheria imempa uwezo Mkaguzi wa kuingia katika maeneo ya wakusanyaji wa taarifa au wachakataji wa taarifa, kufanya ukaguzi wa vifaa vinavyotumika

[267] Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Zambia Nam. 3 ya 2021.
[268] Ibid Kifungu cha 4 (1) na (2)(a-j).

katika uchakataji wa taarifa na ukusanyaji wa taarifa na kuondoa vitu mbali mbali ambavyo vinatumika kinyume na sheria.[269]

### (c) Kurejeshwa kwa Mali.

Sheria hii imetoa uwezo wa kurejeshwa kwa mali ambazo zimezuiliwa baada ya kuwa Mkusanyaji wa taarifa au Mchakataji wa taarifa kubainika kuwa amechukua vifaa hivyo kimakosa na Sheria inataka mara tu baada ya kubainika kuwa hana hatia, vifaa hivyo virejeshwe kwa haraka bila ya kuchelewa.[270]

### (d) Taratibu za Uchakataji wa Taarifa Binafsi.

Sheria imewataka Wachakataji wa taarifa na Wakusanyaji wa taarifa kuhakikisha kuwa taarifa binafsi zinakusanywa na kufanyiwa kazi kisheria, kwa haki na usawa, kuchukua taarifa kwa kiwango kinachohitajika kutokana na jambo linalofanyika na kufanyiwa kazi kwa mujibu wa ulinzi wa taarifa.[271]

### (e) Uchakataji wa Taaraifa Muhimu (Nyeti).

Sheria inaelekeza taarifa nyeti zichukuliwe kwa ajili ya ushahidi katika ngazi za Mahakama au ikiwa uchakataji ni muhimu kwa masuala ya kukinga au

[269] Ibid kifungu cha 7(1)na (2) na kifungu cha 8.
[270] Ibid kifungu cha 11(1) (a) na (b)
[271] Ibid kifungu cha 12(1)(a)-(g).

usalama wa dawa, kwa ajili ya tahmini ya kazi kwa muajiriwa, au kwa maslahi ya umma.[272]

**(f) Ridhaa ya Uhalalishaji wa Taarifa na Pingamizi.**

Kwa mujibu wa Sheria mkusanyaji au mchakataji mwenye taarifa anaweza kutoa ridha ya ukusanyaji wa taarifa zake kwa maandishi, na kuelezwa na akiwa atakataa mkusanyaji wa taarifa au mchakataji wa taarifa haruhusiwi kuendelea na ukusanyaji au uchakataji wa taarifa.[273]

**(g) Uchukuaji wa taarifa kwa Watoto na Watu Wenye Mazingira Maalum.**

Sheria imeweka utaratibu wa kupata ridhaa ya kuchukua taarifa kwa watoto wadogo na watu ambao wapo katika mazingira magumu. Ridhaa itatolewa na wazazi au walezi na kuchukua hatua maalum katika kuchakata taarifa.[274]

**(h) Makosa na Adhabu kwa Kuvunja Taratibu.**

Kwa mujibu wa Sheria ikiwa Kampuni itafanya kosa chini ya sheria hii na kutiwa hatiani adhabu yake itakuwa ni faini ya kiwango Milioni Mia Moja (Unit) au Asilimia mbili ya mauzo ya mwaka. Iwapo akiwa aliyefanya kosa ni mtu

[272] Ibid kifungu cha 14(1)(a)-(c)
[273] Ibid kifungu cha 15(1,2,3,4,5,6,7,8 na 9).
[274] Ibid kifungu cha 17(1,2,3, na 4)

binafsi na akatiwa hatiani adhabu yake itakuwa ni kiwango cha Milioni Moja (Unit) au kifungo kisichopindukia miaka 5 au vyote viwili faini na kifungo.[275]

### 5.3.6 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya United Kingdom Sura ya 29 ya 1998. (Data Protection Act 1998 Chapter 29).

Sheria imetungwa kwa lengo la kuweka vifungu na taratibu ambazo zinajumuisha ukusanyaji wa taarifa pamoja na taratibu za kuweza kuruhusu utolewaji wa taarifa binafsi.[276]

#### (a) Haki ya Upatikanaji wa Taarifa Binafsi.

Mkusanyaji wa taarifa atakuwa na jukumu la kumpa taarifa mtu yeyote wakati wa ukusanyaji wa taarifa ikiwa amepokea maombi rasmi kwa maandishi au kwa kesi maalum.[277]

#### (b) Kukataza Kutumia Taarifa kwa malengo ya kibiashra.

Mkusanyaji wa taarifa anakatazwa kutumia taarifa binafsi kwa ajili ya biashara na ikiwa mahakama itabaini kuwa mtu huyo ametumia au kukusanya kwa lengo la kibiashara, mahakama inaweza kuamuru kuchukuliwa hatua.[278]

[275] Ibid kifungu cha 18(1)(ab)(2)
[276] Sheria ya Ulinzi wa Taarifa UK Sura 24 ya Mwaka 1998.
[277] Ibid kifungu Cha (1)(a)-(d), (2)
[278] Ibid kifungu cha 11(1)-(3).

### (c) Fidia kwa Kushindwa Kufuata Taratibu.

Sheria imekataza matumizi mabaya ya taarifa au kutumia taarifa kinyume na utaratibu. Aidha, sheria imempa uwezo muhusika wa taarifa kudai fidia kutokana usumbufu ambao ameupata au uliosababishwa na matumizi mabaya ya taarifa zake.[279]

### (d) Kukusanya taarifa bila ya kusajiliwa.

Sheria hii pia imekataza mtu yeyote kufanya shughuli ya ukusanyaji wa taarifa bila ya kusajiliwa, isipokuwa kwa taarifa ambazo zinazokubalika kwa mujibu wa sheria, kwa mfano taarifa zinazokusanywa kwa ajili ya uchakataji ambazo kwa njia inayokubalika na sheria au kwa kazi maalum kama historia na takwimu.[280]

### (e) Wajibu wa Kuarifu Mabadiliko.

Sheria imempa wajibu mkusanyaji wa taarifa kueleza mabadiliko yoyote ambayo yatafanywa katika shughuli za ukusanyaji na uhifadhi wa taarifa, na taarifa hiyo inatakiwa kuwasilishwa katika Afisi ya Uhifadhi wa taarifa. Aidha, ikiwa mabadiliko hayo yanaathiri na taarifa za watu basi mkusanyaji anawajibika pia kuwapa taarifa na watoa taarifa.

---

[279] Ibid Kifungu cha 13(1)(2) (a)-(c).

[280] Ibid Kifungu cha 17(1)-(3).

### 5.3.7 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Botswana Nam. 32 ya Mwaka 2018.

Lengo la kutungwa kwa Sheria hii na kuhakikisha kwamba kunawekwa taratibu za kulinda haki ya faragha ya watu binafsi pamoja na kuanzisha Kamisheni ya Ulinzi wa Taarifa na binafsi.[281]

**(a) Kiapo cha Kutunza Siri (usiri).**

Sheria imemtaka Kamishna na afisa yeyote au mfanyakazi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa kula kiapo cha kutunza siri mbele ya Waziri kwa namna itakavyoelekezwa kwa lengo la kuhakikisha kunakuwa na usiri pamoja na siri za taarifa za watu binafsi.[282]

**(b) Uhifadhi wa Taarifa Nyeti.**

Sheria inamtaka mdhibiti wa taarifa binafsi atakapo kuwa anakusanya au anahifadhi taarifa ambazo ni nyeti ahakikishe ametumia njia bora na salama katika kuhakikisha kuwa ulinzi sahihi na usalama wa taarifa hizo.[283]

**(c) Ukomo na Uwezo wa Uhifadhi Taarifa.**

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa imewataka wahifadhi wa taarifa kuwa na ukomo wa uhifadhi wa taarifa hizo, na zinatakiwa kuharibiwa mara baada ya kumalizika

---

[281] Sheria ya ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Botswana Nam. 32 ya 2018
[282] Ibid kifungu Cha 8
[283] Ibid kifungu cha 12.

muda wa matumizi yake, isipokuwa kwa idhini ya mwenye taarifa au kama itakavyoelekezwa na sheria yoyote ya nchi.[284]

### (d) Marufuku kwa Uhifadhi wa Taarifa Nyeti za Binafsi.

Sheria imekataza kukusanya au kuhifadhi taarifa binafsi ambazo ni nyeti isipokuwa kwa masuala ambayo yameruhusiwa kisheria. Miongoni mwa mbambo hayo ni kwa ridhaa ya maandishi ya mtoa taarifa, mwenye taarifa ameamua kufanya kuwa taarifa ya umma, kutoa taarifa hizo ni muhimu kwa maslahi ya umma, au kwa ajili ya kufanya utafiti ambao utasaidia katika jambo husika.[285]

### (e) Kusafirisha Taarifa Nje ya Nchi.

Kwa mujibu wa sheria uhamishaji wa taarifa binafsi kutoka Botswana kwenda nchi nyengine haukubaliki isipokuwa nchi ambazo Waziri ataridhia kwa kuzitangaza kupitia Gazeti la Serikali.[286]

Aidha Sheria hii pia imeruhusu kusafirisha taarifa zilizohifadhiwa au zilizokusanya katika nchi zinazoendelea ikiwa tu nchi hizo zitahakikisha usalama wa taarifa hizo binafsi na kuhakikisha kuwa taarifa hizo zitakuwa siri.[287]

[284] Ibid Kifungu cha 15.
[285] Ibid kifungu cha 20.
[286] Ibid kifungu cha 48.
[287] Ibid kifungu cha 49.

### 5.3.8 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Ghana Nam. 843 ya Mwaka 2012.

Sheria inaweka misingi ya kusimamia ukusanyaji, utoaji na usimamizi wa taarifa binafsi kwa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa . Sheria hii inaanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa, ili kulinda faragha ya taarifa ya mtu binafsi kwa kudhibiti uhifadhi wa taarifa binafsi na kuweka utaratibu wa kupata taarifa binafsi.[288]

**(a) Kuazishwa kwa Kamisheni ya kuhifadhi taarifa.**

Sheria imeanzisha Kamisheni ya Uhifadhi Taarifa, ambayo ina jukumu la kulinda usiri wa taarifa, kutoa maelekezo na utaratibu wa ukusanyaji, na kusimamia masuala ya uongozi. Sambamba na hilo Tume imepewa uwezo wa kufanya uchunguzi wa malalamiko yanayohusiana na masuala ya uhifadhi wa taarifa, kuwasajili wakusanyaji wa taarifa na kudhiti taarifa za wakusanyaji, wachakataji wa taarifa binafsi kwa mujibu wa sheria.[289]

**(b) Uchakataji wa Taarifa Binafsi**.

Sheria imemtaka mtu yeyote ambaye anachakata taarifa binafsi kwa mujibu wa sheria, kuzingatia suala la ulinzi wa faragha katika ukusanyaji au uchakataji wa taarifa.

---

[288]Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Ghana ya 2012.
[289] Ibid kifungu cha (1)-(3).

Aidha, Mdhibiti wa taarifa au mchakataji wa taarifa atakuwa na wajibu wa kuheshimu taarifa za kigeni, mchakataji wa taarifa atalazimika kufuata utaratibu wa sheria ya ulinzi ya mambo ya nje au sheria kama ilivyoelekeza kuhusu utaratibu wa ukusanyaji wa taarifa hizo.[290]

**(c) Uhalali wa Ukusanyaji wa Taarifa na Pingamizi**.

Sheria imezingatia suala la ridhaa kwa mtu ambaye anatakiwa kutoa taarifa binafsi kwa mujibu wa sheria, imekatazwa kwa mtu yeyote kukusanya taarifa au kuzihifadhi taarifa binafsi bila ya kupata ridhaa ya mtoa taarifa.

Aidha, sheria hii imeruhusu kuchukuwa taarifa ikiwa tu kuna haja maalum kwa madhumuni ya mkataba ambao unamuhusu mtoa taarifa, kuidhinishwa au kwa matakwa ya kisheria, au kwa ajili ya maslahi ya umma.[291]

**(d) Wajibu wa Kutoa Taarifa kwa mtoa taarifa binafsi**.

Kwa mujibu Sheria, mkusanyaji wa taarifa au mhifadhi wa taarifa anatakiwa amjuulishe mtoa taarifa binafsi lengo la kukusanya taarifa, ukomo na taarifa hizo, matumizi ya taarifa na kumhakikishia mtoa taarifa usalama wa taarifa zake.[292]

**(e) Uhifadhi wa Kumbukumbu**.

---

[290] Ibid kifungu cha 18.
[291] Ibid kifungu cha 20.
[292] Ibid kifungu cha 23 na 24.

Sheria imemtaka mtu yeyote ambaye anaehifadhi taarifa kwa njia yeyote ile, kuhifadhi taarifa hizo si zaidi ya kipindi ambacho kimekusudiwa na malengo ya uhifadhi wa taarifa. Aidha, Sheria imepiga marufuku kwa mdhibiti wa taarifa kuhifadhi taarifa zaidi ya muda uliokusudiwa kudhibiti taarifa, isipokuwa kwa ridhaa ya mtoa taarifa.[293]

### 5.3.9 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Antigua na Barbuda Nam. 10 ya 2013.

Sheria imekuwa na lengo kuhamasisha ulinzi wa taarifa binafsi zinazochakatwa na Mashirika ya Umma na Mashirika binafsi ambayo yanafanya kazi ya kukusanya na kuhifadhi taarifa binafsi.[294]

#### (a) Utaratibu wa kutoa taarifa binafsi.

Sheria imekataza moja kwa moja utoaji wa taarifa isipokuwa kwa utaratibu wa utoaji wa taarifa binafsi katika mambo ya msingi ikiwemo madhumuni ya taarifa binafsi na lengo linalotajwa katika Sheria kwa taasisi yoyote inayohusiana na mtoaji wa taarifa, takwimu, historia na kwa kuzingatia maslahi ya umma.[295]

#### (b) Uadilifu katika matumizi ya taarifa.

[293] Ibid kifungu cha 24.
[294] Sheria ya ulinzi wa Taarifa ya Antigua na Barbuda Nam 502.
[295] Ibid kifungu cha 7.

Kwa mujibu wa Sheria mtumiaji wa taarifa binafsi anatakiwa kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa taarifa binafsi ni sahihi, kamili, wala taarifa haikupotoshwa na kuzingatia malengo ya kukusanywa kwa taarifa.[296]

**(c) Haki ya Upatikanaji wa taarifa binafsi.**

Kwa mujibu wa sheria chombo cha umma au chombo binafsi kitakuwa na uwezo wa kupata taarifa binafsi kwa ombi maalum la maandishi na kuambatanisha na malipo yaliyowekwa kwa lengo la upatikanaji wa taarifa binafsi, hata hivyo mtoa taarifa atalazimika kumjuulisha mwenye taarifa zake na kuridhia kutolewa kwa taarifa hizo.[297]

**(d) Ruhusa ya kutumia taarifa binafsi**.

Sheria imeweka mazingira ambayo yanaruhusiwa kutolewa taarifa kwa sababu maalum na za msingi ambazo zitasababisha kwa mtu au taasisi kuweza kuruhusiwa kutolewa kwa taarifa binafsi. Miongoni mwa mazingira hayo ni kufanywa uchuguzi wa makosa ya jinai, kufanya makadirio ya ukusanyaji wa aina yeyote ile ya kodi, kwa ajili ya kufanya utafiti na maslahi ya umma.[298]

**(e) Haki ya kukata rufaa.**

[296] Ibid kifungu cha 10.
[297] Ibid kifungu cha 12.
[298] Ibid kifungu cha 19.

Sheria imetoa haki ya kukata rufaa kwa mtu au chombo chochote kutokana na maamuzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Taarifa katika ngazi za Mahakama.[299]

**(f) Adhabu kwa Jumla**.

Mtu anayetenda kosa kwa mujibu wa Sheria hii ikiwemo kuvujisha taarifa, kuuza taarifa, kutumia taarifa kinyume na malengo ya ukusanyaji na ukusanyaji wa taarifa bila ya kusajili ambapo adhabu yake ni faini au kifungo au vyote viwili kwa pamoja.[300]

### 5.3.10 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Zimbabwe Nam. 5 ya 2021

Sheria hii inatoa ulinzi wa taarifa binafsi kwa kuzingatia Azimio la Haki za Binadamu kwa mujibu wa Katiba na maslahi ya Umma. Aidha sheria imeanzisha Mamlaka ya Ulinzi wa Taarifa na kutoa majukumu yao kwa taasisi husika ili kuweza kupata haki na kusimamia haki za faragha pamoja na ulinzi wa taarifa binafsi.[301]

**(a) Mamlaka za Kuchakata Taarifa**.

Mtu yeyote anayepata taarifa na kufanya kazi chini ya Mamlaka ya Mdhibiti au ya mchakataji wa taarifa, pamoja na mchakataji mwenyewe au mtu binafsi

[299] Ibid kifungu cha 24.
[300] Ibid kifungu cha 23.
[301] Sheria ya kuu;inda taarifa ya Zimbabwe Nam 5 ya 2021.

anaweza kufanya kazi ya kukusanya taarifa kama ilivyoelekezwa na Mdhibiti Mkuu wa taarifa bila ya kuathiri wajibu wowote uliowekwa na sheria.[302]

**(b) Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Taarifa Binafsi**.

Sheria imeanzisha Chombo ambacho kitakuwa na jukumu la kusimamia masuala ya uchakataji wa taarifa sambamba na kuhakikisha kuwa taarifa zinazotolewa zinakuwa za ukweli na kuaminika.[303]

**(c) Uhamisho wa taarifa binafsi nje ya nchi**.

Sheria hii imekataza kuwa hairuhusiwi kwa mchakataji wa taarifa kutoa taarifa nje ya nchi isipokuwa kwa kuhakikisha kuwa kuna usalama mkubwa wa taarifa hizo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii. Vile vile sheria hii imekataza utoaji wa taarifa binafsi kwa mtu wa tatu ambaye yupo katika nchi za nje isipokuwa kwa kuhakikisha usalama wa kulindwa kwa taarifa katika nchi hiyo.[304]

**(d) Makosa na Adhabu**.

Mtumishi yeyote wa mamlaka au mtaalamu yeyote, mdhibiti au mkusanyaji wa taarifa atakayekiuka masharti ya Sheria hii atakuwa na hatia ya kosa na akitiwa hatiani atawajibika kwa kulipa faini au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au faini na kifungo.[305]

---

[302] Ibid kifungu cha 17.
[303] Ibid kifungu cha
[304] Ibid kifungu cha 28(1na 2).
[305] Ibid kifungu cha 33

### (e) Kukata Rufaa.

Mtu yeyote atakayeguswa au kuumizwa na uamuzi wa Mamlaka anaweza kukata rufaa katika Mahakama ya Utawala ambayo ina uwezo wa kusikiliza rufaa, aidha ikibainika kuwa mtu huyo aliekata rufaa hakutendewa haki kutokana na maamuzi hayo atarejeshewa haki yake kwa mujibu wa sheria.[306]

## 5.3.11 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Malaysia Nam. 70 ya Mwaka 2010.

Lengo la Sheria ni kudhibiti uhifadhi wa taarifa binafsi katika mambo yanayohusiana na miamala ya biashara na mambo ambayo yanahusiana na ukusanyaji na uhifadhi wa taarifa.[307]

### (a) Misingi ya Usalama wa Taarifa.

Sheria hii imemtaka mtumiaji wa taarifa wakati wa uhifadhi wa taarifa binafsi, kuchukua hatua madhubuti za kulinda taarifa dhidi ya hasara yoyote ambayo itajitokeza kwa kupotea taarifa binafsi, matumizi mabaya, marekebisho

[306] Ibid kifungu cha 34.
[307] Sheria ya ulinzi wa taarifa ya binafsi ya Malaysia Nam 709 ya 2010.

yasiyofuata Sheria, utumiaji usioidhinishwa au utoaji usiofuata utaratibu wa kisheria.[308]

**(b) Kamati ya Ushauri.**

Sheria hii imeanzisha Kamati Maalum ya Ushauri wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi, kamati ambayo itakuwa na jukumu la kumshauri Kamishna juu ya mambo yote yanayohusu ulinzi wa taarifa binafsi, vilevile itashauri usimamizi unaofaa na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Hata hivyo kamishna halazimiki kufuata ushauri huo.[309]

**(c ) Baraza la Rufaa**.

Sheria imetoa mamlaka ya kukata rufaa katika masuala ya usajili wa leseni au kukataliwa kupatiwa leseni. Rufaa itakatwa kwa Baraza la Rufaa lililoundwa chini ya sheria.[310]

**(d) Kutoa/Kusafirisha taarifa binafsi nje ya nchi**.

Sheria imekataza moja kwa moja mtumiaji wa taarifa binafsi, kuhamisha taarifa yoyote binafsi kwa mujibu wa sheria kwenda nje ya Malaysia, isipokuwa nchi ambayo imeainishwa na Waziri baada ya mapendekezo ya kamishna, na taarifa hiyo kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.[311]

---

[308] Ibid kifungu cha 9(1).
[309] Ibid kifungu cha 71(1) (a na b)(2).
[310] Ibid kifungu cha 84.
[311] Ibid kifungu cha 129(1)

Waziri atapendekekeza nchi ambazo zinazo usalama mkubwa katika ulinzi wa mkubwa katika ulinzi wa taarifa binafsi.[312]

### 5.3.12 Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ya Swedish na Finiland 1050 ya 2018.

Madhumuni ya Sheria ni kubainisha na kuongeza taratibu za ulinzi wa taarifa binafsi kama ilivokubaliwa na Bunge la Ulaya (EU) mnamo mwaka 2016 na Baraza kuu Ulinzi wa taarifa binafsi kuhusiana na uhifadhi wa taarifa binafsi.[313]

#### (a) Uhalali wa Uhifadhi wa Taarifa.

Kwa mujibu Sheria taarifa binafsi inaweza kukusanywa kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1) cha Kanuni za Ulinzi wa taarifa ikiwa, mtu yeyote anayefanya kazi ya kukusanya taarifa atakuwa na wajibu wa kukusanya taarifa kwa mujibu wa sheria au kwa ajili ya utafiti wa kisayansi au kwa ajili historia.[314]

#### (b) Ukomo wa umri wa mtoto wa kutoa taarifa.

Kwa mujibu wa Mikataba ya Kulinda Taarifa Binafsi katika Kifungu cha 6(1)(a), ukusanyaji wa taarifa za mtoto unatakiwa uhakikishe angalau au amefika umri wa miaka kumi na tatu (13). Sheria hii imetoa kipaumbele katika kulinda haki ya taarifa binafsi mpaka kwa watoto ambao wapo chini ya umri wa miaka kumi na tatu.[315]

---

[312] Ibid kifungu cha 129(2)(a na b)
[313] Sheria ya ulinzi wa taaria ya swidesh na finish nam 1050 ya 2018.
[314] Ibid Kifungu cha 4 (1,2,3 na 4)
[315] Ibid kifungu cha 6.

### (c) Haki ya Kushtaki

Kwa mujibu wa Sheria, mtoaji wa taarifa anaweza kumshtaki Mkusanyaji wa Taarifa au Mchakataji wa Taarifa ikiwa tu atabaini kuwa kuna ukiukwaji wa Sheria katika jambo lolote ambalo linahusiana na sheria au kuhusiana na taarifa zake. Aidha, Mamlaka ya ulinzi wa taarifa binafsi mara baada ya kutambua jambo liliopo mahakamani, itasitisha zoezi la uchakataji wa taarifa binafsi mpaka pale Mahakama itapotoa maamuzi.[316]

### (d) Kulipa Fidia.

sheria imetoa mamlaka ya kutunga kanuni ya ulipaji wa faini kwa mtu ambaye atahusika na uvunjifu wa sheria kwa wachakataji wa taarifa binafsi, wakusanyaji na wanao hifadhi taarifa binafsi na kulazimika kulipa faini kwa mujibu wa sheria. Vilevile sheria hii pia imeweka wazi kuwa hakuna faini ambayo atatozwa mdhibiti wa taarifa kwa kutoa taarifa binafsi kwa ajili ya mshukiwa wa kosa la jinai.[317]

---

[316] Ibid kifungu cha 21.
[317] Ibid kifungu cha 22

# SURA YA SITA

## 6.0 MATOKEO YA UTAFITI

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu unaojielekeza katika matakwa na malengo ya kuanzishwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Zanzibar. Matokeo haya yamejumuisha maeneo muhimu yaliyobainika katika maoni ya wadau, sera na sheria mbalimbali za ndani ya Zanzibar zinazohusiana na ukusanyaji wa taarifa binafsi za wananchi, pamoja na uzoefu wa sheria za ulinzi wa taarifa binafsi za nchi mbali mbali pamoja na mambo muhimu yaliobainika katika miongozo mbali mbali ya kimataifa.

## 6.2 Njia Zilizotumika katika Utafiti

Njia zilizotumika kufanyia utafiti eneo la ulinzi wa taarifa binafsi, zimehusisha utafiti wa ndani kwa kupitia miongozo mikuu ya nchi, sera na sheria mbalimbali, uzoefu wa sheria za ulinzi wa taarifa binafsi katika nchi mbali mbali, kuangalia mikataba mbali mbali ya kimataifa inayotoa muongozo juu ya ulinzi wa taarifa binafsi.

Aidha njia nyengine ni kukutana na wadau wanaohusika na eneo hili la utafiti, ambao ni Wizara tofauti, Taasisi za Umma na Binafsi zinazohusiana na usimamizi na ukusanyaji wa taarifa za binafsi, Asasi za Kiraia na Mashirika ya Kiserikali na yasio ya Kiserikali.

## 6.3 Makundi ya Wadau (Sampuli ya utafiti) na Uchambuzi wa Takwimu

Kufikia malengo ya utafiti huu, makundi mbali mbali yalihusishwa. Makundi hayo yalijumuisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Taasisi za binafsi zinazohusiana na masuala ya Taarifa binafsi, Wamiliki wa taasisi za uchakataji taarifa, Wataalamu mbali mbali wa mifumo na wadau wengine wa taarifa binafsi. Wadau hao ni kama wafuatao:

1. (OR), Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora
2. ZAECA
3. Idara ya Uhamiaji Zanzibar
4. Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali
5. Tume ya Uchaguzi Zanzibar
6. Mfuko wa Barabara
7. Jeshi la Polisi
8. Mamlaka ya Serikali Mtandao
9. Mamlaka ya Usajili wa Matukio ya Kijamii
10. Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi
11. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii
12. Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale
13. Mamlaka ya Mapato Zanzibar
14. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi
15. Chuo Kikuu cha Taifa – SUZA
16. Benki ya Watu wa Zanzibar
17. OR, Fedha na Mipango
18. Makampuni ya Simu za Mkononi
19. Mahkama
20. Shirika la Umeme

21. Mamlaka ya Mapato Tanzania
22. Mamlaka ya Uwekezaji
23. Taasisi Binafsi na Makampuni
24. Wadau wa Masuala ya Uchakataji Taarifa
25. Watafiti
26. Wataalamu wa Mifumo
27. Asasi za Kiraia

Vikao vya wadau vilifanyika katika maeneo tofauti ya Zanzibar. Jumla ya wadau waliohudhuria katika vikao hivyo ni **117** sawa na **asilimia (91.4%)** ya wadau walioalikwa. Katika idadi hii ya wadau makundi yaliyoshirikishwa kwa idadi kubwa ni pamoja watendaji kutoka taasisi za Serikali zinazoshughulika na uwekaji wa taarifa binafsi. Kwa uchambuzi wa kijinsia utafiti umeonesha jumla ya wanawake **39** walishiriki kutoa maoni yao na wanaume walikuwa **78.**

Wawakilishi kutoka makundi mbalimbali ya wadau ambao wameshiriki katika utafiti huu wametoa mapendekezo tofauti kuhusu mahitaji ya kuanzishwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa ambapo wameunga mkono suala hilo baada ya kuona haja kubwa ya kuwepo kwa Sheria hiyo ambayo italinda taarifa za watu kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mifumo, mitandao ya kijamii na mabadiliko ya sayansi na teknolojia iliyopo duniani kwa ulimwengu wa sasa.

Aidha, wadau wamesisitiza kuimarishwa masuala ya kiutendaji kwa taasisi zilizopo hivi sasa ambazo zinakusanya taarifa za watu binafsi na kuzitumia kwa madhumuni ya taasisi zao. Imependekezwa kuzingatiwa maslahi tofauti ya watendaji na kuimarishwa usimamizi, ukaguzi, tathmini na ufuatiliaji wa karibu katika maeneo ya taarifa za watu pamoja na suala la maadili ya watendaji katika kutoa taarifa za watu wanazozikusanya.

Uchambuzi wa wadau walioshiriki katika utafiti huu ni kama unavyooneshwa na katika majadueli na machati yafuatayo:


## Jadueli Nam. 1 linaonesha Idadi ya washiriki wote na Taasisi walizotoka.

***Jadueli Nam. 1: Idadi ya washiriki wote wa Utafiti.***

| Taasisi za Wadau Walioshiriki | Waliohudhuria | Walioalikwa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| (OR), Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora | 6 | 6 | 100.0 |
| ZAECA | 2 | 2 | 100.0 |
| Idara ya Uhamiaji Zanzibar | 4 | 4 | 100.0 |
| Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | 4 | 4 | 100.0 |
| Tume ya Uchaguzi Zanzibar | 4 | 4 | 100.0 |
| Mfuko wa Barabara | 2 | 2 | 100.0 |
| Jeshi la Polisi | 4 | 4 | 100.0 |
| Mamlaka ya Serikali Mtandao | 6 | 8 | 75.0 |
| Mamlaka ya Usajili wa Matukio ya Kijamii | 6 | 8 | 75.0 |
| Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 2 | 2 | 100.0 |
| Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Pemba | 2 | 2 | 100.0 |
| TTCL Pemba | 2 | 2 | 100.0 |
| Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba | 2 | 2 | 100.0 |
| Mamlaka ya Mapato Zanzibar - Pemba | 2 | 2 | 100.0 |
| Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | 4 | 4 | 100.0 |
| Chuo Kikuu cha Taifa - SUZA | 2 | 2 | 100.0 |
| Benki ya Watu wa Zanzibar | 4 | 4 | 100.0 |
| OR, Fedha na Mipango | 2 | 2 | 100.0 |
| Makampuni ya Simu za Mkononi | 9 | 10 | 90.0 |


| | | | |
|---|---|---|---|
| Mahkama | 2 | 2 | 100.0 |
| Shirika la Umeme | 2 | 2 | 100.0 |
| Mamlaka ya Mapato Tanzania - Pemba | 2 | 2 | 100.0 |
| Mamlaka ya Uwekezaji | 2 | 2 | 100.0 |
| Taasisi Binafsi na Makampuni | 8 | 10 | 80.0 |
| Wadau wa Masuala ya Uchakataji Taarifa | 8 | 9 | 88.9 |
| Watafiti | 4 | 4 | 100.0 |
| Wataalamu wa Mifumo | 8 | 9 | 88.9 |
| Asasi za Kiraia | 12 | 14 | 85.7 |
| **JUMLA** | **117** | **128** | **91.4** |

***Chati Nam.1: Mchanganuo wa washiriki kwa Jinsia***





Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, **asilimia (66.7%)** ya washiriki walikuwa wanaume na **asilimia (33.3%)** walikuwa wanawake. Washiriki wanawake walikuwa wachache kutokana na ukweli kwamba masuala ya mifumo na utaalamu katika uchakataji wa taarifa na masuala ya ICT na wakuu katika taasisi mbali mbali zinashughulika na taarifa binafsi zimeshirikisha wanaume wengi kuliko wanawake.

*Chati Nam. 2: Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu*




Matokeo yanaonesha kuwa **asilimia (6.0%)** ya washirki wana elimu ya sekondari, **asilimia (27.4%)** walikuwa na elimu baada ya Sekondari na **asilimia (66.7%)** walikuwa na elimu ya juu kuanzia Digirii ya kwanza na kuendelea. Lengo kubwa la kufanya uchambuzi huu, ni kuonesha kwamba maoni katika utafiti huu umezingatia wadau wenye elimu tofauti kwa lengo la kupata michango yao kutokana na eneo hili kuwa na changamoto katika usimamizi na ulinzi wa taarifa za watu binafsi.


*Chati Nam.3: Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri.*




Utafiti umezingatia kipengele muhimu katika uchambuzi cha eneo la umri wa wadau, ambapo kundi lenye umri kati ya **miaka 15 hadi 24** ambalo ni kundi la vijana limeshirikishwa kwa **asilimia (20.5%),** kundi la watu wenye umri kati ya **miaka 25 hadi 60** ambao ni tegemezi katika kukuza uchumi na maendeleo ya nchi limeshirikishwa kwa **asilimia (75.2%)** na kundi la mwisho ni kundi la wazee wenye umri kuanzia **miaka 60 na zaidi** ambao ni watu wenye uzoefu na

wastaafu katika eneo la uwekaji wa taarifa za watu binafsi na ambao wamefanya kazi kabla ya mifumo ya kisasa limeshirikishwa kwa **asilimia (4.3%)** katika utafiti huu.

Aidha, utafiti umebainisha na kuonesha makundi yalioshirikishwa kutoka katika taasisi mbali za Serikali na binafsi na taasisi nyengine katika masuala ya ulinzi wa taarifa, ukusanyaji, utafiti na uchakataji pamoja wataalamu na wadau wengine kutoka Asasi za Kiraia.




Katika utafiti huu, wadau kutoka taasisi za Serikali walishirikishwa kwa **asilimia (45.0%),** ikifuatiwa na wadau kutoka taasisi binafsi na asasi za kiraia **asilimia (34.8%)**, wataalamu wa mifumo ya kielektroniki walikuwa **asilimia (12.0%)** na wadau wengine pamoja na watafiti ni **asilimia (8.2%).**

## 6.4 Matokeo ya Utafiti

### 6.31 Matokeo ya Kisera.

**(a) Haja ya Kuwa na Sera ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.**

Kupitia maoni ya wadau wengi muhimu katika suala zima la ulinzi wa taarifa binafsi ambao wameshiriki katika vikao mbali mbali, ipo haja ya kutungwa kwa Sera ya kitaifa kwa Zanzibar itakayohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi. Aidha, utafiti umebaini kwamba maoni hayo ya wadau yamependekeza Sera hiyo iainishe;

(i) Mikakati ya kila taasisi inayoshughulikia na uchukuaji wa taarifa.

(ii) Utumiaji na uchakataji wa taarifa binafsi, mipango madhubuti itakayowezesha kufanyika kwa tafiti zinazohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi Zanzibar

Aidha, utafiti umebaini kwamba kuna umuhimu wa sera hiyo kuweka wajibu wa kuanzishwa kwa chombo maalum cha usimamizi na udhibiti wa ulinzi wa taarifa binafsi ambacho kitakuwa ni chombo cha usimamizi na ufuatiliaji.

**(b) Eneo la Ushirikiano katika utoaji wa taarifa**

Imebainika kupitia maoni ya wadau kwamba kuna haja ya Sera kutafsiri na kubainisha maeneo ya uhusiano kwa taasisi za Muungano na Zanzibar zilizopo Zanzibar; pamoja na utendaji na uwasilishaji wa taarifa kwa taasisi za Muungano au za Zanzibar zilizopo Tanzania Bara ili kuondoa changamoto ya

ubadilishaji wa taarifa kwa taasisi za Serikali na binafsi zinazofanya kazi katika pande mbili za Muungano.

## 6.5 Maoni ya Kisheria.

**(a) Kukosekana kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Zanzibar.**

Baada ya kupitia sheria mbali mbali za ndani zinazohusiana na ukusanyaji wa taarifa binafsi za wananchi, utafiti huu umebaini kuwa kuna haja ya kutungwa sheria rasmi ya ulinzi wa taarifa kwa upande wa Zanzibar. Hii ni kutokana na kuwepo kwa taasisi nyingi ambazo zinashughulika na ukusanyaji wa taarifa binafsi za wananchi na hazina muongozo maalum juu ya ulinzi wa taarifa. Hivyo kila taasisi inayokusanya taarifa imeweka utaratibu wake kisheria. Aidha, utafiti huu umebaini pia mikataba mbali mbali ya kimataifa na Kikanda imesisitiza ulinzi wa taarifa katika nchi wanachama kuzitaka kutunga sheria rasmi za ulinzi wa taarifa binafsi.

Sheria hiyo iwe ndio sheria mama ambayo itasimamia taasisi zote zinazokusanya, kutumia na kuzichakata taarifa binafsi za watu pamoja na kusimamia uhamishaji wa taarifa kwenda nje ya Zanzibar. Vile vile, Sheria iyo iweke vifungu vya uawajibikaji wa taasisi hizo pamoja na uadilifu katika kutekeleza majukumu ya taasisi katika kukusanya, kutumia na kuchakata taarifa za watu pamoja na utaratibu wa makosa na adhabu.

**(b) Ufafanuzi wa Maneno Muhimu katika Sheria.**

Utaiti huu umebaini kwamba kuna haja ya kubainisha, tafsiri ya maneno ili kuondoa mgongano wa uelewa kupitia maana ya maneno kama vile “maana ya taarifa binafsi”, “maana ya ulinzi wa taarifa”, “maana ya taarifa binafsi nyeti” na “maana ya taarifa binafsi za kawaida “wachakata taarifa”, “wahifadhi taarifa”, “wadhibiti wa taarifa”, “Mikataba ya utoaji taarifa”, “taarifa za afya” na “mawasiliano”.

Aidha, kupitia uzoefu wa sheria za ulinzi wa taarifa binafsi katika nchi mbali mbali, utafiti umebaini kwamba baadhi ya maneno muhimu yaliyotumika katika sheria zao yamefanikiwa na kuwekewa tafsiri maalum. Miongoni mwa maneno muhimu ambayo utafiti huu umebaini katika sheria mbali mbali yakifafanuliwa ni pamoja na “afisa ulinzi wa taarifa binafsi”, “kanuni za maadili”, “mahkama”, “mchakataji”, “mhusika wa taarifa”, “mkusanyai”, “mpokeaji”, “mtaalamu wa afya”, “mtoto”, “nyaraka”, “taarifa binafsi”, “taarifa nyeti”, “taarifa za vinasaba”, “usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nchi za nje”, “rejista” n.k.

### (c) Misingi ya Ulinzi wa Taarifa.

Baada ya kufanya utafiti wa kina unaohusiana na ulinzi wa taarifa, utafiti huu umebaini hakuna misingi mikuu ya ulinzi wa taarifa ambayo itahakikisha taarifa zinakuwa katika usalama. Misingi hiyo ni pamoja na kuhakikisha kwamba taasisi ambazo zitakua na jukumu la kukusanya, kuchakata na kuhifadhi taarifa; hazipotezi, hazivujishi na wala haziharibu taarifa.

Vile vile, utafiti huu umebaini kuwa uzoefu katika sheria mbali mbali za nchi nyengine ikiwemo sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi ya Tanzania, zimeweka utaratibu wa kisheria juu ya misingi ya ulinzi wa taarifa. Misingi yenyewe ni kama vile kuhakikisha taarifa zinachakatwa kihalali, kwa haki na uwazi, taarifa zinakusanywa kwa madhumuni mahsusi, ziwe zinatosheleza na ni muhimu kwa madhumuni ya uchakataji, ziwe sahihi, ziwe zinahifadhiwa kwa muda usiozidi unaohitajika, ziwe zinachakatwa kwa kuzingatia haki ya muhusika na usalama wa taariffa zake pamoja na kutosafirishwa nje ya mipaka ya nchi kinyume na sheria. Hivyo, utafiti huu umebaini kuwa sheria zetu za ndani ambazo zinahusiana na ukusanyaji wa taarifa binafsi za wananchi, hazikuzingatia misingi mikuu ya ulinzi wa taarifa.

### (d) Taarifa ambazo hazitabanwa na masharti ya Sheria

Utafiti umebaini kwamba taasisi za taarifa Zanzibar, hazijapewa masharti na taratibu kwa taarifa ambazo hazitahusika au zinaweza taasisi inaweza kutoa ila ya masharti ya Sheria. Maeneo hayo ni kama ubadilishaji wa taarifa baina ya taasisi za Serikali, matumizi ya nyumbani, au taarifa kwa ajili ya matumizi ya ajira n.k.

### (e) Aina za Taarifa zinazopaswa Kulindwa Kisheria.

Utafiti huu pia, umebaini kuwa kuna aina mbili za taarifa ambazo zinapaswa kulindwa kisheria ambazo ni taarifa binafsi na taarifa binafsi nyeti. Kwa upande wa taarifa binafsi, utafiti huu umebaini kwamba masuala yanayojumuishwa ni

(i) rangi,

(ii) asili ya kitaifa au kikabila,

(iii) dini,

(iv) umri au

(v) hali ya ndoa ya mtu binafsi,

(vi) taarifa binafsi zinazohusu elimu,

(vii) historia ya matibabu,

(viii) jinai,

(ix) ajira au

(x) miamala ya kifedha ya mtu binafsi;

(xi) namba yeyote ya utambulisho, alama au

(xii) namna nyingine maalum inayomtambulisha mtu binafsi;

(xiii) anwani,

(xiv) alama za vidole au

(xv) kundi la damu la mtu binafsi;

(xvi) jina la mtu binafsi linaloonekana katika taarifa binafsi za mtu mwengine anayehusiana naye au

(xvii) pale ambapo ufichuzi wa jina hilo utadhihirisha taarifa binafsi za mtu.

Aidha, utafiti huu umebaini mifano ya taarifa nyeti inajumuisha taarifa ya vinasaba, taarifa inayohusu watoto, taarifa inayohusu makosa, hukumu za jinai au hatua za kiusalama, taarifa za kibayometriki, ikiwa imechakatwa ni taarifa binafsi inayoonesha asili ya rangi au kabila, itikadi za kisiasa, imani za kidini au kifalsafa, ushirika, uanachama wa vyama vya wafanyakazi, jinsia na taarifa za kiafya au mahusiano ya kingono; na taarifa binafsi yoyote ambayo kwa mujibu wa sheria inachukuliwa kuwa ina athari kubwa kwa haki na maslahi ya muhusika wa taarifa.

### (f) Kuanzishwa kwa Chombo cha Usimamizi wa Ulinzi wa Taarifa.

Utafiti huu umebaini kwamba hakuna zimeanzisha chombo maalum cha usimamizi wa taasisi zote ambazo zitakua na jukumu la kukusanya na kuchakata taarifa binafsi za wananchi wao kilichoanzishwa. Vyombo ambavyo vinasimamiwa na wasimamizi maalum ambao huteuliwa kwa lengo la kusimamia vyombo hivyo kisheria. Kwa mfano, sheria ya ulinzi wa taarifa ya Tanzania, Ghana na Kenya, zimeanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na kwa upande wa Mauritius na Zambia zimeanzisha ofisi maalum ya ulinzi wa taarifa.

Aidha, utafiti huu umebaini kuwa vyombo hivyo vina majukumu ya kufuatilia utekelezaji wa Sheria kwa wakusanyaji; kusajili wakusanyaji na wachakataji kwa mujibu wa Sheria; kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu; kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya jambo lolote ambalo Tume au chombo hicho itaona linaathiri ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu; kutoa elimu kwa umma kwa kadri itakavyofaa kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria.

### (g) Usajili wa Wakusanyaji wa Taarifa.

Utafiti huu umebaini kuwa sheria za nchi mbali mbali, zimeweka utaratibu wa kisheria wa kufanya usajili kwa mtu yeyote au taasisi zozote zinazojihusisha na ukusanyaji uchakataji au uhifadhi wa taarifa binafsi nchini, ili kupata uwezo wa

kisheria wa kuweza kukusanya, kuchakata au kuhifadhi taarifa binafsi za wananchi.

Imebainika kwamba kwa Zanzibar hakuna chochote kilichosajili au kinachotambua taasisi za Serikali na ninafsi zinazohusika na utoaji taarifa. Aidha, mipaka, taratibu na mifumo ya taasisi hizo haijawekewa utaratibu mzuri na usimamizi.

**(h) Haki na Wajibu wa mtoa taarifa.**

Kupitia utafiti huu, Tume imebaini kuwa uzingatiaji wa Katiba na Mikataba mbali mbali imeainisha haki za kisheria katika Sheria za ulinzi wa taarifa.

Miongoni mwa haki hizo ambazo utafiti huu umeona kupitia sheria hizo ni pamoja na haki ya mtoa taarifa kupewa taarifa juu ya matumizi ya taarifa zake na muda wa kuzitumia taarifa hizo. Aidha, suala la idhini ya kukubali taarifa zake kutumika katika masuala hayo linazingatiwa, kama haki ya msingi.

Imebainika kuwepo kwa mazingira yanayofanya taarifa hizo zitolewe bila ya ridhaa, iwapo taarifa binafsi za mtu zitatakiwa katika vyombo vya kesi za jinai kama vile Jeshi la Polisi, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahkama.

Aidha, wajibu mwengine ambao utafiti huu imebaini ambayo inaweza kupelekea kutolewa kwa taarifa za muhusika bila ya ridhaa yake ni pamoja na

taarifa hizo kuhitajika kwa maslahi ya umma, takwimu za Serikali, kuelezea historia ya nchi.

Kuhusiana na wajibu wa watoa taarifa, imebainika kwamba wajibu unaojumuishwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa taarifa anayoitoa ni ya ukweli na sahihi pamoja na kufanya matumizi sahihi ya mitandao kwa mfano, Kutokutuma picha, video, sauti au vitu vyengine mitandaoni ambavyo vitamtambulisha mwenyewe.

**(i) Utaratibu wa Kusafirisha Taarifa Nje ya Nchi.**

Katika kupitia mikataba mbali mbali pamoja na uzoefu wa Sheria za ulinzi wa taarifa binafsi, utafiti huu umebaini uwepo wa maelezo ya utaratibu wa uhalali wa kusafirisha taarifa za mtu nje ya mipaka ya nchi, namna ya kusafirisha taarifa za mtu binafsi pamoja na mambo muhimu ya kuzingatia katika kusafirisha taarifa hizo.

Imebainika katika usafirishaji, kuna mambo ya msingi ya kuzingatia kama kuhakikisha kuwa nchi ambayo zinapelekwa taarifa hizo zina usalama na isiyo na sifa ya migongano ya kisiasa na kichumi na nchi nyengine, nchi iwe na sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi au iwe na utaratibu wa kufunga makubaliano baina ya nchi inayosafirisha taarifa na inayopokea kuhakikisha ulinzi wa taarifa hizo.

Mambo mengine yaliobainika ni uwepo wa tathmini juu ya umuhimu wa kusafirisha taarifa hizo kwa maslahi ya umma kabla ya kusafirisha taarifa pamoja na kuhakikisha kuwa mpokeaji wa taarifa hizo atazichakata kwa lengo mahsusi lililokusudiwa na si vyenginevyo.

## (j) Suala la Kimaadili kwa Wakusanyaji wa Taarifa.

Utafiti huu umebaini kuwa eneo hili linahitaji kuwekewa utaratibu wa kuweka maadili, utaratibu wa maadili kwa wapokeaji na wachakataji wa taarifa binafsi katika sheria zao.

Miongoni mwa maadili ambayo utafiti huu umebaini ni kutumia taarifa kwa usahihi katika hatua zote ikiwemo wakati wa kuzipokea, kuzichakata na kuzihifadhi; vilevile kuweka maadili ya usiri kwa wapokeaji taarifa kwa kutozivujisha taarifa au kuziuza; na kuweka utaratibu wa kula viapo kwa wakusanyaji wa taarifa.

## (k) Makosa na Adhabu.

Katika kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi, sheria za nchi mbali mbali za ulinzi wa taarifa binafsi zimebainika kupitia utafiti huu kuwa zimeweka utaratibu wa orodha ya makosa yote yanayohusiana na ulinzi wa taarifa. Miongoni mwa makosa hayo ni ufichuaji wa taarifa binafsi kinyume na sheria,uharibifu wa taarifa, ufutaji, ufichaji au ubadilishaji wa taarifa binafsi kinyume na sheria. Aidha, sheria hizo zimebainika kuweka utaratibu wa makosa pale ambapo kosa litakua limetendwa na kampuni au shirika, kampuni au shirika hilo na kila afisa

ambaye kwa kujua au kwa makusudi anaidhinisha ukiukwaji wa sheria atawajibika kwa kosa hilo.

### (l) Haki ya rufaa kwa wakusanyaji wa taarifa.

Katika kupitia uzoefu wa sheria za nchi mbali mbali za ulinzi wa taarifa, utafiti huu umebaini kuwa sheria za nchi nyingi zimeweka utaratibu wa rufaa kwa wakusanyaji wa taarifa pale ambapo mtu binafsi au taasisi inayoshughulika na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa, mtu huyo au taasisi hiyo itakapokataliwa kufanyiwa usajili na kupewa cheti cha ukusanyaji wa taarifa, na ikatokea hawakuridhika na maamuzi hayo ya chombo hicho maalum chenye mamlaka hayo, wanaweza kuwasilisha maombi ya rufaa kwa njia ya maandishi, ambayo nchi kama Tanzania inapeleka rufaa kwa waziri, nchi kama mauritios imebainika kuwa wanakata rufaa katika tribunal ya ulinzi wa taarifa.

Aidha, utafiti huu umebaini pia, wakusanyaji wa taarifa katika nchi nyingi wana haki ya rufaa dhidi ya hatua zozote za kiutawala chini ya chombo husika kinachosimamia ulinzi wa taarifa ikiwa ni pamoja maelekezo yaliyotolewa katika notisi ya adhabu kuhusiana na makosa ya ulinzi wa taarifa, na ikiwa hataridhika na maamuzi hayo ataweza kukata rufaa, ambapo nchi kama Tanzania Zambia na Caribian watakata rufaa katika mahkama kuu.

### (m) Kuweka utaratibu wa kudhibiti wa mitandao ya kijamii katika ulinzi wa taarifa.

Utafiti huu umebaini kwamba hakuna utaratibu wa kisheria uliowekwa kudhibiti mitandao ya Kijamii katika ulinzi wa taarifa. Imebainika matumizi ya mtandao yanaathiri taarifa binafsi. Imebainika kwamba vyombo na Sheria zinaweka udhibiti katika hili.

**(n) Utaratibu wa Kuharibu Taarifa.**

Utafiti huu umebaini kwamba hakuna utaratibu wa kisheria wa kuharibu taarifa binafsi lazima uwekewe muda maalum katika matumizi. Kuhifadhi baadhi ya taarifa binafsi za watu kwa muda mrefu jambo ambalo sahihi na linaweza kupelekea mambo mbalimbali yatokee.

Aidha, utafiti umebaini pia, katika nchi nyingi kwenye Sheria zao za ulinzi wa taarifa zimeweka utaratibu kwa wakusanyaji wa taarifa kuharibu taarifa binafsi kwa njia yoyote ambayo haitapelekea taarifa hizo kuvuja kwa mtu mwengine mara baada ya kumalizika kwa matumizi ya taarifa hizo isipokua kwa dharura maalum za kisheria kama vile kuendelea kuhifadhiwa kwa ajili ya maslahi ya umma, au katika kuweka takwimu za serikali nakadhalika.

**(o) Utaratibu wa Kukusanya Taarifa za Watu Maalum.**

Katika kupitia sheria za nchi mbali mbali za ulinzi wa taarifa binafsi, utafiti huu umebaini kuwa sheria za nchi kama vile Zambia, zimeweka utaratibu wa kukusanya taarifa za watoto na watu maalum kupitia wasimamizi wao wa kisheria kutoa taarifa zao pamoja na kuwawakilisha katika ridhaa ya maamuzi ya taarifa zao zote kwa niaba yao. Imebainika kwamba dhana hii inajumuisha,

wagonjwa wa akili pamoja na wagonjwa waliopo katika hali mbaya sana na ambao hawawezi kujitolea maamuzi au kutoa taaria zao pamoja walemavu wa kusikia na mabubu pale ambapo kutakuwa na ulazima wa kuwakilishwa katika kutoa taarifa zao kutoka kwa wawakilishi wao kwa mujibu wa sheria.

**(p) Kuanzishwa kwa Kamati.**

Utafiti huu pia umebaini kuwa, baadhi ya sheria kama vile Sheria ya ulinzi wa taarifa ya Mauritius, imeweka utaratibu wa kuanzisha kamati za ushauri ambazo hukishauri chombo cha usimamizi wa taasisi za wakusanyaji na wachakataji wa taarifa katika yale masuala yote muhimu ya kuweka ulinzi wa taarifa pamoja na mikakati ya usimamizi bora kwa taasisi zilizosajiliwa kupokea taarifa.

Imebainika kwamba Kamati hizi pia htumika kama vyombo vya ushauri kwa Kamisheni na taasisi za usimamizi wa taarifa binafsi.

## SURA YA SABA

## 7.0 MAPENDEKEZO YA TUME NA HITIMISHO

### 7.1 Utangulizi

Sura hii imejielekeza katika kutoa mapendekezo ya Tume kutokana na yaliyojitokeza katika utafiti huu. Mapendekeo haya ni majumuisho ya matokeo ya ukusanyaji wa taarifa na maelezo kwa maeneo yaliyotumika kufanyiwa utafiti huu, kwa kuangalia sheria na uzoefu wa nchi mbali mbali, Mikataba ya Kimataifa, sheria, sera na miongozo inayohusiana na utafiti huu pamoja na maoni ya wadau. Tume baada ya kufanya utafiti huo, inakuja na mapendekezo mbali mbali ya kisera, kisheria pamoja na mapendekezo ya kiutendaji.

### 7.2 Mapendekezo:

#### 7.2.1 Mapendekezo ya Kisera:

Tume inapendekeza kutungwa Sera ambayo itajumuisha maeneo muhimu ya kusimamia ulinzi wa taarifa binafsi. Maeneo ya jumla ambayo inapendekezwa Sera izingatie ni pamoja na:

**(a) Kuwekwa usimamizi wa ulinzi wa taaarifa binafsi.**

Tume inapendekeza kuwa Sera itakayotungwa itambue na kubainisha haja ya kutungwa kwa sheria mahsusi ya ulinzi wa taarifa binafsi ili kulipa nguvu ya kisheria suala hili la kuzilinda taarifa binafsi dhidi ya matumizi mabaya yanayoweza kuleta athari kwa wenye taarifa hizo.

### (b) Miongozo ya usimamizi wa ulinzi wa taarifa binafsi

Tume inapendekeza kuwa, kwa kuzingatia umuhimu wa kipekee wa usimamizi wa ulinzi wa taarifa binafsi, miongozo mizuri inahitajika kuwekwa kwenye Sera, kwa ajili ya kuwasimamia wachukuaji wa taarifa, wadhibiti, wachakataji pamoja na watoa taarifa ili kuwe na mfumo bora wa uhakika wa ulinzi na udhiti wa taarifa zinazotolewa. Aidha, inapendekezwa Sera hii iainishe mambo muhimu ya ulinzi ikiwemo miongozo ya usiri na miongozo ya ulinzi.

### (c) Mikakati ya usimamizi wa ulinzi wa taarifa binafsi

Kutokana na kuwepo kwa changamoto nyingi katika uvujaji na wizi wa taarifa binafsi duniani, Tume inapendekeza kuwa Sera ya ulinzi wa taarifa binafsi iainishe mikakati ya msingi itakayotumika kusimamia kila taasisi inayoshughulikia uchukuaji, udhibiti, utumiaji na uchakataji wa taarifa binafsi.

### (d) Wajibu wa kuanzishwa kwa chombo cha usimamizi wa ulinzi wa taarifa binafsi

Tume inapendekeza kuwa Sera itakayotungwa ibainishe haja ya kuanzishwa kwa chombo ambacho kitasimamia ulinzi wa taarifa binafsi pamoja na kufanya ufuatiliaji kwa taasisi ambazo zinachukua, kudhibiti, kuchakata na kutumia taarifa ili kuhakikisha kuwa misingi na mikakakti ya ulinzi wa taarifa binafsi inafikiwa.

**(e) Ubadilishanaji wa taarifa Zanzibar na Tanzania Bara.**

Tume inapendekeza Sera iweke msingi wa mashiriano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara katika ubadilishanaji wa taarifa. Aidha ielezwe mipaka, mamlaka na utaratibu wa kupeana taarifa baina ya taasisi moja na nyengine.

**(f) Mipango madhubuti ya Kufanya tafiti**

Tume inapendekeza Sera iweke mipango madhubuti itakayowezesha kufanyika kwa tafiti zinazohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi ili kuweza kuendana na ukuaji wa teknolojia na kuweza kuwa na mbinu mpya zinazolingana na teknolojia katika ulinzi wa taarifa binafsi.

**(g) Mamlaka ya Kisera itakayosimamia taasisi ya ulinzi wa taarifa binafsi**

Tume inapendekeza kuwa Sera ibainishe kwa uwazi mamlaka ya Kisera, kwa maana ya Wizara itakayosimamia masuala ya ulinzi wa taarifa binafsi ili kuupa nguvu Ulinzi wa taarifa binafsi.

Tume inapendekeza kuanzishwa kwa sheria maalum itakayosimamia ulinzi wa taarifa binafsi pamoja na kuweka utaratibu maalum wa kuwasimamia

wakusanyaji wa taarifa, wadhibiti na wahifadhi wa taarifa, wachakataji wa taarifa pamoja na kutoa ulinzi kwa watoaji wa taarifa. Aidha, ukusanyaji wa taarifa binafsi za wananchi unafanyika kupitia taasisi za Serikali na binafsi hivyo, ni vyema kukawa na Sheria ambayo itatoa ulinzi wa taarifa binafsi za wananchi zinazochukuliwa na taasisi hizo.

### (h) Majukumu ya taasisi mbali mbali katika ulinzi wa taarifa

Tume inapendekeza kuwa Sera ibainishe majukumu ya taasisi mbali mbali katika ulinzi wa taarifa binafsi kwa kutambua kuwa kuiachia Taasisi inayoanzishwa pekee katika ulinzi wa taarifa binafsi hakuwezi kuleta tija na kufikia malengo yaliyokusudiwa. Miongoni mwa taasisi zilizopendekezwa kubainishwa majukumu katika ulinzi wa taarifa binafsi ni pamoja na Wakala wa Serikali mtandao, Wakala wa Miundombinu ya Tehama, Wizara husika, taasisi binafsi na asasi za kiraia.

### (i) Kuzingatia mikataba ya kimataifa kuhusu ulinzi wa taarifa

Tume inapendekeza kuwa Sera itambue na kubainisha wajibu wa kuzingatia mikataba ya kimataifa inayohusu ulinzi wa taarifa binafsi ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekubali na kuridhia.

Kwa ujumla, Tume inapendekeza Sheria hiyo izingatie mambo yafuatayo:

(i) Vifungu vya jumla vitakavyozingatia misingi ya sheria, mamlaka ya sheria, na vifungu vyengine vya utangulizi;

(ii) Uanzishwaji wa chombo maalum cha usimamizi wa ulinzi wa taarifa binafsi;

(iii) Utendaji kazi wa chombo maalum cha usimamizi; uwezo wake;uongozi wake sifa za watendaji wake, maadili ya watendaji wake, majukumu ya watendaji wake na masharti ya utaalamu kwa watendaji wa chombo hicho;

(iv) Usimamizi na udhibiti wa wachukuaji taarifa; wadhibiti wa taarifa na wachakataji wa taarifa;

(v) Usajili wa taasisi zinazokusanya, kudhibiti, kuchakata na kutumia taarifa;

(vi) Masuala ya taratibu za usajili na utoaji leseni kwa wakusanyaji, wadhibiti, wachakataji na watumiaji wa taarifa binafsi;

(vii) Mikakati ya ulinzi wa taarifa binafsi;

(viii) Aina za taarifa na ulinzi wake;(taarifa za kawaida na taarifa nyeti);

(ix) Uhamishaji wa taarifa ndani na nje ya nchi na taratibu zake;

(x) Haki za mtoa taarifa;

(xi) Fidia iwapo haki za mtoa taarifa zitavunjwa;

(xii) Makosa na Adhabu;

(xiii) Maadili kwa wakusanyaji, wachakataji, wadhibiti pamoja na wasimamizi wa taarifa binafsi;

(xiv) Mkaguzi na majukumu yake;

(xv) Wajibu wa kuharibu taarifa binafsi baada ya matumizi;

(xvi) Kulinda taarifa za watoto na watu wenye wazingira magumu.

### 7.2.2 Mapendekezo ya Kisheria:

**1. Kuundwa kwa chombo cha kusimamia Ulinzi wa taarifa binafsi**

Tume inapendekeza kuwekwa kwa masharti ya kisheria ya kuanzishwa Chombo huru ambacho kitasimamia ulinzi wa taarifa binafsi, inapendekezwa masharti hayo yajumuishe muundo wa chombo hicho, uwezo, majukumu,

malengo, sifa za watendaji wake, nidhamu na maadili. Tume inapendekeza Chombo hicho kiitwe Tume ya Ulinzi wa Taarifa binafsi.

Aidha, inapendekezwa majukumu ya Tume hiyo yajumuishe:

(a) Kusimamia taasisi zinazokusanya, kudhibiti au kuchakata taarifa ili taasisi hizo ziweze kusimamia malengo yao na kuhakikisha zinafanya wajibu wao ukiwemo ya kuwajengea uaminifu wanaotoa taarifa zao.

(b) Kuhakikisha kuwa taasisi zinazokusanya, kudhibiti au kuchakata taarifa zinatoa uhakika wa ulinzi kwa watoa taarifa (declaration) kuwa taarifa zinazokusanywa zitatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa tu.

(c) Kusajili wachukuaji, wadhibiti na wachakataji wa taarifa binafsi nchini.

(d) Kuweka masharti na sifa zinazofaa kusajiliwa kwa mchukuaji wa taarifa, mdhibiti na mchakataji wa taarifa.

(e) Kusikiliza malalamiko kutoka kwa wananchi pamoja na taasisi zinazokusanya taarifa binafsi na kuchunguza na kutoa maamuzi.

Aidha, Tume ya Kurekebisha Sheria inapendekeza Muundo wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ujumuishe wataalamu wa kada tofauti ambazo zitaweza kusaidia Tume hiyo ya Ulinzi wa taarifa binafsi kufanya kazi zake kwa ufanisi.

## 2. Mikakati ya ulinzi wa taarifa

Inapendekezwa kuwa Sheria iweke mikakati ya ulinzi wa taarifa katika maeneo matatu makuu ambayo ni kuhakikisha taarifa zisiharibike, zisipotee na zisivuje.

Utekelezaji wa mikakati hii utapelekea uwepo wa uhakika katika upatikanaji wa taarifa pamoja na ulinzi wa taarifa binafsi.

**3. Mgawanyo wa taarifa na ulinzi wake**

Tume inapendekeza Sheria iweke mgawanyo wa taarifa kati ya taarifa binafsi za kawaida na taarifa binafsi nyeti.

Aidha, inapendekezwa kuwa ulinzi wa taarifa uendane na aina ya taarifa binafsi, kuwe na masharti maalum kwa ulinzi wa taarifa binafsi nyeti na masharti ya kawaida kwa ulinzi wa taarifa binafsi za kawaida.

**4. Haki na wajibu wa mtoa taarifa binafsi**

Tume inapendekeza Sheria itoe haki kwa mtoa taarifa binafsi ikiwemo

(a) haki ya kuelezwa juu ya matumizi ya taarifa zake;

(b) muda utakaotumika kutumiwa taarifa zake na uhifadhi wa taarifa hizo;

(c) haki ya kushtaki iwapo taarifa zake zitatumika kinyume na makubaliano;

(d) haki ya kulindwa kwa taarifa zake;

(e) haki ya kupata taarifa zake wakati wowote;

(f) haki ya kufahamishwa ikiwa taarifa zake zitahamishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine;

(g) haki ya kupata fidia ikiwa taarifa zake zitavujishwa kwa makusudi;

(h) haki ya kufahamishwa ikiwa taarifa zake zimevuja kwa bahati mbaya.

Aidha, inapendekezwa Sheria hii iweke mazingira ambayo taarifa za mtoa taarifa zitatumika bila ya kuarifiwa iwapo taarifa hizo zitahitajika kwa ajili ya usalama wa taifa, takwimu, mambo ya historia, kukamilisha upelelezi na kwa maslahi ya umma.

Vile vile, inapendekezwa kuwa Sheria iweke wajibu kwa mtoa taarifa binafsi ikiwemo :

(a) Kutoa taarifa zilizo sahihi na za ukweli;
(b) Kutoa taarifa wakati zinapohitajika;
(c) Kufanya matumizi sahihi ya mitandao;
(d) Kutokutuma picha, video au sauti au vitu vyengine mitandaoni ambavyo vitamtambulisha yeye mwenyewe.

**5. Fidia kwa uvujaji wa taarifa**

Tume inapendekeza Sheria iweke utaratibu wa ulipaji wa fidia kwa mtoa taarifa iwapo taarifa zake zitavuja. Aidha, sheria iweke utaratibu wa ulipaji na kuweka wazi mhusika mwenye jukumu la kulipa fidia hiyo.

**6. Uhamishaji wa taarifa ndani na nje ya nchi.**

Tume inapendekeza Sheria iweke utaratibu na masharti juu ya njia za uhamishaji wa taarifa kwa kuzingatia mambo mbali mbali ikiwemo kuwa na makubaliano ya ulinzi wa taarifa baina ya Zanzibar na nchi ambazo taarifa hizo zinahamishiwa (makubaliano hayo yawe kwa mambo ambayo sio ya Muungano), kuwepo kwa utaratibu wa kujulishwa mtu ambaye taarifa zake

zinahamishwa pamoja na kujua taasisi husika inayohamishiwa hizo taarifa pamoja na kuwa na makubaliano ya ulipaji wa fidia iwapo taarifa hizo zitavuja.

Vile vile, inapendekezwa sheria iweke utaratibu maalum na wa wazi utakaotumika kuhamishia taarifa binafsi baina ya taasisi ziliopo ndani ya Tanzania.

**7. Suala la maadili**

Tume inapendekeza sheria iweke Tume ya Udhibiti wa Taarifa Binafsi kuwa ni chombo cha usimamizi wa masuala ya kinidhamu na maadili kwa watendaji wa Tume yenye taasisi za wakusanyaji, wadhibiti na wachakataji wa taarifa.

Maadili yahusishe wajibu wa kutunza siri kwa watendaji wa Tume pamoja na wakusanyaji, wadhibiti na wachakataji wa taarifa na wahamishaji wa taarifa pamoja kuwepo kwa kiapo cha kutunza siri kwa watendaji hao.

**8. Makosa na adhabu**

Tume inapendekeza sheria iweke makosa na adhabu kwa atakayevunja taratibu za ulinzi wa taarifa binafsi. Aidha, inapendekezwa makosa hayo yajumuishe makosa ya kuuza taarifa binafsi, kuzitumia taarifa kinyume na zilivyotakiwa pamoja na kosa la kuvujisha taarifa.

Inapendekezwa sheria iweke makosa ya wakusanyaji taarifa, wadhibiti na wahifadhi wa taarifa pamoja na makosa kwa wachakataji na wahamishaji wa taarifa.

Aidha, kwa upande wa adhabu inapendekezwa sheria iweke adhabu mbali mbali zikiwemo adhabu kwa watendaji na adhabu kwa taasisi moja kwa moja.

**9. Uwepo wa mkaguzi katika eneo la udhibiti wa taarifa binafsi**

Tume inapendekeza sheria impe uwezo Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa taarifa kuteua afisa wake na kuwa mkaguzi katika maeneo ya udhibiti wa taarifa binafsi kulingana na masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

**10. Wajibu wa kuharibu taarifa binafsi**

Tume inapendekeza sheria iweke wajibu kwa wachukuaji, wadhibiti na wachakataji wa taarifa binafsi kuharibu taarifa hizo mara baada ya kukamilika kwa matumizi ya taarifa hizo.

**11. Utaratibu wa ukusanyaji wa taarifa za watoto na watu waliopo kwenye mazingira yenye changamoto**

Tume inapendekeza sheria iweke ulinzi kwa watoto na watu waliopo kwenye mazingira yenye changamoto kwa kutokukusanywa taarifa zao bila ya ridhaa ya watu wanaowasimamia. Watu waliopo kwenye mazingira yenye changamoto kama vile wagonjwa, wazee ambao kutokana na hali zao hawawezi kufanya uamuzi sahihi pamoja na walemavu wa akili.

Aidha, inapendekezwa kuwekwa kwa majukumu na mipaka kwa wanaosimamia na wenye wajibu wa kuzitoa taarifa za watoto na watu wenye mahitaji maalum kama vile wagonjwa, walemavu na wazee.

**12. Utaratibu wa malalamiko na rufaa**

Tume inapendekeza sheria iweke utaratibu maalum wa malalamiko kutoka taasisi mbali mbali zinazohusiana na ulinzi wa taarifa, ili kutoa fursa kwa wananchi kuwasilisha malalamiko yao iwapo taratibu zimekiukwa.

Aidha, sheria iweke taratibu kwa rufaa zinazotokana na wananchi wanaolalamikia taasisi zinazokusanya taarifa binafsi pamoja na utaratibu wa rufaa kutoka kwa taasisi na wakusanyaji wa taarifa dhidi ya wananchi na taasisi nyengine. Vile vile, kuwepo na utaratibu wa rufaa baada ya maamuzi ya Mkuu wa Tume na rufaa baada ya maamuzi ya chombo hiki.

**13. Utaratibu wa kubadilishana taarifa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara.**

Tume inapendekeza kuwepo kwa utaratibu maalum wa kubadilishana taarifa na ujuzi baina ya taasisi za Tanzania Bara na Zanzibar. Taarifa hizo zitolewe kwa kuzingatia masharti maalum yatakayowekwa ili yasikiuke sheria ziliopo.

Aidha, inapendekezwa Waziri husika kutunga miongozo maalum ya usimamizi wa utaratibu wa kubadilishana taarifa muhimu kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.

**14. Usajili wa wakusanyaji,wahifadhi na wachakataji wa taarifa binafsi.**

Tume inapendekeza kuwekwa kwa utaratibu wa kuwasajili na kuwapatia vitambulisho wale wote wanaohusika na ukusanyaji, uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi.

**15. Taafsiri ya maneno**

Tume inapendekeza sheria iweke tafsiri ya maneno kama vile neno ridhaa, maslahi ya umma, taarifa binafsi nyeti na taarifa binafsi za kawaida nakadhalika.

**16. Utolewaji wa elimu.**

Tume inapendekeza sheria iweke utaratibu wa kutolewa elimu kwa wadau muhimu wakiwemo wachukuaji wa taarifa, wahifadhi wa taarifa na wachakataji wa taarifa pamoja na wanachi kwa ujumla. Hatua hii itatoa uelewa wa dhana nzima ya ulinzi wa taarifa binafsi na kuisaidia Serikali katika utekelezaji wake.

Aidha, Tume inapendekeza Taasisi za Serikali zinazohusika na ukusanyaji wa taarifa binafsi kupatiwa elimu na kueleweshwa maadili na wajibu wao katika ulinzi wa taarifa.

#### 7.2.3 Mapendekezo ya Kiutendaji

Kwa upande wa mapendekezo ya kiutendaji Tume inapendekeza yafuatayo:

**1) Ushirikiano baina ya taasisi**

Tume inapendekeza katika kusimamaia ulinzi wa taarifa, Serikali iweke utaratibu maalum na kuratibu ushirikiano baina ya taasisi na mamlaka zote ambazo zitakuwa na wajibu kwa namna moja ama nyengine katika masuala ya ulinzi wa taarifa.

**2) Taasisi ziimarishe ujuzi au taaluma ya teknolojia**

Tume inapendekeza kuwa na mifumo pamoja na teknolojia ya hali ya juu ya utalamu katika ulinzi wa taarifa binafsi. Vile vile, inapendekezwa taasisi husika kuwapatia mafunzo watendaji wao mafunzo ambayo yataendana na teknolojia iliopo ulimwenguni. Hii itasaidia taasisi kuwa na ulinzi imara utakaoepusha uvujaji na wizi wa taarifa binafsi kwa watoa taarifa.

**3) Uwekezaji katika eneo la Ulinzi wa taarifa binafsi**

Ili Tume iliyoundwa iweze kufanya kazi nzuri na kutimiza malengo yaliyokusudiwa, inapendekezwa kuwa Serikali ichukue hatua za uwekezaji

katika ulinzi wa taarifa binafsi. Miongoni mwa maeneo yanayopendekezwa kuwekezwa na Serikali ni pamoja na miundombinu, mfumo ya kisasa ya ulinzi wa taarifa, utaalamu, utafiti na majengo yatakayotumika na ‘’Tume ya ulinzi wa taarifa binafsi.’’

### 4) Kuinua mwamko wa wananchi katika ulinzi wa taarifa binafsi

Kutokana na mwamko mdogo uliopo miongoni mwa wananchi kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi, Tume inapendekeza kuwa taasisi itakayoundwa kusimamia ulinzi huo, ichukue juhudi za kuwahamasisha wananchi kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi ili kujenga uelewa wa kutosha kuhusu dhana hiyo na kusaidia katika mikakati ya kulinda taarifa binafsi.

SMZ

SERIKALI YA ZANZIBAR MAPINDUZI

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

## RIPOTI YA UTAFITI WA MAPITIO YA UTAFITI WA ENEO LA ULINZI NA UHIFADHI WA TAARIFA BINAFSI

## 07 / MWAKA 2023

**INAWASILISHWA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA ZANZIBAR.**